*Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**BUNGE LA TANZAIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Tisa- Tarehe 26 Machi, 2015**

*(Kikao Kilianza Saa 3.00 Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Lediana M. Mng'ong'o) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu hayupo, kwa hiyo na maswali kwa Waziri Mkuu hayatakuwepo leo. Katibu!

**MASWALI YA KAWAIDA**

Na. 94

**Kusuasua kwa Ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma**

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuliza:-

Ujenzi wa Ofisi ya Mkuu ya Mkoa wa Dodoma umeendelea kusuasua kwa muda mrefu.

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka kukamilisha ujenzi wa jengo hili?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Ofisi ya Mkoa wa Dodoma ulianza mwaka 2009/2010 na ulitarajiwa kukamilika mwaka 2012/2013. Makadirio ya gharama ya ujenzi yalikuwa ni shilingi bilioni 15.2, lakini kwa sasa gharama hizo zinafikia shilingi bilioni 16.9. Kati ya fedha hizo Serikali imeshatoa shilingi bilioni 10.5. Utekelezaji wa mradi huu unafanyika kwa awamu, ambapo awamu inayoendelea ni ya nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zinazofanyika ni ujenzi wa msingi, ujenzi wa mihimili mikuu ya jengo na msingi wa ujenzi wa ukumbi. Aidha, kazi zinazotekelezwa katika awamu ya nne ni ujenzi wa kuta, uwekaji wa milango na madirisha na mwendelezo wa kazi za umeme katika hatua ya ufungaji wa nyaya. Kazi nyingine zitakuwa ni ufungaji wa mfumo wa habari na mawasiliano yaani *ICT* awamu ya pili, umaliziaji katika sakafu hadi ghorofa ya pili na kuta za jengo lote, kukamilisha ujenzi wa ukumbi na kazi za mwanzo za mandhali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu hii ya nne ilianza kutekelezwa tarehe 25/6/2014 na imepangwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi saba. Katika bajeti ya mwaka 2014/2015 zimetengwa shilingi bilioni tatu tayari Serikali imekwishatoa shilingi 1,104,413,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa ya ujenzi huo kuchukua miaka mitano badala ya miaka mitatu ni ufinyu wa bajeti inayotolewa kwa ajili ya kazi hiyo na fedha kutopelekwa katika muda muafaka. Hata hivyo, utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kukamilika mwaka huu wa fedha 2014/2015. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI imeiandikia Wizara ya Fedha barua yenye Kumb Na. AB.39/156/01/114 ya terehe 19 Februari, 2015, kuikumbusha Wizara ya Fedha kutoa fedha za miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unaposema kwamba Dodoma ni Makao Makuu ni pamoja na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, jengo hili liliwahi kutembelewa na Kamati ya TAMISEMI na wakaiomba Serikali kwamba jengo hili sasa litengewe fedha za kutosha na jengo liweze kukamilika. Pamoja na kwamba tangu jengo hili lianze kujengwa kuna majengo mengi ya Serikali yameshakamilika, lakini Ofisi ya Mkuu wa Mkoa mpaka leo jengo hili linasua sua. Serikali inasema kwamba mradi huu utakamilika mwaka 2014/2015, lakini katika mwaka huu wa fedha Serikali imepeleka shilingi milioni 400 tu. Siyo kweli kwamba jengo hili litakamilika katika mwaka huu. Naomba kujua ni lini sasa Serikali angalau ipeleke shilingi bilioni tatu kama zilivyoombwa na Mkoa na kama Kamati ya TAMISEMI ilivyoomba?

Swali la pili, kwa kuwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imeonesha nia na ina uwezo wa kusaidiana na Serikali yetu kukamilisha baadhi ya majengo ambayo Serikali itakubali kudhamini. Kwa mfano, *NSSF, National Housing, PSPF* na Mifuko mingine wakidhaminiwa na Serikali wana uwezo wa kukamilisha majengo yaliyokwama kama la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Je, Serikali iko tayari kuidhamini Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wakajengewa na Mashirika haya na Hifadhi ya Jamii?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa ajili ya *records*, sasa hivi hapa natoka kwenye hiyo Ofisi inayozungumzwa na nimemwita Katibu Tawala wa Mkoa tulikuwa wote pale, Ndugu Rehema Madenge pamoja na watu wote wanaohusika na jambo hili tunalozungumza hapa. Tumekuwa tunafanya hivyo, tumekaa Ofisini tumezungumza nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niweke *record* vizuri, shilingi milioni 400 ambazo tumezitamka leo asubuhi hii nimethibitishiwa kwamba shilingi milioni 700 zimeingia wiki hii, ndiyo maana nataka nisahihishe takwimu zile ambazo zimeorodheshwa pale Mheshimiwa Bura achukue na nimemtaja mtu, hapa nimekuwa *concrete*, maana nimemtaja Katibu Tawala wa Mkoa, anaweza aka-*cross check* naye. Kwa hiyo, hela zilizokwenda kule ni bilioni moja milioni mia moja na nne ndizo ambazo zimeshaingia na wanazo *which means* kazi zitaendelea pale, nilitaka kusema hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hela ambazo zilitakiwa ziwe zimekwenda kwa ajili ya kazi yote hii kama hela zote zingekwenda kama zinavyotakiwa, zilikuwa ni shilingi bilioni kumi na sita na *point*. *So far* tumepeleka shilingi bilioni 10.5 ndizo zimeshapelekwa pale na kwa sababu ya *inflation rate* na vitu vingine hapa na kwa sababu watataka kuweka *parking area* na vitu vingine, wanahitaji shilingi bilioni 18 ambazo zinatakiwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nimwambie Mheshimiwa Bura kwamba, nathamini sana, Mbunge huyu amekuwa anasukuma hili jambo kwa nguvu, ni haki yake kwa kweli afanye hivyo na tunamshukuru kwamba anafanya hivyo. Hata hivyo, nataka nimwambie kwamba dhamira ya Serikali iko pale pale, ilikuwa shilingi bilioni tano ndizo zilikuwa zinapelekwa pale, sasa hivi tunapeleka shilingi bilioni tatu. Kwa maneno kwamba kama hela tulizopeleka hapa sasa hivi ni shilingi bilioni 1.104, maana yake tunategemea kwamba tupeleke tena shilingi bilioni mbili na *point*. Ndiyo maana tumesema kwamba tutazungumza na Hazina na wamo humu ndani wanatusikia tukisema jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba ile inayojengwa pale ni nyumba yenye heshima kubwa, kwa maana ya kwamba siyo tu Ofisi ya Mkuu wa Mkoa itakuwa kule, kama kuna Wizara ambayo itakuwa ina tatizo la ofisi wanaweza wakapata pale. Kwa hiyo, ile inaitwa *Government House* ndiyo jina lake hasa, ni nyumba ya Serikali iko pale. Kwa hiyo, Mheshimiwa Felister Bura anazungumza kitu cha msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ameleta hii *aspect* hapa, kwamba labda tungetumia *LAPF, NSSF, National Housing* wakatusaidia. Ninyi wote mnajua jambo hili, anayetakiwa kusema naam mimi nipo tayari, kudhamini jambo hili ni Wizara ya Fedha, siyo *LAPF* aseme niko tayari, *NSSf* aseme niko tayari au *NHC* aseme niko tayari, wao Wizara ya Fedha ndiyo wako humu ndani, ili hela hizi kama hazitalipwa atakayekuwa *held responsible* atakuwa ni Serikali na Mifuko hii imekuwa na kelele mnaifahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuhakikishia nachukua wazo hili analolisema hapa, wamefanya hivyo Hombolo kwenye Chuo cha Serikali za Mitaa, tumefanya hivyo kwenye jengo hili, tumefanya hivyo *UDOM*. Kwa hiyo, ni jambo ambalo linawezekana tunaweza tukasema. Sasa hili litategemeana na Wizara ya Fedha itakavyofanya, lakini nakubaliana na mawazo mazuri aliyotoa Mheshimiwa Mbunge na tutayafanyia kazi.

Na 95

**Mchango kwa Ajili ya Kuandikisha Mwanafunzi**

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA (K.n.y. MHE. JOSHUA S. NASSARI)** aliuliza:-

Wazazi wanatozwa fedha pindi wanapokwenda kuwaandikisha watoto shuleni kama wanavyofanya Shule ya Msingi Upendo iliyopo Nsengony Kata ya King'ori.

(a) Je, michango hiyo inayotozwa kwa wazazi ni halali?

(b) Kama ni halali, je, ni kiasi gani cha fedha anachopaswa kulipa mzazi kwani kiwango kinatofautiana baina ya shule na shule?

(c) Kama si halali, je, Serikali inachukua hatua gani za kisheria dhidi ya walimu wanaokwamisha watoto wasipate haki yao ya Kikatiba?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joshua Samweli Nassari, Mbunge wa Arumeru Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Waraka wa Elimu Namba Nane (8) wa mwaka 2011, imetoa maelekezo kuwa uandikishaji wa wanafunzi kujiunga na darasa la kwanza au kidato cha kwanza unapaswa kufanywa bila masharti yoyote. Hivyo, michango yote inayotozwa wakati wa mwanafunzi kujiandikisha kuanza shule ni kinyume na taratibu na imepigwa marufuku. Hivyo, kimsingi hakuna kiasi chochote cha fedha ambacho mzazi au mlezi anapaswa kulipa anapompeleka mwanafunzi shuleni kama gharama ya kujiandikisha au gharama ya usajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeziagiza Halmashauri zote nchini kuendelea na kuchukua hatua kwa Walimu Wakuu na Wakuu wa Shule wanaobainika kukiuka maelekezo haya na utaratibu wa uandikishaji. Kupitia Bunge lako natoa wito kwa wadau mbalimbali, wananchi na Waheshimiwa Wabunge kutoa taarifa inapotokea mwanafunzi au wanafunzi wanapoandikishwa kwa masharti ya kulipa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nitashirikiana na Mheshimiwa Mbunge kupata taarifa kamili za uwepo wa vitendo vya uandikishwaji wa darasa la kwanza wa wanafunzi katika Shule ya Msingi Upendo kwa masharti ya kulipa fedha ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa katika majibu ya msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba wadau, wazazi na Wabunge wasaidie kutoa taarifa na hatua zichukuliwe. Hapa Mheshimiwa Mbunge ameshatoa taarifa kwa sababu ametaja shule husika na eneo husika, sasa sijui Mheshimiwa Waziri anahitaji tena taarifa zipi? Kinachohitajika hapa ni je, Wizara kama Wizara imechukua hatua gani kwa shule husika kwa vitendo hivyo vya kuandikisha kwa kuwatoza wazazi fedha?

Swali la pili, kwa kuwa kumekuwepo na wimbi kubwa sana la michango shuleni, mara hela ya mlinzi, hela ya uji, sweta na nini, lakini mbaya zaidi sasa hivi kuna utaratibu kwamba kila mtoto anapokwenda shule anapaswa aende na *ream* ya karatasi *A4* na kila mhula. Je, Serikali inasemaje vitendo hivi? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwenye swali la msingi alikuwa anataka kujua hatua iliyochukuliwa na kama ambavyo nimeeleza kwamba hatua kwenye Shule ya Upendo imeshachukuliwa na tulipata taarifa ya aina ya michango ambayo inaelezwa kwamba pale kulikuwa na michango ambayo wazazi wenyewe waliridhia kwa ajili ya kutoa huduma ndogo ndogo pale shuleni.

Michango hii hata sisi Wizara tumeitolea maelekezo kwamba, michango yoyote inayochangishwa ni lazima kwanza Kamati ya Shule kwa Shule za Msingi au Bodi ya Shule kwa Shule za Sekondari, wanapofikia maamuzi hayo, lazima wazazi washirikishwe katika kutoa maamuzi hayo ya jambo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maamuzi hayo ya Kamati ya Shule au Bodi, wakishafanya maamuzi ni lazima waende kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kuona kiwango cha michango kilichoridhiwa kwamba hakiwezi kikawasumbua wananchi kutokana na mapato waliyonayo. Mbali ya hiyo pia, lazima Katibu Tawala aridhike kwamba michango ambayo sasa wananchi wenyewe wameridhia, michango hiyo lazima ipitishwe na ikubalike na Katibu Tawala wa Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo tunalisisitiza kwa sasa ni kwamba, maeneo yote mwanafunzi hawezi kusajiliwa kuingia darasa la kwanza au kidato cha kwanza kwa masharti ya kulipia jambo lolote lile fedha. Hili tumeshatolea utaratibu na bado tunasisitiza kwamba, mtoto yeyote ambaye anatakiwa kwenda shuleni lazima aende kwa masharti hayo kama ambavyo tumeeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la michango ya *ream* na nini sasa haya inategemea kama Kamati ya Shule imeweza kushindwa kabisa kupata uwezo wa kifedha, lakini sisi Serikali

tunatoa fedha inaitwa *capitation* kwenye shule ambayo kwenye *capitation* ile kuna asilimia 20 kwa ajili ya utawala ambapo Mwalimu anaweza kununua chochote kile.

Mheshimiwa Mweyekiti, lakini zipo pia asilimia 40 ambazo Mwalimu Mkuu anazitumia kwa ajili ya kuwataka Walimu kwa vifaa wanavyovikosa ikiwemo na *ream* kama anazihitaji kwa ajili ya kutolea huduma kwenye somo lake. Kwa hiyo, utaratibu umeshawekwa vizuri na haya kama yanajitokeza na kama ambavyo tumepata kwa Shule ya Msingi Upendo ambayo tayari tumeshapata maelezo ya nini na aina gani ya michango imetolewa. Tutaendelea kushirikiana na wadau wanapotupa taarifa ya maeneo ambayo walimu wana-*create* michezo ambayo inawakera wananchi kwenye maeneo yao.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Naomba niulize swali moja tu la nyongeza. Pamoja na michango kumejitokeza tabia mbaya ya Walimu Wakuu wa shule kuwachangisha wazazi michango ya wanafunzi ambao kwa bahati mbaya walifeli mitihani ya darasa la saba wakaingia kidato cha kwanza bila kujua kusoma na kuandika. Wanafunzi hao wanapotakiwa kurudishwa nyumbani Walimu Wakuu wanawachangisha wazazi pesa ili wanafunzi wasirudi nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri analisemaje hilo jambo ambalo si maadili kabisa ya walimu na limekithiri? Kwa mfano, katika Jimbo la Ikungi Magharibi shule nyingi za sekondari zinafanya shughuli hiyo. Naomba majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwanafunzi aliyefeli darasa la saba anakuwa hana uwezo wa kuingia kidato cha kwanza na kwa hiyo hata Mkuu wa Shule mamlaka yake ya kumtoza mwanafunzi huyu ili aweze kupata masomo, sijui masomo ya namna gani ambayo atayapata, lakini inawezekana pia mwanafunzi huyo aliyefeli darasa la saba angehitaji kupata mafunzo ya kidato cha kwanza yake mwenyewe na ameweka utaratibu wake mwenyewe na Mwalimu ambaye anapenda amfundishe kwenye masomo anayotaka, sasa hayo ni makubaliano binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali utaratibu ambao tumeuweka ni kwamba, mwanafunzi ambaye amefaulu darasa la saba atakuwa amekwenda kwenye eneo ambalo ameelekezwa kama ni kidato cha kwanza au tumempeleka kwenye shule ya ufundi au tumempeleka kwenye mafunzo mengine yoyote yale kwa utaratibu wa Serikali, huyu hatakiwi kuchangia jambo lolote lile.

Kwa hiyo, tunaweza kuwa na mambo mawili ya kijana ambaye anataka kujiendeleza yeye mwenye, ana uwezo wa kumtafuta Mwalimu kwa masharti ambayo watakubaliana wao wenyewe ili kuweza kupata elimu anayoitaka. Kwa hiyo huo ndiyo utaratibu ambao tunao kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kama kuna jambo hili ambalo linaendelea na linawekwa kama jambo rasmi, hilo tupewe taarifa ili tulichukulie hatua. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, unaweza kutuambia ni shule gani ya sekondari kule Ikungi Magharibi inafanya jambo hilo ili tuichukulie hatua mara moja.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana kwa hali ilivyo katika sekta ya elimu nchini, hali ni mbaya. Anapotuambia Waziri kwamba kuna maelewano baina ya mwanafunzi na mwalimu

binafsi, halafu tunaruhusu michango pale ambapo tumesema elimu ni bure. Kwa sababu kama elimu ya msingi ni bure, maana ya elimu ya bure ni nini? Sasa hivi tumesema elimu ya sekondari kuanzia mwaka ujao itakuwa bure, maana yake ni nini? Itakuwa bure kama nilivyosoma mimi au itakuwa ni bure ya sasa hivi ambapo michango ya shule ya msingi inafika mpaka zaidi ya laki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali ituambie nini maana ya elimu ya bure? Vinginevyo hali ilivyo sasa hivi tuna uchuuzi wa elimu, *mercantilistic education,* ndicho tunachofanya hapa ambapo haifai. Naomba tupate kwa usahihi maana ya elimu ya bure ni nini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni kwamba, tumeazimia kutoa elimu bora kwa vijana wote wa Kitanzania na elimu hii tunaizungumza kwamba kwa elimu ya msingi ni elimu bila ya ada ama *fee free education*, kwamba hatotozwa ada mzazi kwa ajili ya kumpeleka mtoto shuleni. Sekondari hatukuwa tukifanya hivyo na sasa Mheshimiwa Rais ametangaza kwamba tumeanza safari ya kufanya hivyo kwa shule za sekondari kwamba wanafunzi watasoma bila ya ada. Michango ya kuchangia elimu, hakuna kitu kizuri kama kuchangia elimu ya mtoto wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna jambo lingine la msingi la kimaendeleo kama kuchangia elimu; siyo kuchangia harusi wala kuchangia madogoli wala kuchangia kitu kingine, ni kuchangia elimu na utaratibu umewekwa maalum kwa Kamati za Shule, kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri au Bodi za Shule ndizo zitakazotathmini mahitaji ya ziada katika shule na kutathmini hali ya wazazi ya uwezo wa kulipa ndipo watakapoomba ruhusa ya kuchangisha. Michango itaendelea kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirejea swali la msingi kutoka kwa Mheshimiwa Christowaja ilikuwa kwamba suala la nyongeza la Mheshimiwa Christowaja kwamba kuna wanafunzi ambao wamekwenda sekondari wakichukuliwa kwamba walifaulu mitihani yao ya darasa la saba. Wamefika sekondari imegundulika hawajui kusoma na kuandika. Walimu wamekuwa wakifanya mipango ya kuwachangisha pesa ili wajue kusoma na kuandika, lakini kinachozungumzwa hapa sijakifahamu. Nilichotaka kujua, tunafanyaje na watoto ambao tulifikiri kwamba wanajua kusoma na kuandika na wamefaulu kwenda sekondari, kumbe wamefika sekondari hawajui kusoma na kuandika. Nini kauli ya Serikali katika mazingira kama haya? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, shule za sekondari si taasisi za kufundishia vijana fani za kusoma, kuandika na kuhesabu. Hatutegemei katika shule za sekondari Mwalimu yeyote apokee mwanafunzi asiyejua kusoma, kuandika wala kuhesabu. Hao wanafunzi ambao waliokuwepo mimi nimewasaka sana katika kila shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge ambao wanao wanafunzi hao waniletee mimi kama Waziri mwenye dhamana ya elimu kwa sababu moja, mwanafunzi hajui kusoma, hajui kuandika, hajui kuhesabu mtihani anaufanya namna gani, kwa sababu chini ya yote aweze angalau kuandika tu namba yake ya mtihani na kurudisha karatasi ili ile karatasi iende kusahihishwa. Hajui kusoma wala kuandika, wala kuhesabu ile namba ataiandikaje kwenye karatasi. Maneno ya fitina yasiwepo, lazima tujue kwamba Serikali imefanya kazi nzuri na wanafunzi wanasoma na shule hizi zinaendelea vizuri.

Na. 96

**Halmashauri Kukopesha Vijana na Wanawake**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA** aliuliza:-

Halmashauri nyingi nchini hazitekelezi mpango wa kukopesha vijana na wanawake ambayo ni asilima tano inayotokana na mapato kwa vijana na asilimia tano kwa wanawake:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kwa Wakurugenzi walioshindwa kutekeleza hilo?

(b) Je, Serikali inadaiwa kiasi gani na Mifuko hiyo iliyopo kila Halmashauri?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli baadhi ya Halmashauri hazitengi asilimia tano kwa ajili ya vijana na asilimia tano kwa ajili ya Mfuko wa Wanawake. Kwa kuzingatia hali hiyo, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI imechukua hatua kupitia kikao cha Wakurugenzi wote kilichofanyika tarehe 3 Julai, 2014 katika Mkoa wa Tanga na tarehe 7 Novemba, 2014 katika Mkoa wa Morogoro kwa kuzielekeza Halmashauri zote kuhakikisha fedha hizo zinatengwa, ikiwa ni pamoja na kupeleka fedha ambazo hazikutengwa katika miaka iliyopita.

Pamoja na hatua hizo ufuatiliaji umekuwa ukifanyika katika Halmashauri zote kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatengwa. Aidha, kutotengwa kwa fedha hizo katika Mifuko limekuwa likiibua pia hoja ya ukaguzi katika taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*; kitendo ambacho hulazimu Halmashauri kupeleka katika Mifuko kiasi cha fedha kilichobaki ili hoja hizo ziweze kufungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(LAAC)* pamoja na Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, zimekuwa zikiweka msukumo kwa kila Halmashauri kutekeleza agizo hili. Kuhusu Wakurugenzi ambao hawatengi na kupeleka fedha hizo ni kwamba watakuwa wamekwenda kinyume na maagizo ya Serikali, kwa hiyo, watachukuliwa hatua kali za kinidhamu.

(b) Mheshimiwa Mweyekiti, katika kipindi cha miaka miwili 2013/2014 na mwaka 2014/2015, hadi Desemba, 2014 Halmashauri zilichangia jumla ya shilingi bilioni tatu na *point* nane katika Mfuko wa Wanawake na Vijana. Fedha zilizopaswa kupelekwa katika kipindi hiki ni shilingi bilioni 50.7 ambayo ni asilimia kumi ya fedha zilizokusanywa.

Kwa takwimu hizo kiasi ambacho hakikupelekwa ni shilingi bilioni 46.9. Hivyo kutotengwa kwa fedha hizo, ndilo tatizo la msingi linalofanya vijana na wanawake wasinufaike na Mfuko huu. Aidha, kutorejeshwa kwa mikopo hii ni sababu nyingine inayofanya Mfuko huu kutokuwa endelevu. Mfano kwa mujibu wa taarifa ya *CAG* ya mwaka 2012/2013,

kiasi cha shilingi bilioni moja na *point* nne kilikuwa hakikurejeshwa kutoka katika vikundi vilivyokuwa vimekopeshwa fedha katika Halmashauri 58 nchini. Serikali itaendelea kuhimiza Halmashauri kutekeleza agizo hili ili fedha hizo ziweze kuwanufaisha vijana na wanawake kwa kuwapatia mikopo.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Agizo hili lilitolewa toka mwaka 1993 na lengo lake lilikuwa kuwanasua vijana na akinamama kutoka katika lindi kubwa la umasikini kwa kupata mikopo hii yenye riba nafuu. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuweka utaratibu mzuri wa upatikanaji wa mikopo hii kuliko ilivyo sasa, kwani vijana wengi hawana ajira na akinamama wengi wanahangaika? Mikopo hii ni nafuu inaweza kuwasaidia kujiajiri ili kuondoa tatizo hili kubwa la kutokuwa na ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, kwa mujibu wa taarifa ya *CAG* ya 2012/2013, inaonekana kwamba mapato yaliyopatikana katika Halmashauri zote yalikuwa takriban bilioni 270, hivyo asilimia kumi ni kama bilioni 27, lakini Mfuko huo ulikuwa pungufu, yaani Halmashauri zote ukiangalia ripoti inaonekana ilichangia *only* bilioni saba. Pamoja na nia hiyo njema ya Serikali lakini asilimia 98 ya Halmashauri zote hawajatoa fedha katika Mfuko huu.

Je, Serikali haioni kwamba agizo hilo lilitolewa kisiasa ndiyo maana utekelezaji unakuwa mgumu, hivyo wameshindwa kutekeleza agizo lao wenyewe na ndiyo maana ukienda Halmashauri nyingi unakuta pesa hizo zinatolewa *may be* kwa itikadi za kisiasa zilizopo na maeneo mengine unakuta pesa hizo zinatolewa kwa ndugu wa wale Madiwani au wale wanaofahamiana na watendaji. Serikali inasemaje juu ya suala hili?

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokielewa hapa ni kwamba, haya ni maagizo na maelekezo ya Serikali ambayo yanajaribu kuangalia jinsi ambavyo unaweza ukawasaidia akinamama na jinsi ambavyo unaweza ukawasaidia vijana. Utaratibu huu tuliouweka ndiyo huu, ndiyo ambao tumesema na hela zinazozungumzwa hapa tunazungumza hela za mapato ya ndani, ni *own source* ndiyo inazungumziwa hapa, si mapato yote yanayoingia katika Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapa tumekiri kabisa kwamba kama ulitegemea kuchukua shilingi bilioni 50 na hela zilizokwenda ni bilioni tatu, maana yake inaonesha kwamba kuna tatizo hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema jambo moja hapa Waheshimiwa Wabunge wenzangu ili tuweze kuelewana vizuri, kwa sababu jambo hili limepigiwa kelele, *Local Authorities Accounts Committee* wamelisemea na Kamati ile ya Mheshimiwa Kigwangala wamelizungumzia sana na tumesema hapa. Tungetoka hapa na azimio na agizo hapa tukasema hivi, tunakwenda katika Halmashauri zetu, hakuna kupitisha bajeti hapa mpaka utuoneshe hela zilizotengwa kwa ajili ya vijana na akinamama. Mtakuwa mmetusaidia sana katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewaita hawa Morogoro wamekuja pale, tumewaita Tanga wamekuja pale. Kama mnakumbuka mwaka 2012 hapa ndani, tulitoa ripoti kuhusu Kongwa kwamba Mkurugenzi Mtendaji pamoja na Mhasibu na wenzake pamoja na Kondoa walipewa tozo kupitia Kamati hizi ambazo nimezitaja hapa. Kwa hiyo, nataka kusema hivi, hili jambo si jambo la kusema tutafanya sisi wenyewe, sisi tutasukuma kwa maana hii inayozungumzwa hapa, lakini tunaomba Waheshimiwa Wabunge hapa msipitishe bajeti katika Halmashauri bila kuhakikisha kwamba hizi hela zimetengwa, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumeulizwa hapa kwamba tunafanya nini? Tumeshawaambia Wakurugenzi; Mkurugenzi ambaye hatatenga hizi hela maana yake kazi imemshinda, ndicho tunachosema hapa, mwende kule mkatusaidie, la kwanza hilo maana tumeulizwa hapa, ndilo swali lililoulizwa na Mheshimiwa Mhonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, fedha zilizokuwa zipite mwaka wa juzi na mwaka wa jana lazima akuletee mpango unaoonesha jinsi atakavyofidia hizo hela ambazo zilitakiwa ziende kule, kwa sababu hawezi kuchukua hela zote, kama anapata bilioni moja na *point* nane hawezi kuchukua zote akazipeleka moja kwa moja kwenye hii Mifuko, atakwenda awamu kwa awamu. Hili nalisema ili Wabunge mtusaidie kulifuatilia, tumewaagiza, tumewaambia aoneshe mpango utakaoonesha jinsi atakavyokuwa anafidia kidogo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni la kwetu sisi wote, sasa tunaambiwa tunaleta *politics*, nani analeta siasa hapa. Sisi tunawapa vikundi vya akinamama na humu ndani wanasema tunaongea siasa, humu ndani kazi yetu ni kuzungumza siasa, yaani mtu ambaye hazungumzi siasa humu ndani, hajui kilichomleta huku. Huu ndiyo mtambo wa kuzungumza siasa, siasa hii tunayozungumza hapa ni siasa ya kuwawezesha akinamama na vijana, si siasa mbaya. Tukitenga hizi hela asilimia tano wakizipata zitakwenda kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameuliza swali la pili, asilimia 95 hawajatoa fedha hizo. Nimekiri hapa ni kweli, tusaidieni Wabunge, msipitishe bajeti bila kuona kwamba hela hizi zimetengwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso!

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti naona umenichanganya, mimi Pauline, lakini si tatizo sana…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pauline Gekul!

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Wizara ya Habari, Vijana na Utamaduni, wametoa mwongozo katika Halmashauri zetu kwamba vijana wajiunge kwenye *SACCOS* ili wakopeshwe, lakini sasa kuna tatizo. Vijana hao wamenyimwa asilimia tano za fedha za Halmashauri ambazo zinatengwa kwa ajili yao kwa kuwa wamejiunga kwenye *SACCOS*, mfano mzuri ni Halmashauri ya Mji wa Babati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufahamu, TAMISEMI na Wizara hii hawana mawasiliano hadi vijana hao kunyimwa hizo asilimia tano, kwa kuwa wameshajiunga zaidi ya vijana 300 katika hizo *SACCOS*?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Pauline Gekul, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Manyara, kama ifuatavyo:-

Labda tuinanii hapa, Mifuko hii ni Mifuko miwili tofauti tunavyoizungumzia hapa. Hii *five percent* tunayozungumza hapa ni *five percent* ambayo inatokana na *own source*, hiyo ni upande mmoja. Hii inakuwa *managed under* Ujamaa *and Cooperatives* katika Halmashauri zetu, *that is number one* na wewe ni msomi, kwa hiyo najua kwamba utakuwa unanielewa kitu ninachozungumza hapa, ile Idara ya Ushirika ndiyo inayosimamia na mambo ya *SACCOS* na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nyingine anayosema ya Maendeleo ya Jamii, ni kweli inatoka Wizarani kama anavyosema na zikitoka pale zinakwenda kwenye Idara hiyo hiyo ya Maendeleo ya Jamii ndiko zinakopitia kule. Utaratibu wao ili uweze kuzi-*capture* hizi hela lazima uwapitishe katika utaratibu wa ki-SACCOS, *otherwise* hizi hela zitakuwa zimeondoka moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawezi kwenda mtu pale anasema hivi, mimi nataka mkopo hapa, unamuuliza nyumbani kwako ni wapi, anasema ni pale kwenye kichuguu, ukikata kona hapo kwenye mfereji, kule juu karibu na Msikiti, chini yake hapa kuna mfereji ,hapo ndipo nyumbani kwangu. Tunamtaka mtu anayekuja hapa atuambie kwamba ana anwani. Nani Mwenyekiti wa hicho kikundi, nani Katibu wake, nani Mweka Hazina wake, ukimuuliza Mkurugenzi anasema naam, nawafahamu hawa watu, ili hela hizi ziweze kurudi tena, ndiyo msingi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuhusu kwamba kuna watu ambao wamejiunga hivyo anavyosema Mheshimiwa Gekul, ni jambo ambalo nitahitaji kufuatilia, nijue vizuri kwamba ni nini kilichojiri ili niweze kuipata hii. Hata hivyo, nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge nitashirikiana naye katika jambo hili kuona kwamba ni kwa nini sasa mtu anajiunga na hivyo vikundi halafu ndiyo inakuwa sasa kigezo cha kumnyima hizo hela, *it's a contradiction*.

**NAIBU WAZIRI HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI naomba kuongezea majibu machache.

Mfuko wa Vijana ambao unasimamiwa na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo hauna mahusiano na ile fedha inayotolewa ndani ya Halmashauri kwa mujibu wa bajeti zao. Tunachofanya kwenye Wizara yetu ni kuwahamasisha vijana kujiunga pamoja katika vikundi, katika Halmashauri; wakishajiunga pamoja Maafisa wa Wizara wanakwenda kutoa mafunzo kwa vijana hawa ili waweze kutumia fedha zile vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini zinapitia kwenye Halmashauri, ili tuwajue vijana hawa wako wapi na wanafanya nini. Fedha ile haitolewi tu hivi hivi kwamba umekuta vijana njiani unatoa, hapana, lazima wapitie hatua zote hizo ili unapokopesha ile fedha unajua kabisa utakwenda kumshika nani.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi. Narudi kwenye jibu la msingi la Mheshimiwa Naibu Waziri. Alisema kwamba fedha nyingi kati ya zile ambazo zilikuwa zimekopeshwa hazirudi. Nataka kuiuliza Serikali, kwa sababu Manispaa nyingi hazina wataalam ambao wanaweza kuwa na ujuzi wa kutoa mikopo na kufuatilia hiyo mikopo. Ni kwa nini sasa Serikali isitafute benki ambayo fedha hizo zingeweza zikaenda huko, halafu vijana na wanawake wakakopeshwa kwa kutumia hiyo benki ili ziweze kuwa zinakopeshwa, lakini zaidi sana zinarudi ili watu wengine waweze kupata kwa wakati fedha hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo anayoisema anasema kitu cha kisasa, anasema kitu *modern* kizuri. Yaani kupitisha fedha, mikopo nini, ukipitishia kwenye mfumo wa benki *is a modern way of living*. Hakuna mtu anaweza akampinga Mbunge hapa akamwambia kwamba hicho kitu unachokisema ni kitu cha ajabu ajabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema hapa liko tatizo. Tunatakiwa tutatue tatizo la msingi kwanza, alisema Mao; *resolve the primary contradiction, the secondary one* itaondoka tu. Kama watu hawachangi hizi hela, hawapeleki kule hata benki utapeleka nini. Tunachozungumza hapa Mheshimiwa Mwaiposa ni kwamba tusaidieni kuweka msukumo kuhakikisha kwamba Halmashauri zetu katika *own source* wanatenga hizi hela, hicho ndicho tunachokisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili analolisema kwamba tutumie utaratibu wa kibenki, kwa maana ya kwamba benki zitasaidia, lazima zitakuwa zinatoka kwenye Halmashauri zitakwenda kule na hela zetu zote huwa zinatunzwa katika benki, ni utaratibu mzuri na sisi tutazingatia maoni yake.

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nasikitika sana kwa sababu naona Serikali inahangaika kunyoosha kivuli wakati mti umepinda. Tatizo la pesa asilimia tano kwenye Mfuko wa Wanawake na Vijana ni tatizo ambalo limetengenezwa tangu awali kwa kupitisha utaratibu kisiasa. Kwa sababu utaratibu ule hauruhusu mtu mfano akipewa pesa leo, halafu harejeshi, hauruhusu mtu yule kuwajibishwa au kufuatwa ili pesa azirudishe kwa sababu pesa hizo wanapeana watu kutumia itikadi na si kwa malengo ya kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka niulize, je, ni lini Serikali itakuwa tayari kubadilisha ile kanuni, huo utaratibu wa kwenye Halmashauri na si kuwalazimisha Wakurugenzi kupeleka pesa ambazo zinakwenda kuliwa bila faida? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwelewa anachosema. Anasema kwamba huu utaratibu, hiki kitu kimefeli na nini. Tunaweza tukapinga kila kitu hapa, lakini hatuwezi kupinga jitihada hizi ambazo tunazionesha hapa kuona kwamba sasa tunawasaidiaje hawa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kusema hapa ni kwamba, kama tunafikiri kwamba huu utaratibu tunaouzungumza hapa, umekuwa *totally disfunctional* tunazo Kamati zetu tunaweza tukapitisha kule tukasema hivi, kuna haja ya kuishauri Serikali ili ibadilishe mfumo mzima huu ili tuwe na mfumo mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni tatizo kabisa katika jambo hilo, kama kuna njia nzuri ambayo tunafikiri kwamba inaweza ikasaidia, tukimweleza Mheshimiwa Waziri Mkuu tukamwambia kwamba tazama, hili jambo tumejaribu tunaona kwamba tunapata matatizo. Wabunge wanashauri *one, two, three and four*, kwa hiyo tutumie utaratibu huo, hakuna tatizo kabisa Mheshimiwa Kuruthum, sisi kama una utaratibu ambao unafikiri unaweza ukasaidia zaidi kuliko huu, tupo tayari kupokea kama tulivyosema kwa Mheshimiwa Mwaiposa.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Bahati nzuri nipo Kamati ya *LAAC* tumezunguka Halmashauri nyingi na mara zote Serikali imeendelea kulazimisha Wakurugenzi wapeleke hizi fedha 5% kwa vijana na wanawake. Vijana na wanawake kimsingi katika Taifa hili ndiyo watu wa maana sana kushughulikiwa, wapate huduma inayopasa.

Sasa kwa kuwa, limekuwa dondandugu hili na haliwezekani kutekelezwa, moja, ukiangalia hizi *own source* kwa Halmashauri zote hawatimizi wala hawana fedha kama ambavyo Serikali Kuu haina fedha. Sasa naona tunalazimisha kitu ambacho hata hakiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuiuliza Serikali, ni vizuri sasa hiki ambacho kinasemwa 5% kwa wanawake na vijana lifutwe maana limeshindikana na haliwezekani, uje mfumo wa kuhakikisha kwamba vijana na akinamama wanapata haki. Kwa hiyo, Serikali ikiri imeshindwa, itoe kauli na wafanye nini sasa ili kusaidia vijana na akinamama, ndiyo kauli ya Serikali ambayo nataka kuhusu jambo hili la 5%.

**WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui niseme nini kwa sababu hapa sijasikia swali, lakini nimesikia amesema Mfuko huu ufutwe, ndivyo nilivyosikia. Labda nijibu kwenye hilo kwa sababu sikusikia swali na kama kuna swali naomba uniambie ili nimjibu, lakini nimeelewa sentensi zake, nimeelewa alichozungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia swali la nyongeza lililoulizwa, mimi Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, nasimama hapa nasema hivi kuanzia leo nawatangazia kwamba Mfuko huu umefutwa, kweli inawezekana habari ya namna hiyo? Mimi nasema hivi, Mheshimiwa Natse usinitie majaribuni bali uniokoe na yule mwovu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nieleze vizuri kwamba nitatamka hapa kwa jambo kubwa, zito namna hii ambalo linagusa nyoyo za watu na Serikali inalifahamu, sitaweza!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nasema na narudia tena kwamba kauli yetu sisi katika jambo hili ni kwamba, hatuwezi kubishana na Wabunge hapa kwa sababu Wabunge wanatoka kwenye *field,* wanajua hali halisi iliyopo Rombo, Kyela, Kigoma na kwingineko, wanajua hali halisi iliyopo kule. Kama *seriously speaking* tumefika mahali tunasema Mfuko huu haujasaidia, nataka niseme leo hapa kwamba hizi jitihada ndizo zilizozaa kiasi hiki cha pesa mnachokitaja hapa, kule nyuma zilikuwa hazitengwi kabisa

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunafahamu tukienda katika maeneo ya vijijini, sasa hivi vijana ndiyo wanapiga kelele sana na akinamama nao ndiyo wanapiga kelele sana. Kwa hiyo, tunaona kwamba *at least* ipo Serikali ambayo inajali kwamba wananchi wake wako katika hali hii. Sisi sote tunafahamu, tusifike kule tunataka haki zetu, tunaonewa, tunataka haki zetu, tunaonewa, sasa hii inajibu, lakini kama inaweza ikaboreshwa, tukapata hali nzuri zaidi ambayo itasaidia katika jambo hili. Sisi kama Serikali tunasema tuleteeni tupo tayari kufanya jambo hilo.

Na. 97

**Kata ya Msinjahili Lindi Kupatiwa Kivuko**

**MHE. SALUM K. BARWANY** aliuliza:-

Kata ya Msinjahili katika Manispaa ya Lindi inatenganishwa na Bahari ambapo wananchi hulazimika kuzunguka umbali mrefu au kuvuka kwa mitumbwi/boti:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka kivuko katika Kata hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mbunge wa Lindi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilituma wataalam wake mwishoni mwa mwaka 2013 kwenda Mkoani Lindi kufanya tathmini ya eneo hilo ili kuona kama linafaa kuweka kivuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya wataalam inaonesha kuwa sehemu inayotumika kuvusha watu kwa mitumbwi kati ya Lindi Mjini na Kitunda katika Kata ya Msinjahili ina idadi ndogo ya abiria na kiasi cha mizigo inayovushwa ni kidogo. Aidha, mazingira yaliyopo sasa hivi pande zote mbili za mkondo wa bahari hayaruhusu kuweka kivuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali halisi ya mazingira ya eneo husika na shughuli za kiuchumi katika eneo hilo, chombo kinachofaa kwa sasa kwa ajili ya kuhudumia eneo hilo ni boti inayoendeshwa kwa injini. Hivyo nashauri Halmashauri ya Wilaya ya Lindi, itenge fedha za kununua boti itakayoweza kutoa huduma katika eneo husika.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, kwa muda mrefu katika kivuko cha Bahari ya Hindi kati ya Lindi Mjini na Kitunda ni ahadi ya Rais na aliahidi kwamba ndani ya kipindi chake hiki cha miaka mitano atahakikisha kwamba ataleta kivuko kwa ajili ya kuwahudumia watu zaidi ya 10,000 ambao wanaishi ndani ya eneo hilo. Je, kwa mujibu wa taarifa za wataalam zimekiuka ahadi ya Rais ambayo ameitoa katika ziara zake katika Mkoa wa Lindi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, wakati Mheshimiwa Rais amekwenda Lindi, wazee wa Kata ya Msinjahili walimuona kwa kuomba wapate huduma ya kivuko. Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, ni kwamba kivuko hakiwezi kuwekwa mahali ambapo hakitaweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu pili, hivi vivuko kwa vyovyote vile ni lazima kuwe na abiria wa kutosha na watu wa kutosha ili kusudi kiweze kujiendesha na ndiyo maana ushauri sasa ni kwamba badala ya kivuko tuweke boti. Kwa hiyo, baada ya kuweka boti, Halmashauri ya Wilaya ya Lindi itakuwa imetekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Tathmini iliyofanywa ya kivuko hiki ilikuwa ni ya miaka mingi, sasa hivi watu wamezaliana wapo zaidi ya 10,000 na watu wa Kitunda hutegemea kuja Lindi Mjini kila siku hospitalini, shuleni, kununua vyakula, wanakwenda *stand* kusafiri na pia wanakuja kupiga kura. Sasa hivi watu wameongezeka, boti peke yake haitoshi, tunataka kivuko, tunaomba Serikali leo iseme hapa ni lini kivuko hiki kitaanza kushughulikiwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sipingi kwamba wananchi wangependa wawe na boti, lakini mazingira yale tunatoa kitaalam na ukiweka boti ambayo watu wanaotumia boti lile hawawezi kuendesha hata *operation costs* nani atakayekuwa analipa? Kwa sababu Serikali inawekeza kununua boti, lakini uendeshaji inategemea mizigo na watu waliopo pale. Sasa nafikiri kama katika miaka miwili watu wamezaliana mara tatu zaidi ya vile tulivyoona basi tutakwenda kuangalia tena, tuone hiyo idadi ya watu na tuone kama vigezo hivi vinaweza kuwa ni tofauti na wakati ule.

Na. 98

**Kuchimba Mabwawa ya Kuteka Maji ya Mvua**

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU (K.n.y. MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI)** aliuliza:**-**

Je, Serikali ina mpango gani wa kuchimba mabwawa ya kuteka maji ya mvua ili kuwawezesha wakulima wa mpunga wa Skimu ya *Lower Moshi* kufufua kilimo cha mpunga kinachokabiliwa na ukame?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Cyril August Chami, Mbunge wa Moshi Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Skimu ya *Lower Moshi* iliyojengwa kati ya mwaka 1984 na mwaka 1987 kwa ushirikiano wa Serikali ya Tanzania na Serikali ya Japan, ina eneo linalofaa kwa kilimo cha mpunga hekta 1,100 na mazao mchanganyiko hekta 1,200. Hata hivyo, kutokana na upungufu wa maji eneo linalomwagiliwa kwa sasa ni hekta 600 kwa mpunga na hekta 500 za mahindi. Aidha, uhaba wa maji kwenye eneo linalolimwa umesababishwa na mabadiliko ya mahitaji ya maji ambayo yametokana na upanuzi wa maeneo ya kilimo cha mpunga kwa kutumia vyanzo vilevile vya maji, uharibifu wa vyanzo vya maji na ukame unaosababishwa na mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia changamoto ya upatikanaji wa maji kwa ajili ya umwagiliaji katika Skimu ya *Lower Moshi,* visima viwili virefu vimechimbwa na vimeonesha kuwepo kwa maji na mipango iliyopo ni kuweka miundombinu ya kutumia maji hayo kwa ajili umwagiliaji. Aidha, Wizara imeandaa andiko la mradi *(project proposal)* kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu *(feasibility study),* ujenzi wa mabwawa katika Skimu, uchimbaji wa visima virefu vinne pamoja na uwekaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu hiyo kwa gharama ya sh. 5,309,755,000/= na mradi huo unatarajiwa kujenga katika kipindi cha miezi 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia gharama kubwa ya utekelezaji wa mradi huo, Wizara itaendelea na mikakati ya kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ili kuboresha miundombinu ya umwagiliaji katika Skimu ya *Lower* Moshi kwa manufaa ya wakulima ambapo maombi ya kiasi cha shilingi milioni 400 yamewasilishwa katika Mfuko wa *Food Aid Counterpart Fund (FACF*) kwa ajili ya kupata fedha za utekelezaji wa mradi huo. Aidha, katika kuhakikisha mradi wa *Lower Moshi* unatekelezwa kwa wakati katika bajeti ya mwaka 2015/2016, Wizara imewasilisha maombi maalum Hazina kwa ajili ya kupata fedha za utekelezaji wa mradi huo kwa manufaa ya wakulima wa Moshi.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa majibu. Kwa ninavyomfahamu Mheshimiwa Naibu Waziri hata yeye mwenyewe haridhiki nayo. Sasa nataka niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, mradi huu umesemwa utatekelezwa kwa kipindi cha miezi 24 bila kutamka mradi huo utaanza kutekelezwa kuanzia lini na utafutaji huu wa fedha, ni kwa nini Serikali sasa isiangalie vyanzo vingine aidha kuingia mikataba na makampuni au taasisi binafsi ili kuweza kuwekeza katika mradi huo? Hilo la kwanza.

Pili, pamoja na utekelezaji wa miradi hii Serikali imeshindwa vipi kukubaliana na makampuni ya ujenzi ambayo yamekuwa katika nchi nzima yanachimba michanga na udongo kwa ajili ya kwenda kujenga barabara? Kwa nini maeneo yale yasirekebishwe na kuwa mabwawa ya uhifadhi wa maji ambayo yangesaidia katika *scheme* mbalimbali za umwagiliaji

ili kuwasaidia wananchi kutumia maji yale, tatizo la nchi yetu tuna tatizo la *water management*, hatuna ukame lakini hatuwezi kuhifadhi na kuyatumia maji ya mvua tunayoyapata.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba Mheshimiwa Mbunge afahamu kwamba mradi huo wa *Lower Moshi* siyo mradi mpya bali ni mradi wa siku nyingi kama nilivyosema ulijengwa mwaka 1984 kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Japan.

Changamoto kubwa tuliyoipata katika eneo lile ni mabadiliko ya tabia nchi ambayo yamesababishwa na maji yaliyokuwa yanatiririka kutoka milimani pia yapungue lakini pia kuongezeka kwa shughuli za kilimo katika maeneo yale imesababisha maji kuwa kidogo, shughuli zinaongezeka, lakini vyanzo vya maji vinabaki kuwa vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuliona hilo na umuhimu wa mradi wa *Lower Moshi* ndiyo sababu tumeanza sasa kuhangaika na uchimbaji wa mabwawa mengine ili tuweze kuongeza nguvu ya maji ambayo yanaweza yakatumika katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri nimeshatembelea mradi huo, hizo changamoto nimeziona na Wizara inafanya kazi kubwa ya ziada ya kuhakikisha kwamba hiyo kazi inafanyika. Sasa anasema tumetaja miezi 24 bila kutaja lini. Kazi hii itafanywa miezi 24 kutegemeana na pesa itakapopatikana, kwa sasa bado pesa hiyo haijapatikana, lakini itakapopatikana mradi huu utajengwa kwa kipindi cha miezi hiyo 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, anasema kwamba maji yale ambayo yanabaki katika maeneo ambayo mchanga unachotwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara sehemu zile zigeuzwe kuwa kama mabwawa ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunapata mipango kutoka Halmashauri za Wilaya au maeneo yanayohusika. Sasa kama kuna eneo ambalo lilitumika kuchota mchanga kwa ajili ya ujenzi wa barabara na likaonekana lina maji na Halmashauri zika-*recommend* kwamba maji hayo yanafaa kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kijamii sisi kama Wizara hatutakuwa na matatizo yoyote.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji jana wakati anajibu swali la Mheshimiwa Chiligati aliahidi kwamba wanategemea kutenga fedha kwa ajili ya kwenda kuchimba mabwawa ya skimu za umwagiliaji za Mbwasa na maeneo mengine na kwa kuwa skimu ya umwagiliaji ya Mkwese mashine yake au pampu imekufa, je, Serikali itakuwa tayari kwenda kutengeneza au kupeleka pampu mpya ili kufufua mashine ya skimu hiyo ya umwagiliaji ambayo sasa hivi haifanyi kazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu na naomba yawe mafupi!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Chilolo kwa swali lake, lakini suala la kwamba pampu ya maji haifanyi kazi, halafu likawa suala la Wizara ya Kilimo, nadhani Halmashauri inayohusika itakuwa haijawajibika sawasawa.

Kwa hiyo, naiomba Halmashauri inayohusika itenge pesa kwa ajili ya kutengeneza au kununua pampu mpya ili usukumaji wa maji kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji katika Skimu ya Mkwese ambayo Mheshimiwa Mbunge ameisema basi iweze kufanyika. Kama tatizo ni kubwa

zaidi, basi wahusishe ofisi yetu ya Kanda iende kufanya tathmini na kama wakiona tatizo ni kubwa zaidi, basi walete mahitaji hayo Wizarani.

Na. 99

**Kusuasua kwa Mradi wa Maji Heru Juu**

**MHE. MOSES J. MACHALI** aliuliza:-

Je, ni sababu gani zinazosababisha mradi wa maji wa Heru Juu kusuasua hadi sasa kwa kushindwa kuanza kwa utekelezaji wa ujenzi wa mradi huo ili wananchi hao wapate maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Mradi wa Maji wa Heru Juu umechelewa kuanza kutokana na kuchelewa kukamilika kwa usanifu wa kina wa mradi. Kwa sasa usanifu umekamilika mwezi Agosti, 2014 na mradi huu unatarajiwa kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya ukarabati wa mradi kwenye Kijiiji cha Heru Juu na upanuzi wa mradi kwenye Vijiji vya Kavunga na Muhunga. Hadi kufikia mwezi Juni, 2014, jumla ya shilingi milioni 372.9 zimetumwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kwa ajili ya ukarabati wa mradi. Fedha nyingine zitatumwa kulingana na upatikanaji wake ili kukamilisha ukarabati wa mradi huo. Mradi huu utakapokamilika utawanufaisha wananchi wapatao 28,032 kwa vijiji vya Heru Juu, Kahunga na Muhunga.

Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ipo katika hatua ya kumpata mzabuni wa ununuzi wa vifaa kwa ajili ya ukarabati wa Mradi wa Heru Juu. Kazi ya ukarabati itaanza mara baada ya manunuzi ya vifaa kukamilika.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa nimuulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza, Mheshimiwa Waziri nimshukuru kwani amekuwa ananipa ushirikiano katika kufuatilia mradi huu, lakini nina maswali mawili yafuatayo:-

Kwanza kidogo nasikitika kwa kuona majibu haya, ambapo inawezekana pengine wamekupa taarifa ambazo si sahihi. Ukiangalia tangu mwaka jana mwezi Novemba wakati tumefanya ufuatilia mimi na wewe, ndiyo maana nimesema nakushukuru, walisema wametangaza zabuni mwezi Novemba, lakini kama unavyoona ni kwamba mlolongo wa zabuni hii umekuwa ni wa muda mrefu kiasi kwamba mpaka leo wamechelewa kumpata Mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nimweleze Mheshimiwa Waziri tu kwamba kimsingi mchakato mzima wa kuweza kumpata mkandarasi mjenzi unachelewa kwa sababu baadhi ya Madiwani wamekuwa wakijihusisha na zabuni na wengine tunasikia kwamba wameomba kazi hii, kuna kama kupigana huku kwenye Halmashauri sasa naomba kauli ya Serikali. Swali la kwanza, je, Mheshimiwa Waziri unaonaje pengine ungefuatilia kwa ukaribu na uniambie kwa maslahi mapana ya wananchi hawa wa Heru Juu, Kahunga pamoja na Muhunga kazi hii ya kumpata mkandarasi mjenzi itakamilika lini? Ningeomba kupata *time frame*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naomba tu anisaidie *time frame* ya kwamba mkandarasi atapatikana lini na kazi itaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikiri kwamba amekuwa mara kwa mara akifuatilia mradi huu, mimi na yeye tumepiga simu tukaweka *loud speaker,* tukamsikiliza Mhandisi na Mkurugenzi, niseme tu kwamba mlolongo huu sasa nimuahidi tu kwamba, mimi kama Naibu Waziri na Waziri pale nimeshamweleza na ili mradi hawa watu Mhandisi na Afisa wa Manunuzi wako Dar es Salaam, basi nawaagiza Jumatatu badala ya kwenda Kasulu wapite hapa Dodoma ili tuweze kulijadili jambo hili lakini pia kwa taarifa zilizopo ni kwamba wameshaandaa huo mkataba ili utoke na kwenda Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na baada ya hapo siku 45 ndiyo uanze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa umuhimu na maslahi mapana ya Wanakasulu Mheshimiwa Mbunge anaowasemea, basi namuagiza Mhandisi na Afisa Manunuzi wapite hapa Dodoma Jumatatu kwa ajili ya kumaliza jambo hili na kulisukuma liende kwa haraka zaidi.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa miradi mingi ya maji imeendelea kusuasua na wananchi wanaendelea kupata shida ya maji katika miji mbalimbali ukiwamo Mji wa Bahi, lakini kwa bahati nzuri tumepata mfadhili wa *UNDP* ambaye ametufadhili pale Bahi shilingi milioni 230 kwa ajili ya ukamilishaji wa maji wa kutoka Mkakatika kwenda Bahi lakini unahitaji milioni 400 zaidi.

hata hivyo Serikali imetutengea fedha shilingi milioni 400 kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa kutoa maji Mbwasa Manyoni na kuleta Bahi lakini upembuzi yakinifu huo hauwezi kutupa maji kwa sasa, nilimwandikia Mheshimiwa Naibu Waziri kumuomba wabadilishe matumizi ya zile fedha shilingi milioni 400 kutoka upembuzi yakinifu ili zije zikamilishe huu mradi wa kutoka Mkakatika kwenda Bahi. Sasa nataka kujua Waziri amefikia wapi juu ya jambo hili kwa ajili ya kuwapa wananchi wa Bahi ili waweze kupata maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Badwel ameniandikia barua, tumefanya mazungumzo na wazo lake tumelipokea lakini nilimwambia kuwa barua ile aliyonipa, nimewapa wataalam ili wafanye tathmini halafu watushauri ipasavyo kuweza kubadilisha hayo matumizi.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Utakuwa umeona kwamba Wabunge wengi ama wamesimama au wamekuwa wakipiga meza kutaka kupewa nafasi kuuliza maswali ya nyongeza kuhusu matatizo ya maji katika maeneo yao. Kwa hiyo, hii inadhihirisha kuwa hii ni kero *number one* katika Majimbo mbalimbali nchini.

Sasa katika Mkutano wa Bunge la Bajeti ambapo Wabunge walizungumza kwa nguvu kweli juu ya jambo hili niliiomba Serikali itoe majibu juu ya sababu ya ahadi ya Rais aliyoitoa Bungeni mwaka 2005 akizindua Bunge kuwa maji ni kero *number one* na Serikali itatekeleza mpango kabambe ili ifikapo mwaka 2010 tatizo la maji liwe limemalizika na sasa ni 2015 halijamalizika. Mheshimiwa aliyekuwa anakaimu nafasi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Mwandosya alisimama akaahidi kwamba ili hatua ziweze kuchukuliwa katika kila Mkutano wa Bunge Serikali itakuwa inawasilisha taarifa maalum juu ya utekelezaji wa miradi ya maji katika maeneo mbalimbali ambayo itawagusa Wabunge kwa ujumla wake maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ni lini sasa Wizara ya Maji na Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu katika Mkutano huu wa Bunge watawasilisha taarifa hiyo ili tunufaike Wabunge wa Majimbo yote kama alivyoahidi Kaimu Waziri Mkuu?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa fursa ya kujibu swali la Mheshimiwa John Mnyika na napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba liko tatizo kubwa sana la maji katika Majimbo mbalimbali, lakini pia ni kweli kwamba Wizara yangu imepanga na imeanzisha utekelezaji wa miradi mingi sana katika Majimbo mbalimbali na Wilaya zote hapa nchini na kwamba miradi mingi haijakamilika kutokana na ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tunatoa ripoti ya upatikanaji wa maji katika nchi kila wakati tunapokuja kuingia Bungeni (tunatoa kwenye Kamati yetu ya Kilimo, Mifugo na Maji) na tumeendelea kufanya hivyo tangu Mheshimiwa Mwandosya aliposimama siku ile akatoa ahadi hiyo. Kama ripoti hiyo inatakiwa hapa ndani tutaendelea kuitoa na hapa ndani kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge wote, lakini kama unavyojua Kamati za Bunge zinafanya kazi kwa niaba ya Bunge lako.

Na.100

**Bwawa Lililopo katika Kijiji cha Itombololo**

**MHE. DEO K. SANGA** aliuliza:-

Katika Kijiji cha Itombololo kuna bwawa kubwa ambalo huko nyuma wananchi walikuwa wanapata samaki lakini sasa bwawa hilo limejaa magugu na samaki hawapatikani tena.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa magugu hayo ili wananchi waendelee kupata samaki?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Njombe Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa la Itombololo lenye ukubwa wa hekta 1,200 lilijengwa na Serikali mwaka 1961 kwa matumizi ya binadamu na viwanda. Bwawa hilo lilipandikizwa samaki aina *black bass* ambao asili yao ni nchi za Ulaya na Amerika Kaskazini ambako kuna ubaridi. Baadaye samaki aina ya perege walionekana na wananchi wanaoishi jirani na bwawa hilo na walianza kuwavua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuongezeka kwa idadi ya wavuvi na zana za uvuvi, uwepo wa uvuvi haramu, matumizi makubwa ya maji ikiwa ni pamoja na maji yanayotumiwa na *Kibena Wattle Company* ya Njombe na mabadiliko ya hali ya hewa yaliyosababisha upungufu wa mvua, kina cha maji katika Bwawa la Itombololo imeendelea kupungua sanjari na kupungua kwa wingi na ukubwa wa samaki wanaovuliwa katika bwawa hilo. Aidha, shughuli za kilimo na ufugaji zimesababisha mmomonyoko wa udongo na kujaza sakafu ya bwawa. Vitendo hivi vimesababisha kina cha bwawa la Itombololo kupungua hadi kufikia kina cha mita mbili kutoka mita nne za awali, vitendo hivi vimesababisha kuota kwa magugu maji katika bwawa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Bwawa la Itombololo linasimamiwa na uongozi wa Vijiji vya Muhaji na Lusisi, Wilaya ya Wanging'ombe. Kwa kuwa Menejimenti ya Bwawa hilo inahusisha wadau wengi, Wizara itashirikiana na wadau husika kufanya utafiti ili kubaini aina ya magugu maji yaliyoota kwenye bwawa hilo kwa lengo la kutathimni gharama za kuyaondoa

ikiwa ni pamoja na kudhibiti shughuli za uvuvi kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya mwaka 2003 na Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009. Lengo ni kuongeza wingi na ukubwa wa samaki waliopo ili kuwezesha uvuvi endelevu kufanyika katika bwawa hilo.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Waziri nina maswali ya nyongeza. Kwa sababu swali la msingi nimeelezea kwamba bwawa hili wananchi wa Wilaya ya Njombe hususani Njombe, Mtwango, Makambako na vijiji vinavyozunguka Bwawa hilo kama alivyotamka Waziri, tulikuwa tunapata samaki kupitia bwawa hilo na wananchi hao walikuwa wanapata mapato mbalimbali kupitia samaki wanaopatikana katika eneo hilo. Je, Serikali ni lini itaondoa magugu hayo ili iweze kupanda samaki ili wananchi wa maeneo hayo na Wilaya nzima tuendelee kupata kipato na kupata afya kutokana na virutubisho vya samaki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Waziri atakuwa tayari sasa kuongozana na mimi na Wabunge wa Wilaya ya Njombe akiwemo Injinia Lwenge na Mheshimiwa Spika ili aongozane na wataalam twende pamoja tukaone tatizo lililoko eneo hilo ili liweze kutatuliwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri majibu, ukizingatia lishe ni muhimu!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika majibu yangu ya msingi, wataalam wangu wako tayari kwenda kufanya tathmini ya aina ya magugu ili hatimaye mbinu sahihi iweze kujulikana ni namna gani yatatumika pamoja na gharama zake.

La pili, kwanza nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi anavyofuatilia ufanisi wa bwawa hili kwa manufaa ya wananchi wa Wilaya ya Njombe. Napenda kumuahidi tu kwamba wakati wowote atakapokuwa tayari Wizara yangu iko tayari kwa kazi tutapanga tufuatane na wataalam ili kwenda kuangalia hali ilivyo na kujua namna ya kufanya. Ahsante sana.

Na. 101

**Maeneo Yaliyopitiwa na Miundombinu ya Umeme - Bukoba**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Katika kutekeleza miradi ya kupeleka umeme Bukoba Vijijini kuna maeneo ambayo yamepitiwa na mitandao na mifumo ya umeme hadi vijiji vya mbele zaidi, Kijiji cha Igombe katika Kata ya Nyakato ni moja ya vijiji hivyo ambapo waya za umeme zimepita juu lakini chini hakuna umeme na mazao ya wananchi katika vijiji hivyo yameharibiwa sana wakati wa kusimika nguzo kupeleka umeme vijiji vya mbele. Je, Serikali haioni kuwa huu ni uonevu mkubwa kwa wananchi kama hawa wa Kijiji cha Igombe?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini kama ifuatavyo:-

Kijiji cha Igombe katika Kata ya Nyakato kimeshaingizwa kwenye mpango wa kupatiwa umeme kupitia mpango kabambe wa *REA* awamu ya pili ambao unatekelezwa Mkoani Kagera na Mkandarasi aitwae *Urban and Rular Engeneering Limited,* tayari mkandarasi ameshafanya upimaji *(survey)* na kuweka vigingi *(pegs)*. Wigo wa kazi unahusisha kujenga...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tupunguze kelele.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, wigo wa kazi unahusisha kujenga kilomita mbili za msongo wa *volt* 400 na kusimika transfoma moja ya *KVA* 50. Kazi inaendelea katika Mkoa wote wa Kagera na utekelezaji wake umefikia 55%. Inategemewa vijiji vyote vilivyomo ndani ya wigo wa kazi pamoja na Kijiji cha Igombe vitaunganishwa umeme ndani ya mwaka huu na wananchi wote wanaohusika watapata huduma hii.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii na pia namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Moja, nina taarifa kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri alitembelea Mkoa wa Kagera kama alivyosema kwamba Mkoa wa Kagera unaunganishiwa umeme, lakini hakufika katika Wilaya za Bukoba Vijijini. Napenda kujua ni kwa nini hakufika Bukoba Vijijini kuona kazi inavyoendelea?

Pili, hili alilolisema kwamba vijiji vinavyounganishiwa umeme na Igombe ikiwemo ni kwamba umeme huu unakwenda sehemu za mijini, unapita barabara kuu hauingii ndani ya vijiji kule ndani ambako wananchi wapo, je huu ndiyo umeme vijijini?

Swali lingine, sasa kuna maeneo mengi ambayo hayana umeme kabisa pale Bukoba Vijijini, Kata nzima ya Lukoma haina mpango wa umeme, Vijiji vya Kata ya Kibirizi, Kata nzima ya Kikomero haziko kwenye mpango huu, Kata nzima ya Mugajwale haiko kwenye mpango, Izinda yenyewe ni mjini tu pale kama nilivyosema, kule Buturage hakuna mpango huo, Bujugo kazi haijaanza na sasa hivi ni mwaka wa pili wamechimba mashimo. Je, kazi hii itaanza lini na vijiji hivi vitaingizwa lini kwenye mpango?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango yote na makaratasi ya Mheshimiwa Rweikiza ya kufuatilia umeme, yamejaa ofisini na nimeyaona nimeyapeleka ofisini kwangu, siyo kwa nia mbaya kwamba sikufika kwako, lakini ni kutokana na mapendekezo mengi aliyoleta ofisini kwetu nimeyatengea muda ili nije niyashughulikie kikamilifu, hilo swali la kwanza nimelijibu.

Swali la pili, kwamba kuna Kata nyingi namna hii hazijafikiwa, sina jibu la moja kwa moja. Namuomba *Regional Manager* wa Kagera na *District Manager* wa Bukoba Vijijini, mwende muangalie hayo maeneo anayoyasema yako kwenye *REA II* au hayapo na kama hayamo mtutafutie *scope* tuweze kujua kuwa tutayaweka kwenye *REA II additional scope* au kwenye *REA III* ambayo itakuja nchi nzima.

**MHE. SELEMAN S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa juhudi kubwa aliyofanya baada ya mawasiliano marefu, lakini suala hili nimekuwa nikilirudia mara kadhaa. Kule Kisarawe tuna muda mrefu sana tunasubiri umeme, lakini danadana imekuwa kubwa sana. Najua Mheshimiwa Naibu Waziri analifuatilia hili kwa karibu, lakini nataka kujua kwamba ni jinsi gani Serikali imejipanga kumlazimisha mkandarasi hivi sasa aweze kushusha transfoma na kupeleka umeme katika *line* inayotoka Kisarawe kwenda Maneromango mpaka Msanga. Nataka kupata *commitment* ya Serikali katika hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi anayefanya kazi sehemu ya Kisarawe, Mkoa wa Pwani ndiye aliyeko sehemu ya Morogoro na ndiye aliyeko sehemu ya Lindi, napenda kusema siridhishwi na utendaji wake wa kazi. Nitakapotoka hapa nakwenda kukutana na Mkandarasi huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kumweleza Mkandarasi aweke *sub-contactors* ili aweze kutimiza kazi hiyo na mojawapo ya kazi za kufanya ni kuweka hiyo transfoma

inayokwenda Maneromango, hili ni agizo kwa Meneja wa Kisarawe kwamba anza kutengeneza mchakato wa kupata *transfoma* moja ya 50 *KVA* siyo tatizo. Kwa hiyo, ni majukumu ambayo *District Manager* anapaswa kutekeleza. Narudia kutangaza ninyi Mameneja wa Wilaya na Mikoa muwasiliane na Wabunge kusudi mnipunguzie mzigo hapa Bungeni.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la msingi la Mheshimiwa Rweikiza ameongelea nyaya zinazopita juu na wananchi wanaoishi katika maeneo hayo kukosa umeme. Takribani sasa ni mwaka mmoja na nusu tangu Mheshimiwa wa Nishati na Madini Simbachawene akiwa Naibu Waziri wa Nishati mpaka sasa amekuwa Waziri wa Nishati nikiongelea suala kama hili na kwa Mheshimiwa Naibu Waziri nimeshakwenda zaidi ya mara tatu.

Sasa ningependa kujua eneo la *TX* pale Ilemela pamoja na Maliganya Kayenze Ndogo kuna nyaya zimepita juu na tataizo lilikuwa ni transfoma na nikaambiwa suala hili liko kwa Sophia, mpaka leo ni mwaka na nusu. Sasa ningependa kujua ni lini eneo hili watashushiwa hiyo transfoma na umeme uwake?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri kwa kifupi, Waheshimiwa Wabunge tusikilizane kelele zimezidi, vikao vimekuwa vingi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tatizo la nyaya kupita lengo la miradi hii ilikuwa ni kuhakikisha tunafikisha umeme karibu na wananchi tukiwa tunalenga kufika kwenye vijiji au kwenye Makao Makuu ya Wilaya, ikatokea kwamba maeneo mengine yakapitwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango tunaokuja nao ni kwamba tunataka kushusha zile nyaya ziwafikie wananchi. Katika mpango huo zimeagizwa transfoma; mahitaji ya nchi nzima ni transfoma 4000. Kwa hiyo, transfoma 4000 zitaletwa, tutashusha umeme kusudi watu wapate umeme, lakini suala la Mwanza siyo tatizo la Mariganya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nimemwelekeza *Zonal Manager* wa Mwanza kwamba hii transfoma moja ya Mariganya isituletee ugomvi mimi na wewe Mbunge. *Zonal Manager* wa Mwanza na *District Manager* mwende Mariganya mseme hiyo transfoma haiwezi kupatikana duniani kusudi mimi nijue.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la mwisho la Mheshimiwa Lolesia Bukwimba litaulizwa na Mheshimiwa Maria Hewa.

Na. 102

**Hitaji la Umeme Vijiji vya Busanda**

**MHE. MARIA I. HEWA (K.n.y. MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA**) aliuliza:-

Je, ni lini umeme utawaka katika Vijiji vya Ndelema, Imalampaka, Kamena, Nyalwanzaja, Buyagu, Nyabulolo, Kashishi, Nyakamwaga, Shilungule, Busanda, Msasa Nyamalimbe, Nyakagwe, Nyakagomba, Nungwe, Nyamwilolewa, Kageye, Buziba katika Jimbo la Busanda, Wilayani Geita?

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE (NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini kwa kushirikiana na *TANESCO*, imefanya upembuzi wa awali kwa kazi ya kupeleka umeme katika vijiji vya Ndelema, Imalampaka, Kamena, Nyalwanzaja, Buyagu, Nyabululo, Kashishi, Nyakamwaga, Shilungule, Busanda, Msasa, Nyamalimbe, Nyakagwe, Nyakagomba, Nungwe, Nyamwilolewa, Kageye na Busiba vilivyomo katika Wilaya ya Geita, Mkoa wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia upembuzi huo, kazi ya kupeleka umeme katika vijiji hivyo itahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa Kilovolt 33 yenye urefu wa kilomita 95.3; ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa Kilovolt 0.4 yenye urefu wa kilomita 54.5; ufungaji wa transfoma 21 zenye uwezo mbalimbali; na kuunganisha wateja wa awali wapatao 2,056. Gharama ya mradi huu inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 5.05.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufinyu wa bajeti, vijiji vilivyotajwa havikujumuishwa kwenye Mpango Kabambe wa Umeme Vijijini Awamu ya Pili chini ya ufadhili wa Mfuko wa Nishati Vijijini *(REF)*. Hata hivyo, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*), inatafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza kazi hiyo ikijumuisha vijiji vilivyotajwa ambavyo vitapewa kipaumbele katika awamu inayofuata kama ilivyoainishwa kwenye *National Electrification Investment Prospectus* kwa mwaka wa 2015/2016.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maria Hewa, swali la nyongeza!

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili tu mafupi ya nyongeza.

Kwanza, kutokana na jibu la Mheshimiwa Waziri anasema Serikali imefanya upembuzi yakinifu, maneno ambayo kwangu huwa ni kero kweli kweli! Imefanya kwa hivyo vijiji husika, wakati huo huo anasema vijiji vilivyotajwa ambavyo vimefanyiwa upembuzi yakinifu, havikujumuishwa (naomba swali langu lieleweke) kwenye mpango kabambe wa Umeme Vijijini, wakati huo huo inatafuta fedha. Hivi majibu haya mbona kama ni mkorogo tu wa Kiswahili kiasi ambacho wanakijiji wa Busanda au wa Jimbo la Busanda hawaelewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo, je, ni nini hiki ambacho kinafanyika, ni upembuzi, hela inatafutwa, halafu haipo?

Pili, kama suala hili litafanikiwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016, ni kwa nini watakapofanikiwa katika kuvipelekea vijiji hivi umeme katika Jimbo la Busanda wasiunganishe na taasisi kwa mfano kwenye sekondari, zahanati na vituo vya afya ili suala zima katika Jimbo hili la Busanda wakatoka jumla?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zote zinazoletwa Serikalini kama utatoa majibu bila kuwatuma watalaam kwenda kuangalia, utakuwa unawadanganya watu. Hata yote yanayoulizwa hapa! Ndiyo maana nasisitiza mwende kwa Mameneja; *District Manager* na *Regional Manager* kusudi wao wapitie. Kule kupitia, kufanya tathmini, ndiyo unaitwa upembuzi.

Kwa hiyo, kwa sabau mradi huu haukuwa kwenye *REA Phase II* na Mheshimiwa Mbunge huyu alishaleta swali hili mwezi Januari, tukatuma watalaam waende waangalie. Kile kitendo cha kuangalia na kutathmini ule mzigo wa kazi ambao ni bilioni 5.05 ndicho kinachoitwa upembuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotakiwa sasa ni kwamba mwaka ujao 2015/2016 tutatafuta hiyo pesa bilioni 5.05 tuweze kujenga. Lakini Waheshimiwa Wabunge ikitokea zikapatikana hizo pesa leo nawahakikishia, kabla ya mwisho wa mwezi wa sita naweza kujenga mradi huo. Kwa hiyo, upembuzi hauepukiki. Kama unafanya kazi kisayansi, upembuzi ni lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niwaeleze jambo moja, siyo kwa sababu ya eneo lako tu, lakini ni kwa sehemu zote. Ni maelekezo ya Serikali na ni mipango yetu sisi Wabunge wa Bunge la Kumi. Tulikubaliana kwamba umeme ni lazima upite kwenye makanisa, kwenye misikiti, upite kwenye shule, upite kwenye zahanati. Hatupeleki umeme kwenda kuangazia miti, taasisi ni lazima. Ninyi watalaam, mtaniponza na mimi nitawaponza kabla sijaponzwa. Hakikisha hizo taasisi zinakuwa na umeme. Hatupeleki umeme kwa mtu kabla ya taasisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tangazo moja. Kuna mahali watu wamechimba nguzo kama kule Arusha - Arumeru Magharibi, kama sehemu za Karagwe, sehemu za Bunda halafu mtu ameshachimba mashimo ameweka nguzo halafu anakuja anahamisha nguzo. Hamruhusiwi kuhamisha nguzo hizo mpaka mpate jibu kutoka kwenye mamlaka; na mwenye mamlaka ni Waziri wa Nishati na Madini ndiye atasema hapa ulichimba, umekosea. Lakini hakuna kilichokosewa, mahali nguzo zilikopelekwa kuna Watanzania na kazi yetu sisi ni kuangaza Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa!

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona, nami niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sana nimekuwa nikiulizia hapa kuhusu suala la Jiji la Mbeya na zile Kata za pembezoni kama Kata ya Iduda, Itezi, Mwansanga, Tembela, Nonde na nyinginezo. Hizi Kata za pembezoni zimekuwa hazina umeme kwa muda mrefu sana na hili tatizo limekuwa sugu. Nimeongea na Meneja wa Mkoa wa *TANESCO* mpaka tumekwenda kwenye mikutano na wananchi, lakini mpaka leo hakuna kilichofanyika. Nilikuwa namhitaji Mheshimiwa Naibu Waziri atoe tamko hapa atueleze wananchi hawa wa Jiji la Mbeya, Kata za pembezoni kwa muda mrefu hakuna umeme na ahadi zimekuwa hazitekelezeki, ni lini zitatekelezeka? Nashukuru.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE (NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kata katika Jiji la Mbeya na viunga vyake kwamba havina umeme, sawa, nataka Meneja wa Mbeya na Meneja wa Mkoa mlete taarifa, mnieleze, je, mkandarasi amechelewa zipo kwenye *scope* au haziko kwenye *scope!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, bila kupata upembuzi na taarifa za kitalaam siwezi kufanya lolote. Lakini nakuahidi kwamba katika mizunguko yangu niliyopangiwa na mkuu wangu wa kazi, Mheshimiwa Simbachawene, Mbeya ipo kwenye programu. Nitafika Mbeya sehemu unayoisema, nione Kashenamboni kwamba Jiji la Mbeya halina umeme.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saidi Mtanda, swali la nyongeza!

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona; na upande huu uwe unawaangalia sana, maana huku ndiyo nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo tu. Kwanza ni kuipongeza Serikali kwa sababu asilimia 98 ya Vijiji vya Mchinga vitapata umeme kutoka vijiji viwili sasa vijiji 48 kati ya vijiji 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kufahamu sasa kutoka Serikalini, kwa kuwa mkataba wa kuwasha umeme ilikuwa ni mwezi wa tano na sasa tupo mwezi wa tatu kuelekea mwezi wa nne, je, ifikapo mwezi wa tano umeme kwenye Jimbo la Mchinga wenye thamani ya shilingi bilioni 5.9 utakuwa umewaka?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru kwa kupongeza. Unajua ukiwa hapa mtu akakupongeza, unapata nafuu kidogo. Nakushukuru sana kwa kunipongeza!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamjibu, niseme jambo moja. Akina Mheshimiwa Mzee Arfi wanakumbuka, akina Mheshimiwa Mama Buyogera mnakumbuka. Mimi nilikuwa Mwenyekiti wa suala la Mtwara katika ushamiri na kuweza kuvuna rasilimali. Kazi tuliyopendekeza kwenye Kamati na nimeamuru wale Watendaji wetu, vijiji vyote kutoka Mtwara linakopita bomba la gesi, ninyi mtulie.

Katika mojawapo ya majukumu yetu tutahakikisha mnapata umeme kabla gesi haijaja kuchoma umeme. Kwa hiyo, kuanzia Mtwara, Madimba wapi huko, wote wanapata umeme kabla gesi haijaja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mtanda unashukuru asilimia 98, nitahakikisha itakuwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala la utekelezaji wa malengo, nisingependa kuwadanganya watu. Mimi ni mtekelezaji na ninasimamia watekelezaji. Kama Wizara ya Nishati Kitengo cha *REA* kitapata pesa mlichokiahidi, nawahakikishia umeme utawaka Mei, Juni na sehemu zote. Momba umeme utawaka, Ubungo nitakuja, sehemu zote nitakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la muhimu bila kudanganyana, ni lazima zile pesa za *REA* zipatikane na wale watenda kazi wapate pesa. Wakipata pesa, kazi ya kujenga umeme nimeshaielewa, ni kazi rahisi.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri ameitaja Momba kwamba umeme utawaka, swali langu lilikuwa dogo tu kwamba mwaka wa fedha uliopita tuliitengea *REA* fedha na mpaka sasa *REA* imepata karibu shilingi bilioni 33 tu na bado shilingi bilioni 105 Serikali haijapeleka fedha yoyote kule.

Nataka nifahamu moja ya sababu inayokwamisha miradi ya Momba, nguzo zimesimama lakini nyaya hazijafika. Ni kwa nini mpaka sasa Serikali haijapeleka shilingi bilioni 105 za *REA* ili zikakamilishe miradi ya umeme kote? *(Makofi)*

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE (NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi hili swali ni kweli Serikali haijapeleka hizo pesa shilingi bilioni 105, lakini mimi nilipokuangalia usoni nilishajua swali lako, nikakwambia mkileta pesa tunatekeleza. Kimsingi hili swali Waziri wa Fedha yupo humu ndani, anisaidie asimame aseme. Nisiseme ambayo wakubwa zangu hawajanituma. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, majibu ya nyongeza!

**MHE. MWIGULU L. M. NCHEMBA (NAIBU WAZIRI WA FEDHA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la fedha za *REA*, kwanza Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kwamba tuliingia na kiporo ambacho tulitoka nacho mwaka wa fedha uliopita.

Wizara ya Fedha tayari ilishalipa zote zile ambazo tulivuka nazo mwaka na kwa sasa tumeweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba fedha zile za *REA* pamoja na fedha nyingine zinazohusu mifuko maalum zikishakusanywa, zikapita mfuko mkuu, zipelekwe moja kwa moja kwenye mifuko husika kabla ya mgao mwingine wa matumizi mengineyo kuweza kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nalihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara imejipanga kuhakikisha kwamba fedha hizo ambazo zinatakiwa kwenda kwenye umeme zitakuwa zinakwenda sawasawa kama ambavyo zimekusanywa kuhakikisha kwamba hatuvuki na deni katika mwaka wa fedha huu tunaoenda nao.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kasulu Vijijini lina zaidi ya vijiji 60; na Serikali ilituahidi kutuletea umeme. Tangu tarehe moja, mwezi Agosti, 2012 nina barua ambayo imesainiwa na aliyekuwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Simbachawene ambaye leo ndiye Waziri.

Nimewasiliana na Mkandarasi, barua ilikuwa inasema tutaletewa umeme katika vijiji 23. Lakini baada ya kuwasiliana na Mkandarasi akaniambia kwamba atapeleka umeme kwenye vijiji tisa tu. Hata hivyo vijiji tisa, hakuna nguzo iliyokwishawekwa katika Kijiji chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupata maelezo kwa Serikali kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kasulu Vijijini, ni lini watapata umeme nao waweze kuhesabika katika Watanzania wenzao?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri!

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE (NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekutana na *Zonal Manager* anayesimamia Kanda ambayo Kasulu imo. Nimeongea na *Regional Manager* wa Kigoma kuhusu tatizo la Kasulu. Jibu nililolitoa mwanzoni kuhusu suala la Mheshimiwa Ole-Medeye na *DC* wa Arusha, linahusika na Kasulu vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambayo wapimaji wamepima halafu wakawaambia wananchi kateni mazao yenu tutawapatia umeme, halafu mtu anakuja anasema hawawezi kupata umeme, hilo suala siyo la Mkandarasi. Inapotokea kutofautiana, akimbie aende kwa *Regional Manager* wa *TANESCO* na *Regional Manager* wa *TANESCO* aende kwenye *zone; zone* wawasiliane na *REA* tuweze kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwasha umeme Tanzania, ndiyo jukumu letu, hatubagui, hatuchagui, Tanzania ni moja. Kwa hiyo, vijiji vyenu hivi 23 na hivi tisa; tisa kutotengenezwa ni matatizo ya Mkandarasi. Muulize Mkandarasi atakwambia, niko naye shingo moja, tunakabana hii miradi tisa inatekelezwa.

Sasa tatizo nililonalo ni hii tofauti kurudisha kwenye 23 na nitahakikisha 23 inatekelezwa na inatekelezwa kwa sababu Waziri mwenye dhamana ya pesa ameshasema, kwamba zile

shilingi bilioni 105 zitakuja na zikishafika, mimi kote nitafika Mheshimiwa Buyogera ili mambo yawe mazuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mshama!

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya yetu ya Misenyi kuna vijiji takribani kama 24 vilikuwa vimeahidiwa umeme na kweli mashimo na nguzo zimewekwa. Sasa nimemsikia Waziri anasema kulikuwa na tatizo la fedha, sawa. Je, ile Kata ya Mshasha Kijiji cha Bulembo ambapo kila kitu kimekamilika, imebakia kuwashwa na Kijiji cha Ishozi ambako kumekamilika kila kitu, ni kuwasha; nauliza ni lini utawawashia umeme ili tuone kwamba ile Shule ya Ishozi inapata umeme na kuendeleza masomo ya sayansi?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi!

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE (NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bulembo nimefika, Ishozi nitakwenda baada ya Pasaka. Tatizo la Mkandarasi *Urban and Rural* ni kwamba transfoma zake zimekwama kwa sababu ya matatizo hayo ya pesa tunayoyazungumza. Nilikwenda Bulembo, mapokezi yalikuwa mazuri, mizigo yake ikishafika, tulikubaliana kwamba wanapowasha niende nibonyeze kitufe cha kuwasha umeme. Kwa hiyo, vifaa vikifika tunawasha umeme mara moja.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu kwamba juzi tulikuwa na kikao kati ya Kamati ya Bajeti pamoja Wizara yake, vilevile watu wa *REA* walikuwepo na tulizungumza nao kuhusu suala hili la kusambaza umeme vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililopo ni kwamba *REA* hawapati fedha za kutosha na inavyoelekea ni kwamba kile chanzo cha fedha cha *REA* ni kidogo. Sasa Waziri anasema nini au Serikali inasema nini? Kwanini wasije na pendekezo hapa Bungeni la chanzo kingine cha fedha kwa *REA*, ili *REA* iweze kupata fedha za kutosha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba nchi hii umeme umewaka kwa sababu ushahidi ni kwamba kijiji chochote ambacho umeme umewaka maendeleo yake pia yameonekana kwamba yanakwenda kwa kasi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE (NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Selasini lake siyo swali, ni pendekezo. Nimezunguka sehemu za nchi hii watu wote wanataka umeme.

Kwa hiyo, Wizara yetu sisi italeta mapendekezo, iyapitishe kwenye Kamati zenu, myachakate, tuweke tozo ambayo itaweza kuharakisha Tanzania yote iwake kwa wakati mmoja. Kwa sababu hakuna Tanzania nusu na Tanzania nzima. Tanzania yote ni moja, tunaleta mapendekezo myachakate halafu tupitishe tozo kusudi watu wapate umeme. Umeme ni mzuri sana bwana! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Maswali yameisha. Sasa ni wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; kuna wageni 29 wa Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla, Mbunge, ambao ni wanakwaya kutoka *Tanzania Assemblies of God, Nzega*

*Christian Centre,* wakiongozwa na Mchungaji Andrew Samuel Kayamba. Wako wapi? Karibuni sana Bungeni hapa. Mbunge wenu anachapa kazi. Ahsanteni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 35 wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge na Waziri wa Nchi, Sera, Uratibu na Bunge, ambao ni viongozi wa CCM na Umoja wa Vijana wa CCM kutoka Wilaya ya Mbarali wakiongozwa na Ndugu Ibrahimu Mwakabuhama; Kamanda wa Umoja wa Vijana wa Wilaya ya Mbarali. Wako wapi hao? Karibuni sana Bungeni hapa. Ahsanteni kwa kazi nzuri Mbarali na Mheshimiwa Waziri anachapa kazi. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge na Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kutoka Jimboni kwake Mbozi Mashariki, Mkoa wa Mbeya. Wako wapi hao? Karibuni sana.

Wageni watano wa Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, wakiongozwa na Mheshimiwa Ashura Antony, Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa CCM Wilaya ya Ruangwa. Wako wapi hao? Karibuni sana kutoka Ruangwa. Ahsante sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Wageni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 100 kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma, Tawi la Mbeya. Wanafunzi 100 kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma kutoka Tawi la Mbeya. Karibuni na jana tulipitisha Azimio linalohusu Utumishi wa Umma. Tunategemea mtakuwa Watumishi wa Umma wenye maadili. Karibuni sana kwa mafunzo.

Wanafunzi 35 kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(DARUSO)* karibuni sana. *(Makofi)*

Ndugu Asha Nassoro na Ndugu Tatu Bunduki kutoka Dodoma. Wako wapi?

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni waliotutembelea.

Matangazo ya kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Prof. Peter Msolla anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuwa leo tarehe 26 Machi, saa 7.00 mchana kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo. Kikao hicho kitafanyika katika Ukumbi Na. 227, Jengo la Utawala.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Selemani Zedi, anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* kwamba leo saa 7.00 mchana kutakuwa na Kikao cha Kamati katika Ukumbi Na. 231, ghorofa ya pili, Jengo la Utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Joelson Lugaha Mpina, anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara kwamba leo saa 7.00 kutakuwa na Kikao cha Kamati katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Said Mtanda, anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwamba kutakuwa na Kikao leo saa 5.00, lakini saa 500 hapana. Iwe ni saa 7.00. Ukumbi haujatajwa! Kutakuwa na Kikao, lakini Ukumbi haujatajwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, Ukumbi haupo, naomba ulete tangazo ni Ukumbi gani kutakuwa na Kikao saa 7.00 siyo saa 5.00 asubuhi.

Tangazo lingine ni kwamba leo saa 7.00 mchana kutakuwa na Ibada ya Wabunge na Watumishi wa Madhehebu ya *CCT* katika Ukumbi wa Msekwa, ghorofa ya pili. Kanisani saa 7.00 mchana.

Mwenyekiti wa Kamati ya TAMISEMI Mheshimiwa Khamis Kigwangalla, Mbunge, anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya TAMISEMI kwamba leo saa 7.00 kutakuwa na Kikao cha Kamati katika Ukumbi wa Msekwa 'C.'

Mheshimiwa Christowaja Mtinda, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote waliosoma Msalato kwamba kutakuwa na Kikao katika Ukumbi wa Pius Msekwa 'C.'

Mwisho wa matangazo.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwongozo wa Spika!

**MWENYEKITI:** Katibu!

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Mwenyekiti!

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Blandes!

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MBUNGE FULANI:** Kanuni ipi?

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Nimesimama hapa kwa mujibu wa Kanuni ya 48(3). Nasikia naulizwa Kanuni ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ambalo limenifanya nisimame hapa ni jambo ambalo linahusu masharti ya jumla kuhusu jambo la dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Serikali ilielekeza wamiliki wote wa pikipiki, kwa maana ya bodaboda kwamba wazifanyie usajili upya. Zoezi hili limekwenda lakini limekuwa na matatizo hasa katika Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera una Wilaya zipatazo karibu nane ikiwemo Wilaya ya Karagwe pamoja na Kyerwa na Ngara na sehemu nyingine. Usajili huu umekuwa ukifanyika Mkoani Kagera, kwa maana ya Bukoba Mjini. Sasa mtu wa Karagwe, Kyerwa na kutoka Ngara umbali karibu kilometa 300 na zaidi kwenda kufanya usajili huo.

Pia pale Mkoani wananchi wetu wanakaa Mkoani wakisubiri usajili kwa muda wa siku mbili, tatu, wiki hata wiki nne na hata mwezi, sababu kubwa ni kwamba mtandao haufanyi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ni kwamba wakati tangazo hili linatoka, wananchi hawa walitangaziwa kwamba watasajili pikipiki kwa shilingi 50,000/=. Sasa kwa bahati mbaya wamekuja kuongezewa tena shilingi 10,000/= ambayo ni hela ya ziada, tunaambiwa kwamba ni ya Zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangazo hili linawataka wenye bodaboda wawe wamesajili pikipiki zao ifikapo tarehe 31 mwezi huu wa tatu, kwa maana ya siku kama nne ambazo zimebaki na wakati nchi nzima zoezi hili limeendelea kukwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itueleze ni kwa nini wasipeleke huduma hii kwenye Wilaya kurahisisha huduma hizi kwa watu wenye bodaboda na hasa huko Karagwe na sehemu nyingine za nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa kuwa zoezi hili linaisha tarehe 31 mwezi wa tatu mwaka huu, ni kwa nini Serikali isiongeze muda huu angalau tukafika mpaka mwezi wa sita au Desemba wananchi wenye bodaboda wakapata muda wa kutosha kusajili pikipiki zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nafikiri Serikali imelisikia, italitolea maelezo.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mwongozo wa Mwenyekiti!
**MWENYEKITI:** Mwongozo wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Silinde!

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii. Nami nataka unipatie Mwongozo wako unaotokana na Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi hapa Bungeni safari moja kwamba wakati wowote panapotokea vifo vyenye utata, hususan vile vinavyotokana na vyombo vya dola *against* wananchi, Serikali itatumia Sheria ya *Inquest Act* kuhakikisha inaunda vyombo vya kiuchunguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Mji wa Tunduma palitokea fujo ambazo zimepelekea kifo cha kijana mmoja anaitwa Sajo, pamoja na mama mmoja mjamzito ambaye alipigwa na bunduki tumboni ambayo ilipelekea mimba yake kuharibika na kuondolewa kizazi.

Sasa nilikuwa nataka Kauli ya Serikali hapa na iwe ni Mwongozo wako, ni kwa nini sasa Serikali kupitia Kauli ya Waziri Mkuu ambayo ndiyo ahadi yake Bungeni isiunde chombo cha kiuchunguzi kwenda kuchunguza huu utaratibu unaoendelea wa vyombo vya dola kuua wananchi wasiokuwa na hatia, wakiwemo mama wajawazito kama ambavyo imetokea katika Mji wa Tunduma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mwongozo wako juu ya jambo hilo. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khalifa.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami naomba nitumie Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mgawanyo wa madaraka katika nchi yetu tuna vyombo vitatu na kila mmoja wetu anajua hapa ni Bunge, Serikali na Mahakama. Kwa muda mrefu chombo cha Bunge kimekuwa kikifanya kazi yake vizuri sana. Lakini katika siku za hivi karibuni

inaonekana kuna tatizo kubwa la Bunge kushindwa kufanya kazi yake kwa matatizo ya fedha. Kamati za Bunge zinakutana Wabunge wanakopwa; safari za kikazi za Wabunge nje ya nchi zinashindwa kufanywa kwa sababu, Bunge halina pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba utupe Mwongozo wako, huo ni mkakati maalum wa Serikali wa kuli-*paralyse* Bunge au ni tatizo la ukosefu wa fedha Serikalini? Au ni Bunge lenyewe linafanya hiyana halitaki kufanya kazi yake ipasavyo? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Toa hoja!

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tutumie muda mchache tujadiliane na Serikali na hapa itoe kauli, hali hii inasababishwa na nini? Maana kila leo tunaambiwa kuwa Serikali inakusanya zaidi, inakusanya zaidi, lakini Wabunge au Bunge linaumizwa kwa makusudi au ni kwa sababu Bunge halina Mfuko wake, linategemea Ofisi ya Waziri Mkuu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja tuweze kujadili suala hilo! *(Makofi)*

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hamna hoja hapa, kaeni tu wote. Hilo tumeshalitoa, tutalisisitiza baadaye. Mheshimiwa Mwanjale! *(Kicheko)*

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka nifanye masahihisho tu ya tangazo ambalo limepita kwamba wanaotakiwa kwenda kwenye ibada pale ni watu wa *CCT*. Nilikuwa naomba kusema ni *CCT* na *PCT* wote wanatakiwa wawepo pale kwenye ibada. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Soma lilivyokuwa limeandikwa. Mheshimiwa Mnyika!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 38, Kipengele cha (3) na cha (5) juu ya Maswali kwa Waziri Mkuu na nitaomba nisome; "Kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu kitakuwa kila siku ya Alhamisi na hakitazidi dakika 30," kila siku ya Alhamisi, 38(5). "Iwapo siku hiyo kwa sababu maalum Waziri Mkuu hatakuwepo Bungeni, hakutakuwa na Maswali kwa Waziri Mkuu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mapema leo hakukuwa na maswali kwa Waziri Mkuu, lakini yanakosekana Maswali kwa Waziri Mkuu wakati ambapo nje ya Bunge kuna Kauli nyingi za Waziri Mkuu. Vyombo vya Habari vimekuwa vikiandika "Hesabu za *BVR* zimegoma;" vimeandika "Kauli ya *NEC,* ni vigumu Kura ya Maoni kufanyika Aprili;" Kura ya Maoni ambayo uratibu wake ni chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Vile vile Vyombo vya Habari vimekuwa vikiandika "Mashine za *BVR* zaitesa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, yatumia siku 30 kuandikisha Njombe. Waziri Mkuu asema Kura ya Maoni iko palepale."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *NEC* inasema ni vigumu Kura ya Maoni kufanyika Aprili, Waziri Mkuu anasema Kura ya Maoni iko palepale. Maswali haya yangeweza kupatiwa majibu hapa Bungeni kama Mheshimiwa Waziri Mkuu angekuwepo kujibu maswali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba muongozo wako ili Kaimu Waziri Mkuu alieleze Bunge ni sababu ipi maalum iliyofanya Waziri Mkuu asiwepo Bungeni leo na ni lini Waziri Mkuu atakuja kutoa majibu hapa Bungeni? Siyo kupitia tu Maswali kwa Waziri Mkuu kwa sababu yako mbele sana, ni lini atakuja mapema ndani ya siku chache zijazo kutoa Taarifa ya Serikali humu

Bungeni kuhusu uozo mzima ulioko kwenye mfumo wa *BVR*? Vilevile aseme ni kwa nini Serikali haikubaliani sasa na ukweli kwamba haiwezekani Kura ya Maoni kufanyika tarehe 30 Aprili? Iahirishe zoezi la Kura ya Maoni, nchi ielekee kwenye maandalizi ya Uchaguzi Mkuu, tuweze kufanya uchaguzi huru na haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Miongozo yote hiyo itatolewa maelezo baadaye. Kwa hiyo, tunaendelea na ajenda inayofuata. Katibu!

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Wakala wa Usimamizi wa Maafa wa Mwaka 2014 *(The Disaster Management Bill, 2014)***

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuliahirisha siku ile kupiga kura kuhusu Muswada huu kwa sababu *quorum* ilikuwa haitoshelezi, tulikuwepo wachache. Kwa hiyo, leo tutaupigia kura Muswada huu na nitawahoji.

Naomba sasa nimwite Waziri, ili aje ahitimishe hoja yake.

**Muswada wa Sheria ya Wakala wa Usimamizi wa Maafa wa Mwaka 2014 *(The Disaster Management Bill, 2014)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria Ibara kwa Ibara na imeukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria Mpya ya Menejimenti ya Maafa wa Mwaka 2014 yaani *The Disaster Management Bill, 2014,* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeungwa mkono. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa Muswada huu. Sasa nawatangazia kwamba Muswada huu umeshapita, hongereni sana. Tuendelee, Katibu! *(Makofi)*

***Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi wa Mwaka 2014 (The Tax Administration Bill, 2014)***

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba kusoma Mwongozo wa Spika kuhusu suala lililoombewa Mwongozo na Mheshimiwa *Engineer* Mohammed Habib Mnyaa, Mbunge kuhusu utaratibu utakaotumika kufanya maamuzi kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji ya mwaka 2014 *(The Immigration Amendments Bill, 2014)*.

Katika kikao cha tatu cha Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 19 Machi, 2015 Mheshimiwa Mhandisi Habib Mohammed Mnyaa, Mbunge, alisimama akitumia Kanuni ya 68(7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Aprili, 2013 kuomba Mwongozo juu ya utaratibu utakaotumika katika kufanya uamuzi kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji wa mwaka 2014 *(The Immigration Amendments Bill 2014)*.

Katika kujenga hoja yake, mtoa hoja alitumia Ibara ya 98(1)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inayosomeka kama ifuatavyo:-

Kipengele 98(1)(b) "Bunge laweza kutunga Sheria kwa ajili ya kubadilisha masharti yoyote ya Katiba hii kwa kufuata kanuni zifuatazo: Muswada wa Sheria kwa ajili ya kubadilisha masharti yoyote ya Katiba hii au masharti yote ya Sheria yote yanahusika na jambo lolote kati ya mambo yaliyotajwa katika orodha ya pili kwenye orodha ya pili iliyoko mwishoni mwa Katiba hii utapitishwa tu iwapo utaungwa mkono kwa kura za Wabunge ambao idadi yao hawapungui theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Bara na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Zanzibar."

Ibara hiyo mtoa hoja alitaka Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji wa mwaka 2014 *(The Immigration Amendment Bill, 2014)* uamuliwe kwa msingi wa theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya Wabunge kutoka Tanzania Zanzibar.

Baada ya kupata hoja hiyo, niliunda Kamati ya Wabunge kutoka pande zote mbili za Muungano ambao Wajumbe hao walikuwa Mheshimiwa Jasson Rweikiza - Mwenyekiti na Wajumbe ni Mheshimiwa Andrew Chenge, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Ummi Mwalimu, Mheshimiwa George Masaju - Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Ali Khamis Seif na Mheshimiwa Mhandisi Habib Mohammed Mnyaa.

Aidha, Kamati ilipokutana ili kutekeleza jukumu hili ilifanya majadiliano ya kina na kueleweshana kuhusu tafsiri halisi ya Ibara ya 98(1)(b) ambayo ndiyo msingi wa hoja ya Mheshimiwa Mnyaa. Tafsiri ya Ibara ya 98(1)(a) na (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 Ibara ya 98(1) (a), (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 inaelekeza ifuatavyo; "Ibara ya 98(1) Bunge laweza kutunga Sheria kwa ajili ya kubadilisha masharti yoyote ya Katiba hii kwa kufuata kanuni zifuatazo:-

(a) Muswada wa Sheria kwa ajili ya kubadilisha masharti yoyote ya Katiba hii isipokuwa yale yanayohusika na aya ya (b) ya Ibara hii ndogo; au masharti yoyote ya Sheria yoyote iliyotajwa katika orodha ya kwanza kwenye nyongeza ya pili, utaungwa mkono kwa kura za Wabunge ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya Wabunge wote. *(Makofi)*

(b) Muswada wa Sheria kwa ajili ya kubailisha masharti yoyote katika Katiba hii au masharti yoyote ya Sheria yoyote yanayohusika na jambo lolote kati ya mambo yaliyotajwa katika orodha ya pili kwenye nyongeza ya pili, iliyopo mwishoni mwa Katiba hii, utapitishwa tu iwapo utaungwa mkono kwa kura za Wabunge ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Bara na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Zanzibar.

Kipengele cha pili, kwa madhumuni ya ufafanuzi wa masharti ya Ibara ndogo ya (1) kubadilisha masharti ya Katiba hii au masharti ya Sheria, maana yake ifahamike kuwa ni pamoja na kurekebisha au kusahihisha masharti hayo au kufuta na kuweka masharti mengine badala yake au kusisitiza au kubadilisha matumizi ya masharti hayo." Mwisho wa kunukuu.

Mambo ya Muungano yametamkwa katika Ibara ya (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuorodheshwa katika Nyongeza ya Kwanza ya Katiba hiyo. Miongoni mwa mambo hayo ni Kodi ya Mapato inayolipwa na watu binafsi na mashirika, ushuru wa forodha na ushuru wa bidhaa zinazotengenezwa nchini Tanzania unaosimamiwa na Idara ya Forodha, Uraia, Uhamiaji na kadhalika.

Kwa mujibu wa Ibara ya 98(1)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1997, Miswada ya Sheria ikiwemo ile Sheria iliyotajwa katika Nyongeza ya Pili, orodha ya kwanza, inapitishwa kwa kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote. Miongoni mwa Sheria hizo ni Sheria ya Uraia ya mwaka 1995, Sheria yote; Sheria ya Uhamiaji ya mwaka 1995, Sheria yote; Sheria ya Kuthibitisha Tanganyika kuwa Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1962 kifungu cha 3, 27, 18 na 26; Sheria ya Uhamiaji ya mwaka 1995; Sheria ya Uraia ya mwaka 1995; na Sheria ya Kuthibitisha Mapato ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ya mwaka 1964 zinatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa ujumla wake, lakini bado zinapitishwa kwa utaratibu wa kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote.

Sheria ya Kuthibitishwa Tanganyika kuwa Jamhuri ya mwaka 1962 ambayo baadhi ya vifungu, Ibara zake kwa maudhui yake inagusa Muungano bado inapitishwa kwa kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote. Kutokana na mwongozo huu wa Kikatiba, pale ambapo sheria za kawaida zinazotumika kwa ujumla wake katika pande zote mbili za Muungano au sehemu tu ya Sheria hizo, ndiyo inayotumika katika pande zote za Muungano, sheria hizo zitapitishwa Bungeni kwa kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote.

Mambo ambayo Muswada wa Mabadiliko yake yanahitaji kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Zanzibar, kwa mujibu wa Ibara ya 98(1)(b) yameorodheshwa katika orodha ya pili katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Mambo hayo ni kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwepo kwa Ofisi ya Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, madaraka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kuwepo kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Madaraka ya Serikali ya Zanzibar, Mahakama Kuu ya Zanzibar, Orodha ya Mambo ya Muungano na idadi ya Wabunge kutoka Zanzibar.

Mambo haya kama yalivyo kwa asili yake ni ya Kikatiba kwa kuwa yametajwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, ndiyo maana ya mabadiliko ya mambo hayo, sharti yaungwe mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Zanzibar. Kwa sababu hiyo, kama Muswada husika ungekuwa ni wa kubadilisha masharti ya Orodha ya Mambo ya Muungano kwa kuongeza, kusisitiza au kufuta baadhi ya mambo katika Orodha ya Mambo ya Muungano ili Bunge liupitishe, ingepaswa kuunga mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Zanzibar. *(Makofi)*

Mwongozo wangu kwa maudhui ya Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2014, Muswada wa Sheria ya takwimu 2014, Muswada wa Sheria ya Uhamiaji 2014 haibadilishi Katiba kwa mambo yaliyotajwa katika Nyongeza ya Pili. *(Makofi)*

Orodha ya pili kwa mujibu wa Ibara ya 98(1)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivyo naomba nirudie kusoma kifungu hiki.

Kwa mwongozo wangu ni kuwa maudhui ya Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2014, Muswada wa Sheria ya Takwimu 2014 na Muswada ya Sheria ya Uhamiaji wa mwaka 2014 haibadilishi Katiba kwa mambo yaliyotajwa katika nyongeza ya pili. Orodha ya pili kwa mujibu wa Ibara ya 98(1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivyo Miswada hii itapitishwa kwa kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote kwa mujibu wa Ibara ya 98(1)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo Mwongozo. Katibu!

Waheshimiwa Wabunge, tulikuwa tunashauriana. Muswada uliokuwa unafuata ilibakizwa sehemu ya kupiga kura na kutokana na Mwongozo ni kwamba ni theluthi mbili ya Wabunge wote tunatakiwa tupige kura. Lakini kwa idadi iliyomo humu ndani mpaka sasa hivi tupo Wabunge 162. Kwa hiyo, kengele ipigwe Waheshimiwa Wabunge waweze kuingia, lakini wakati huo huo tuendelee na Muswada mwingine.

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

***Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji wa Mwaka 2014 [The Immigration Amendment Bill 2014]***

**KUHUSU UTARATIBU**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chenge!

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kuomba utaratibu. Mwongozo wa Spika uliousoma umetiririka vizuri sana. Tulipaswa sasa tuingie kwenye hatua ya kupiga kura.

Kwenye hatua hii ya maamuzi hatuwezi kufanya tukiwa kwenye Kamati. Hiyo *two third* tunayoitafuta ni kupitia katika Bunge Zima. Yawezekana shabaha uliyonayo ni kwamba tunataka tupitie kifungu kimoja baada ya kingine, lakini hatuwezi, huko tulishapita. Ndiyo maana nilikuwa nasema nipate Mwongozo wako kwa *point* hii ambayo ni muhimu sana katika mtiririko wa maamuzi ya Bunge lako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chenge Muswada wa Kodi ndiyo uliokuwa unahitaji kupata theluthi mbili ya Wabunge wote na nimetaja idadi ya Wabunge waliopo ndani humu ni 162. Wakati Wabunge wakiingia tuwe tunaendelea na shughuli nyingine, sasa tumeingia Muswada mwingine ambao tuliuachia kwenye hatua ya Bunge Zima. Tuko kwenye Muswada wa Uhamiaji, ule ulikuwa Muswada wa Kodi. Ni Miswada miwili tofauti.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kuhusu utaratibu!

**MWENYEKITI:** Subiri, bado Mheshimiwa Chenge ana hoja.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi na Muswada wa Sheria ya Takwimu, yote hiyo miwili haihitaji theluthi mbili ya Wabunge wote. Hiyo inahitaji ipitishwe kwa wingi tu wa kura za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wa Uhamiaji *(Immigration),* kwa sababu umetajwa katika nyongeza ya pili, orodha ya kwanza, ndiyo unahitaji uamuliwe kwa theluthi mbili ya Wabunge wote. Hiyo ndiyo tafsiri sahihi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano kama ninavyoelewa mimi suala ambalo nimeishi nalo kwa muda mrefu sana na ninajaribu sana kulieleza Bunge hili lielewe utaratibu huu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Kwa maelezo ya Mwongozo niliousoma toka kwa Mheshimiwa Spika ni kwamba zitapigwa kura theluthi mbili ya Wabunge wote.

Hoja ya Mheshimiwa *Engineer* Mnyaa ilikuwa zipigwe kura kwa theluthi mbili ya Wabunge kutoka Tanzania Zanzibar na theluthi mbili ya Wabunge kutoka Tanzania Bara. Lakini kwa Mwongozo wa Spika ni kwamba ni theluthi mbili ya Wabunge wote kwa ujumla wao bila kuangalia theluthi mbili ya upande wowote. Ndiyo Mwongozo niliousoma. *AG!*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo sharti la theluthi mbili ya Wabunge wote tunaopitisha Miswada hii, tutaenda tu kupiga kura kama kuna ulazima, yaani unauliza tu, wanaounga mkono waseme ndiyo! Ndiyo! Sasa kukiwa na ulazima wa kwenda kuhesabu kura, ndiyo tunaenda sasa kuhesabu kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hata juzi Miswada imepita kwa namna ile, ndivyo tumekuwa tukifanya siku zote. Ndivyo ambavyo tunafanya kwa sababu isiyopungua *two third* ndivyo Katiba inavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama kitu hakina ubishi, mnaenda kuhesabiana kwa sababu gani? Kwenda kuhesabiana kura ni pale ambapo kuna *issue* Wabunge wanasema ah ah, hii bwana tupige kura kwa maana kwamba kila mmoja ahesabiwe. Kwa hiyo, huo ndiyo ushauri wangu. *(Makofi)*

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nimesimama kusema jambo la utaratibu ili kuweza kukisaidia Kiti chako.

Katika hatua ya Bunge Zima kabla hatujaelekea kwenye Kamati, Bunge kukaa kama Kamati, ulisema kwamba tunakaa kama Kamati juu ya Muswada wa Sheria ambayo umeitamka. Lakini Bunge hili linaongozwa kwa Orodha ya Shughuli.

Kwa kadri ya Orodha ya Shughuli ya leo, ukurasa wa saba, Miswada ya Sheria ya Serikali. Miswada mitatu ya kwanza yote iliandikwa kupigiwa kura tu, wakati ambapo Muswada wa Sheria ya Takwimu wa mwaka 2013 ndiyo ambao uliandikwa Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa kwa Mara ya Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira ya Orodha hii ya Shughuli, nakishauri Kiti chako turejee kuwa Bunge Zima halafu turudi kukaa kama Kamati kwenye Muswada wa Sheria ya Takwimu kama kuna jambo ambalo tunataka kulishughulikia kwa Kamati ya Bunge Zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala hilo la utaratibu lizingatiwe.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji wa mwaka 2014, ni kweli imeandikwa kwamba kupigiwa kura tu. Imekosewa, *Order Paper* iliyo sahihi inaletwa. Waheshimiwa, tukubaliane kwamba hata sisi huwa tunakosea, hizi ni mashine tu, imekosewa kuandikwa, inaletwa ile ambayo iko sahihi. Kwa hiyo, hii hatua tuliyoenda ndiyo hatua sahihi.

**MWONGOZO**

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiiwa Mwenyekiti, Mwongozo!

Ukweli wa mambo, Muswada wa Sheria ya Marekebisho kuhusu Uhamiaji, tulijadili tulikaa kama Kamati, ukabakia katika *level* ile ya kupiga kura tu. Hapo mimi nilipouliza ilikuwa ni *level* ya kupiga kura tu. Kwa hiyo, hapa haijakosewa kama siku ile ya tarehe ile tulijadili Muswada wote mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada ambao hatujakaa kama Kamati ni wa Takwimu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbukumbu zangu zinani-*serve* kwamba tulipoanza kukaa kwenye Kamati ndiyo Mwongozo ukatoka kabla ya kupitisha vifungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili tutende haki na taratibu zisimamiwe, tunatakiwa tukae kwenye Kamati ya Bunge Zima, halafu tupitishe vifungu, hatukuvipitisha.

**MWENYEKITI:** Tuendelee.

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji wa mwaka 2014**
***[The Immigration Amendment Act, 2014]***

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 4
Ibara ya 5

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8

Ibara ya 9
Ibara ya 10

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 11

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*
*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji**

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe taarifa kwamba baada ya Bunge lako Tukufu kukaa kama Kamati na kupitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji Sura ya 54 ya mwaka 2014 *(The Immigration Amendment Act, 2014)* kifungu kwa kifungu pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Bunge lako lipitishe Muswada huu. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Huo tumeishaupitisha naipongeza Wizara Katibu.

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Takwimu wa Mwaka 2013**
***[The Statistics Bill, 2013]***

Ibara ya 1

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya*

*Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 10

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadliko yoyote)*

Ibara ya 11

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 16

**MHE. JOHN J. MNYIKA (Kny. MHE. EZEKIA D. WENJE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara hii, Mheshimiwa Wenje amependekeza; *by deleting the whole clause and renumber*. Kwa hiyo, anapendekeza kifungu kinachosomeka ifuatavyo kifutwe:-

*"No act done by any officer or employee of the Bureau if done or omitted to be done in good faith in the exercise of performance or purported exercise of performance of his duty or functions as an officer or employee of the Bureau shall subject such an employee or an officer to any action liability or demand of any kind."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tafsiri kifungu hiki kinasema; kutokuwajibishwa, kutokufanya kosa, kifungu cha 16: "Hakuna jambo lolote litakalofanywa na mwajiriwa wa ofisi, ofisi hii ya Takwimu, ikiwa kama atalifanya au kuacha kufanya kwa nia njema katika kutekeleza majukumu au kutekeleza kazi zake kama afisa au mwajiriwa wa ofisi na mwajiriwa huyo hatawajibishwa kwa kosa lolote linalohitaji kufanya hivyo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Wenje amependekeza kwamba kifungu hiki kiondolewe. Utaona kwamba ofisi hii ya Takwimu ina majukumu makubwa sana katika masuala mazima sio tu ya uzalishaji uratibu, usimamizi na usambazi wa taarifa, bali katika masuala

mahsusi, iwe ni kwenye sensa ya watu, iwe ni kushauri Serikali kwenye masuala ya msingi ya kitakwimu ya kuiwezesha Serikali kufanya maamuzi, iwe ni kukusanya taarifa maalum na kutoa takwimu kuhusu taarifa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kifungu hiki kinasema kwamba iwapo makosa yakafanyika, makosa ambayo mengine yanaweza kuwa na madhara makubwa sana, ukitoa takwimu zisizo sahihi, unaweza kusababisha hata migogoro wakati mwingine katika nchi kama ambavyo ilijitokeza wakati wa hoja ya takwimu za *TBC* kuhusiana na idadi ya watu Tanzania kwa uwiano wa kidini na mambo kama haya.

Sasa kwa kazi hii nzito na nyeti, kuna kifungu cha 16 kinachotamka kwamba atakayefanya hayo makosa kwa kinachoitwa nia njema, hatawajibika kuchukuliwa hatua yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vyovyote vile ni vyema kifungu hiki kikafutwa kwa sababu kinaweza kutumika kama kichaka cha uzembe wa kitakwimu wenye madhara makubwa kwa nchi na wananchi.
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Wenje, naomba kutoa hilo pendekezo.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Maelezo ya Mheshimiwa Mnyika yameeleweka na yana mantiki, kimsingi yana mantiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini madhumuni makuu ya kifungu hiki sijui kwa nini ana-*relate* na matokeo ambayo yalitolewa na *TBC!* Madhumuni makuu ya kifungu hiki ni kuwalinda wafanyakazi wa Ofisi ya Takwimu ambao wamepewa *training* ya kutosha, ambao wanalindwa na misingi ya kiuadilifu, ambao tunawasimamia kwa dhati kabisa, kukiwa kumetokea kosa lolote kwenye masuala ya takwimu ambayo baada ya kufanya uchunguzi tukaona makosa yaliyotolewa yamefanywa katika *good faith*, kifungu hiki ni kwa ajili y wale *staff,* ofisa wa *Bureau, not any other officer,* ofisa wa *Bureau*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika *performance* ya *duty* zake*,* wakati anaendesha kazi zake, tuna misingi ya kuendesha kazi hii, ndiyo tunaposema kwamba kama tutabaini kwamba yale makosa ameyafanya kwa *good faith* katika ku-*exercise duty* yake, basi tunaweza tukam-*exempt* kwenye *liability* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hiyo haitokei hivi hivi, tutafanya uchunguzi, tutaandaa taratibu zote na kama tunahakikisha kwamba kweli aliyoyafanya yalikuwa tu katika mlolongo mzima wa utendaji wa kazi yake, basi hiki kifungu kitakuwa kinamlinda. Siyo kila mtu na wala huwezi ku-*relate* na makosa ambayo yamefanywa na vyombo ambavyo kisheria havipaswi kutoa takwimu zisizo rasmi. Taasisi pekee yenye kutoa takwimu, kuchambua na kuelezea ni *National Bureau of Statistics* ambayo sheria yake ndiyo tunataka kui-*adopt*. Ahsante.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilijua kabisa *TBC* siyo Tanzania *Bureau of Statistics,* wala haihusikani na hilo, nilijua hivyo. Na kama ungenisikiliza vizuri Mheshimiwa Waziri, nilisema hivi, madhara ya kutoa takwimu zisizo sahihi yanaathari kubwa kwa nchi na kwa wananchi; na nikatolea mfano wa *TBC*. Sasa fikiri chombo cha takwimu na chenyewe afisa wake akatoa takwimu zisizo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ningemuelewa Mheshimiwa Waziri na ningesema hili pendekezo tunaliondoa kama tu angesema yuko tayari kufanya mambo mawili muhimu sana ili kuepusha kulinda uzembe na udhaifu wa kitakwimu.

Moja, Sheria hii ya Takwimu, ingekuwa na vifungu vinavyoweka utaratibu pale ambapo takwimu zimetolewa kimakosa na hao maafisa wa chombo cha takwimu, *procedure* za kiuchunguzi zikoje, mfumo wa wananchi kulalamikia hizo takwimu na hatua ili hiyo nia njema iweze kupimwa kiuhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii haina huo mfumo kamili wa utaratibu wa malalamiko na ushughulikiaji wa mashauri bali amezungumza Waziri hapa kwa mdomo, ndani ya sheria hakuna mchakato mzima wa utaratibu wa namna hiyo. Kwa hiyo, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ambalo lingepaswa kufanyika, hicho ambacho kinaitwa *good faith* (nia njema), kingeelezwa nia njema maana yake ni nini ili usije uzembe au udhaifu mwingine au nia ya makusudi kabisa ya kutoa takwimu potofu ikafichwa kwa kivuli cha nia njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipitia kwenye sheria hii, kifungu cha 3 cha sheria kinachohusu tafsiri ya maneno ambapo kuna tafsiri ukurusa wa 28, ukurasa wa 29, ukurasa wa 30, hakuna mahali popote ambapo nia njema *(good faith)* imetafsiriwa. Katika mazingira kama haya, ukipitisha kifungu hiki kikakaa kama kilivyo bila kurekebishwa kuwekewa misingi mingine, ni wazi watu watatoa takwimu potofu na hawatawajibishwa kwa kivuli cha kujifunika kwa nia njema. Kwa hiyo, bado naona umuhimu wa uwepo wa kufutwa kwa kifungu hiki ili kuisaidia nchi.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua wasiwasi wa ndugu yangu Mheshimiwa Mnyika, lakini labda amesahau tu kwamba hizi sheria ndivyo zinavyoandikwa. Hata kwenye Bunge hili tumeshapitisha sheria nyingi, kwenye Mkutano huu tu wa aina hii. Na hapa si kwamba huyu ofisa hatawajibika kwenda Mahakamani, ataenda tu Mahakamani, ila katika kutamka ama aadhibiwe kwamba ana hatia au hana hatia, Mahakama itapima ile kwamba hiki kitu kilifanyika kwa nia njema. Ukiangalia, Mheshimiwa Mnyika, angalia pale mwishoni *liability*, hakuna anayeweza kutangaza hiyo *liability*, isipokuwa ni Mahakama yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kushauri kwamba Ibara hii kama ilivyoletwa na Serikali ibakie jinsi ilivyo. Na wasiwasi wa Mheshimiwa Mnyika, kuna kanuni. Ukisoma Ibara ya 38 pale inataja Waziri atatunga kanuni hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi tu Waheshimiwa Wabunge tukawa na sheria ambayo kwa aina yake Serikali ikatunga sheria ambayo hakuna mtu anayeweza kuwajibika, na sisi wote tunajua kwamba hakuna mtu ambaye yuko juu ya sheria, hakuna mtu ambaye yuko juu ya sheria, wote tunawajibika pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Ibara ya 107 ya Katiba ya Jamhuri inasema yenyewe ndiyo yenye kauli ya mwisho ya Mahakama. Kwa hiyo, huyo atapimwa kwa vitendo vyake. Kwanza, anawajibishwa, hata akifanya mambo ya hovyo, uongozi wenyewe unamwajibisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama inaendelea hivi, inaenda Mahakamani na ndiyo maana Mwanasheria Mkuu wa Serikali anawajibika kuunganishwa kwenye mashauri haya pale ambapo taasisi za umma zimefanya kazi, ili akionekana kwamba wewe bwana ulifanya hivi, awajibishwe. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kumshauri Mheshimiwa Mnyika akubaliane na mapendekezo ya Serikali kama ilivyo kwenye Ibara hii kifungu kiendelee.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, pamoja na maelezo hayo ya kina…

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo haya yananipa sababu ya ziada ya kufuta hiki kifungu ili pengine Serikali ije na mapendekezo mengine kwenye marekebisho mbele ya safari yatakayoweka msingi mzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru maelezo haya yametolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mwanasheria Mkuu wa Serikali nakubaliana na wewe ni kweli sheria nyingi tunazozitunga hapa Bungeni, tunapounda vyombo mbalimbali na hata juzi tumetunga Sheria ya Kudhibiti Dawa za Kulevya, tukaweka kifungu kama hiki cha kinga kwa watumishi, Kamishna na wengine wanapofanya kazi zao, umekuwa ni utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sio utamaduni mzuri wa kuweka kinga isiyokuwa na mipaka na mchakato wa ushughulikiaji pale ambapo kinga hiyo inatumika vibaya. Kwanza, tafsri ya nia njema, lakini pili, mchakato wa malalamiko pale kwenye nia mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano halisi, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali wewe unafahamu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliyekutangulia alitoa ushauri kwamba fedha za *Escrow* zisitozwe kodi, alipoulizwa akasema ni kwa nia njema, lakini upepo ulipotibuka kweli kweli, akasema anajiuzulu kwa sababu tu amechafua hali ya kisiasa, siyo kwa sababu alitoa ushauri wenye nia mbaya, na mpaka sasa hivi tunavyozungumza Mwanasheria Mkuu yule wa Serikali hayuko Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira kama haya ni kipi kitufanye tuamini kwamba tuweke vifungu tu vya kulinda kulinda kulinda kulinda makosa ambayo watu wanatakiwa kuwajibika kwa uzembe, kwa kivuli tu cha kwamba sheria zinataka ziwape uhuru wanayoyafanya kwa nia njema.

Kama hatutatoa tafsiri ya nia njema ni nini, na kama hatutaweka utaratibu wa kushughulikia malalamiko pale ambapo wananchi wana mashaka kwamba hili halikufanyika kwa nia njema, kama hatuweki utaratibu huo kwenye sheria, hakuna sababu ya kuwa na kifungu hiki kwenye masuala ya takwimu. Tujenge utamaduni mpya kuanzia leo wa kuweka vifungu ambavyo vitasaidia uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashikilia kwamba kifungu hiki kifutwe.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo yametosheleza na kifungu hiki tunakiomba kwamba kiende kama kilivyokuwa kimeandikwa. Kwa sababu bado kuna nafasi, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameleeza tuna nafasi ya kutunga kanuni na kanuni tutazitunga kuelezea mlolongo mzima ni nia safi.

Lakini hata hivyo tayari tuna *code of conducts* kwa watakwimu wote, zinaeleza jinsi gani ya kutekeleza kazi kwa upande wa takwimu, kila kitu kimeelezwa pale. Kwa hiyo, mimi sioni sababu kwa nini Mheshimiwa Mnyika anashikilia hili wakati kuna taratibu nzima zimeelezewa na zitaelezewa kwenye kanuni, zipo katika *code of conducts* na bado uchunguzi wa jambo utakuwa unaendelea kimahakama kama alivyosema Mwanasheria Mkuu.

Kwa hiyo, tunaomba hiki kifungu kiendelee kubaki kama kilivyo na Serikali itakuwa inatimiza wajibu wake kuona kwamba inawachukulia hatua wale wote wakibainika kwamba wanakwenda kinyume na taratibu zote za kazi zao ambazo wanapaswa kuzifanya. Naomba hiki kifungu kibaki kama kilivyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, kwa maelezo hayo unakubaliana?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni zinatungwa na Waziri, hazitungwi na Bunge, hatuwezi kuwa na uhakika kwamba haya yatawekwa. Angeahidi kwamba mambo haya yatakuja kuwekwa kwenye sheria huko mbele, pengine tutafanya marekebisho, ningemuelewa, lakini, Kanuni!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatunga sheria hivi sasa masharti hayo tungeweka kwenye sheria. Kwa hiyo, tupige kura tu ibaki kwenye *record* kwamba tunaendeleza mambo yale yale. Tungefungua ukurasa mpya kuanzia sasa kufanya mabadiliko taratibu taratibu ya kimfumo kwenye mifumo yetu, lakini inaelekea Mheshimiwa Waziri angependa tuendeleze mambo yale yale siku zote.

**MWENYEKITI:** Hatupigi kura kwa kuendeleza yale yale, tunapiga kura kwa kukubaliana. Sasa naomba tupige kura.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 21

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 22

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.
Katika kifungu hiki cha 22, Mheshimiwa Wenje amependekeza katika kifungu kidogo cha pili ambacho kinasomeka "*the Bureau may cause the statistics collected and any official statistical information made available to be published.*"

Sasa Mheshimiwa Wenje amependekeza, nitasoma jedwali lake, *"in clause 22(2) by deleting the word "may" appears between the word "Bureau and cause" and substitutes with the word "shall".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tafsiri rahisi kifungu hiki ni cha kuhusu ukusanyaji wa takwimu. 22(1) inasema ofisi inaweza kukusanya takwimu zinazohusiana na jambo lolote au mambo yoyote yaliyoainishwa katika jedwali la tatu la sheria hii. Pili, ofisi inaweza kuelekeza kwamba takwimu zilizokusanywa na taarifa nyingine yoyote rasmi ya kitakwimu ichapishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Wenje anapendekeza, badala ya inaweza, kwamba inaweza, ikisema inaweza, inaweza vilevile isiweze yaani isifanye. Kwa umuhimu wa

takwimu zilizotajwa katika orodha ya jedwali lililoainishwa, Mheshimiwa Wenje na mimi binafsi naunga mkono, tunadhani kwamba takwimu hizi ni muhimu kweli zichapwe, hivyo chombo hiki kilazimishwe kwa kuweka neno "*shall*" kuhakikisha kwamba takwimu hizi zinachapwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Kifungu ambacho anazungumzia Mheshimiwa Mnyika kwa niaba ya Mheshimiwa Wenje ndiyo kinavyozungumza kwamba, "*the Bureau* maana ya *National Bureau of Statistics may cause* na *the statistic collected,* yaani hizo takwimu zilizokusanywa, *and any official statistical information made available to be published*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tunaona hicho kifungu kimekaa sawa. Kwa nini tuilazimishe taasisi ambayo kisheria ndiyo yenye mamlaka ya kukusanya, ku-*analyse*, ku-*publish,* vilevile ndiyo yenye mamlaka ya kutoa ruhusa kwa wengine kwa kufuata taratibu za kukusanya na kutoa takwimu kwamba lazima zitangazwe, hapana. Itakapoona inafaa kwamba ni takwimu muhimu kutangazwa itaruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa haina sababu kama *procedure* zote za hiyo taasisi ama mtu zimefuatwa na yeye atakuwa hana sababu ya msingi sana ku-*publish,* atamruhusu a-*publish*. Lakini ukimuwekea "*shall*" kwamba kila takwimu inayokuswanywa, kila *official statistics* inayokusanywa ndiyo itangazwe, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiachie chombo hiki ambacho kimsingi ndicho chenye usimamizi wa takwimu, basi kifanye maamuzi yake. Kama itakapoona takwimu hizi hazina madhara yoyote kwa jamii kwa kuwa imefuata misingi yote ya ukusanyaji wa takwimu pamoja na kui-*interpret* haitakuwa na sababu ya yeye kumzuia. Lakini "*shall*" maana yake moja kwa moja lazima hizo takwimu zitangazwe, hilo haliwezekani. Hii nchi inakwenda kwa misingi ya sheria na vyombo ambavyo vimeaminiwa kwa mujibu wa sheria zinazotungwa zitafanya kazi yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kifungu kibaki kama kilivyo.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hakizungumzii takwimu zinazokusanywa na watakwimu wengine ambao wamepewa ruhusa na chombo kinachohusika kukusanya takwimu. Kifungu kinazungumzia takwimu zilizokusanywa na chombo chenyewe cha kukusanya takwimu.

Jedwali la tatu ukiangalia *nature* ya takwimu zenyewe zilizotajwa kwenye orodha hakuna zenye *nature* ya siri za Serikali, ni Sensa ya Watu na Makazi, Usajili wa Vifo, Vizazi na matukio ya jamii, uhamiaji, biashara nje, urali wa biashara na utalii, taarifa za kiuchumi, kilimo, ujenzi, viwanda, madini, bidhaa, soko la ajira, fedha za Serikali, umaskini na mgawanyo wa mapato, masuala ya jamii, benki, biashara za kitaalam, elimu na afya, madhara na fidia, umiliki wa ardhi, mambo yote haya ni muhimu kwa wananchi, mazingira, biashara, habari, jinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, orodha ni ndefu ya mambo ya kawaida ambayo takwimu zake ni muhimu kwa nchi na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali hii imekubaliana na Mpango wa Serikali Wazi *(Open Government Partnership)* na mnayaambia mataifa mengine kwamba Tanzania iko tayari kuwa wazi, Serikali kuwa wazi na mnaleta kwa Hati ya Dharura, Muswada wa Dharura wa Haki

ya Taarifa, halafu kwenye kuvipa wajibu vyombo kutoa taarifa, kutoa takwimu, mnaweka zuio kwa takwimu ambazo siyo siri za Usalama wa Taifa wa siyo siri za Kijeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi bado nasisitiza kama tumetumia gharama kubwa ya wananchi kukusanya takwimu, tusizifiche hizo takwimu makabatini zikashindwa kutuongoza kwenye maamuzi. Kwa hiyo, kifungu hiki bado kilazimishe takwimu hizo kutolewa.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo tunalobishania, mimi nadhani ni lugha tu, lakini uhalisia wake ni ule ule. Tunapoweka *flexibility* kwamba mamlaka inayokusanya hizo takwimu ipate fursa ya kupima na kutoa hizo takwimu, tunazingatia pia mazingira ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, takwimu zinaweza zikakusanywa lakini *standard* ya kutoa hizo takwimu zinatakiwa zitolewe *quarterly,* hatuwezi tukasema zote ambazo wameshazikusanya zinatakiwa zitoke muda uleule. Kwa hiyo, tunawawekea mazingira yale ya *flexibility* ambayo itawaruhusu wakusanye na watakapokuwa wamejua zimeishaiva waweze kuzitoa.

Vilevile kuna takwimu zingine ambazo kwa kusudi lililokusudiwa kukusanywa sio za muhimu kutoka. Tusiwalazimishe kwamba zote ambazo walishazikusanya lazima zitoke. Zingine zinaweza zikatumika kama *raw data* kwa ajili ya kukamilisha kile kilichokuwa kimekusudiwa katika takwimu. Kwa hiyo, tusiwatake zote walizokusanya na zenyewe lazima zitoke. Hata unapofanya *study,* una *present* kile ambacho kimekusudiwa kwenye *study* yako, sio una-*present* kila ulichokusaya, vingine vinakuwa *for personal use* ili uweze kupata takwimu ambayo ulikuwa umekusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la lugha lisitusumbue sana, lakini ile *intended purpose,* takwimu ambazo zinakusudiwa kwa ajili ya jamii kama ilivyo tayari zitawafikia jamii kwa sababu ya uzito wake. Kwa hiyo, naomba Bunge pamoja na Mheshimiwa aliyeleta hii hoja, aridhie kwamba hapa ni lugha tu, lakini kile kilichokusudiwa kwa ajili ya wananchi kitawafikia, tuiachie mamlaka kutoa kile ambacho ni kwa ajili ya wananchi, lakini kile ambacho ni kwa ajili ya kuandaa zile takwimu isiwe lazima kwamba chote kilichokusanywa lazima kitolewe.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Nimesikiliza hoja ya Mheshimiwa Mnyika, lakini nimesikiliza majibu ya Serikali. Kuna mambo mengine kama viongozi lazima tuwe wawazi, tunakubaliana kote, lakini siyo uwazi wa namna hiyo ambao Mheshimiwa Mnyika yeye anausema. Haiwezekani kila kitu kikatangazwa.

Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri kwamba tuwape nafasi, kuna mambo ya msingi ambayo kama mengine ambayo ameyasema ya takwimu, kama sensa ya makazi, mbona hayo yanatangazwa. Lakini lazima hiki chombo tusikifunge, haiwezekani, kuna mambo mengine ya ardhi, kuna mambo ya nini, kila takataka useme unaenda kutangaza kwenye Gazeti la Serikali na vilevile hivi vitu pia vinatumia pesa. Kwa hiyo, hatuwezi tukatumia pesa kwa kutangaza kitu ambacho hakina ulazima wa kutangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vya msingi Serikali ambavyo inaona kama *issue* ambayo Mheshimiwa Mnyika amesema sensa na makazi tunatangaza. Hata huko duniani sio kila kitu ambacho wanatangaza, wanapima uzito kipi tutangaze na kipi tusitangaze. Hatuwezi tukatumia mwanya wa uwazi vibaya kwa kuhalalisha kitu ambacho kama Taifa, kama chombo ambacho kimepewa mamlaka wana uwezo wa kupima.

Mheshimiwa Mnyika, nakuomba wewe kiongozi, Naibu Katibu Mkuu kwenye chama chako hutangazi kila kitu, kuna mambo ambayo unapima watu wayajue na mengine unapima watu wasiyajue, ndiyo Serikali inavyoendeshwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Bulaya. Ahsante. Haya Mheshimiwa Mnyika!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ambayo yanapimwa yasitangazwe huwa yanaingizwa kwenye Sheria ya *Classified Information*. Mambo ambayo hayajaingizwa kwenye Sheria ya *Classified Information* huwezi kupima kuyatangaza au kutoyatangaza na kuweka ukomo. Hata katika chama cha siasa chochote nyaraka za siri za chama zitakuwa siri, lakini masuala mengine yoyote ambayo hayapo katika *category* ya siri za kimkakati ambazo ukizitoa wapinzani wako wanaweza kuzitumia, huwezi kuyafanya kuwa siri, utayaweka kuwa wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachokisema ni nini hapa? Tunaweza kuchukulia jambo rahisi tu kwamba ni kaneno "*may and shall*", lakini *in actual sense* hako kaneno kadogo tu kamoja kana uzito. Hii *discretion* itaendelea kutumika vibaya kuficha taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeielewa Serikali kama ingesema tuko tayari kuweka *category* kwamba aina hii baada ya kupata takwimu, tukipata takwimu ambazo tunaona kwamba *for national interest* hatuna sababu ya kuzi-*publish, category* hiyo ya takwimu hazitolewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuweka tu kwa ujumla kwamba *you may choose to publish or not to publish,* kwa kweli *unless* mtuambie Mpango wa Serikali Wazi hamna dhamira wa kuutekeleza, *unless* mtuambie kwamba Muswada mnaotaka kuuleta wa Uhuru wa Taarifa una lengo la kuficha taarifa na sio kuachia taarifa wazi, kama tayari kwenye takwimu tu mmeshaanza utamaduni wa kuficha taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupige kura tupate *record* ya wangapi wanataka kuendelea kuficha taarifa waitikie tu ndiyo.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona Mheshimiwa Mnyika anachanganya mambo mengi sana bila ya sababu wala msingi. Serikali tuna *Implement Open Government Initiative* na tuko *very proud* katika kui-*implement* hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki, kwanza hii sheria tukisha kuipitisha, kuna *resources* nyingi hapa zitahitajika. Lakini kitu kimoja tu, sio kama tukisema kwamba *Bureau* inaweza ama yaani katika *discretion* yake, sawa, lakini lazima taasisi yoyote ni lazima iwe *flexible* kulingana na hali ya mazingira ilivyo. Leo hii tukishakuweka hapa *the Bureau shall cause the statistics to be published* na nini…

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu tunavyoiendesha inahitaji gharama, inahitaji watu na vitu vingine kama hivyo. Haina sababu *NBS* kuficha taarifa yoyote, na *NBS* ni chombo ambacho kimekuwa kikifanya kazi vizuri sana, imekuwa ni taasisi ambayo iko *very reliable worldwide* (duniani kote). Siku tutakapokuwa hatuna *resources,* hatutaweza ku-*publish*. Lakini tukisema tukiweka "*may*" wala haimzuii kama pale tunapoona kwamba hii taarifa ni kwa manufaa ya umma itoe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja ambalo tunalitekeleza vizuri, kila mwezi tunatoa taarifa juu ya hali ya *inflation*, inatoka kila mwezi tarehe iliyokubalika *internationally,* tunatoa. Kwa hiyo, wala hiki siyo kifungu ambacho tunasema kwamba tuna nia ya kuficha taarifa, taarifa

zitatolewa lakini bado tuipe taasisi hii *flexibility* kwa sababu inaendana na hali ya *resources* yenyewe ilivyo. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 23

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 24

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika kifungu hiki ambacho ni kifungu cha 24(3), Mheshimiwa Wenje ana mapendekezo ambayo naomba niyasome, kifungu hiki kinahusu *sampling*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, 24(3) inasema "*it shall not be a defense to a person who fails to fill in return or to answer any enquiry by reason that only a portion or a particular group of persons is require to fill the return or to answer the enquiry.*" Kwa tafsiri ya Kiswahili, utaratibu wa sampuli, kifungu cha 24(3); "haitakuwa utetezi kwa mtu yeyote atakayeshindwa kujaza dodoso au kujibu maswali yoyote kwa sababu sehemu tu au kundi fulani la watu linatakiwa kujaza au dodoso au kujibu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Wenje anapendekeza kwamba kifungu hicho kifutwe kwa sababu kimsingi ukikisoma hiki kifungu na kwa sababu Serikali imesema ni utaratibu wa sampuli sio jambo la lazima kwa kila mtu, ni *sample*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama unafanya sampuli, halafu unalazimisha sampuli na unatoa adhabu pale ambapo una mashaka kwamba pengine sampuli yako unayoitaka haitafikiwa kwa sababu ambazo unazitaka wewe au zilizopo, basi watu wakikataa kushiriki kwenye dodoso ya hizo sampuli wanaadhibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa hakikisho la Serikali kabla sijakubali kwa niaba ya Mheshimiwa Wenje kwamba kifungu hiki kiondolewe, ni kwa vipi kifungu hiki kinaendana kikamilifu na matakwa ya Ibara ya 18(a) ya Katiba ya nchi, ambapo kila mtu anao uhuru wa kutoa maoni na kueleza fikra zake, ana uhuru wa kupokea, kupewa taarifa na uhuru mbalimbali wa maoni.

Kwa hiyo, ningependa kupata ufafanuzi wa Serikali kwamba kama kifungu hiki kinaheshimu matakwa hayo na wakitoa ufafanuzi wa kuridhisha, nitakuwa tayari kifungu hiki kiondolewe, lakini bila hivyo, ni afadhali kifungu kifutwe ili kuondoa utata wa watu kuadhibiwa kwa makosa ambayo sio lazima kushiriki kuyatolea majibu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari ilishaleta mabadiliko kwenye kifungu hiki kwa jedwali ambalo limewasilishwa tayari kwenye Bunge lako Tukufu na sasa badala ya neno *sampling* itakuwa ni takwimu *(statistics)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwa sababu ni siku nyingi zimepita, kwa hiyo, ukiangalia kwenye jedwali utaiona hii, kwa hiyo, hiyo hoja sasa inakuwa haina maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ambacho naomba kulishauri Bunge hili ni kwamba kila haki ina wajibu, yaani kama hiyo tunajaribu ku-*reconcile* ile Ibara ya 18 ile, sehemu ya Katiba hii inayoeleza juu ya haki, inaeleza pia na wajibu wa wananchi. Kwa hiyo, hapa wajibu wake ni atoe taarifa hizi ili takwimu hizi zipatikane. Akikataa kuzitoa hizi takwimu anawajibika. Kwa hiyo, hakuna haki ambayo *in itself so much absolute,* ni lazima haki inaenda wajibu na kwenye Katiba yetu hii sehemu hii inasema haki na wajibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya Mheshimiwa Mnyika kuwa ameiona ile, anaridhika na sisi. Naomba tushauri kwamba tubaki na hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, kwa maelezo hayo unaridhika?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naridhika, tu kwa minajili ya kutoonekana mbishi kwa sababu tu…

**MWENYEKITI:** Ahaah! Ridhika tu vizuri sio kuonekana mbishi.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Muswada umetolewa siku nyingi sana, siku nyingi zimepita, hapa hatuna hayo majedwali ya Serikali. Kwa hiyo, maana yake ili kutouziwa mbuzi kwenye gunia, niseme tu sijaliona jedwali la Serikali, lakini kama ni lazima hizo takwimu kwa kila mwananchi kujaza ni wajibu hilo ni suala lingine.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 25

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 26
Ibara ya 27

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34
Ibara ya 35

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 36

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 37

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru katika Ibara ya 37 inayohusu makosa na adhabu kwa mtu yeyote, na imeainishwa na mtu ni pamoja na vyombo kwa tafsiri ya kisheria. Sasa kuna vipengele vitatu ambavyo Mheshimiwa Wenje amependekeza kwamba vifutwe.

Cha kwanza, kinasema chombo chochote cha habari ambacho kinachapisha taarifa za kitakwimu za uongo au za upotoshaji au kinatangaza kipindi chochote kinachohusu shughuli za ukusanyaji wa taarifa ambayo imefanywa au inafanywa na ofisi na hatimaye kusababisha wananchi wasishiriki kwa shughuli hiyo ya ukusanyaji wa taarifa au wasishirikiane na maafisa wa ofisi kinatenda kosa na kitakapotiwa hatiani kitawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni 10 au kifungo cha muda usipungua miezi kumi na mbili au vyote viwili.

Kipengele cha tano, kinasema mtu yeyote au wakala ambaye bila idhini ya kisheria kutoka kwa ofisi anachapisha au anasambaza taarifa za kitakwimu ambazo zinaweza kusababisha upotoshwaji wa taarifa husika anatenda kosa na akipatikana na hatia atatakiwa kulipa faini isiyopungua shilingi milioni 10 au kifungo cha muda usiopungua miezi 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaendelea kipengele cha sita, kwa madhumuni ya chombo hiki, chombo cha habari kinajumuisha kituo cha redio, kituo cha televisheni, gazeti au jarida, tovuti au chombo kingine chochote kinachotoa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipengele hivi vya 4, 5, 6, kwenye kifungu namba 37, havina tofauti na vifungu vya kisheria ambavyo Tume ya Nyalali huko nyuma kwa sheria nyingine za nyuma, iwe ni Sheria ya Magazeti, iwe ni Sheria ya Usalama wa Taifa…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, naomba tuelewane hapo, Serikali kwenye marekebisho ya jedwali imekubaliana kufuta kifungu cha 4 na cha 5, kilichobaki ni 6, 4 inawekwa upya.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kifungu cha sita kina-*hang?*

**MWENYEKITI:** *Yeah,* sasa nilikuwa napenda kwenye hivi ujielekeze vile ambavyo…

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tu ya kuruhusu shughuli hizi kuendelea, jambo hili, sheria hii ilikuwa ni ya muda mrefu sana na ingepita muda mrefu sana. Ili kuweza kukubali hicho, nitahitaji nilisome jedwali la Serikali ambalo nimeletewa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ama sivyo kama wengine mnataka kupitisha tu kwa sababu ya kupitisha tu, pigeni kura ya ndiyo kupitisha kwa sababu ya kupitisha, halafu wananchi huko mbele ya safari watakuja kuamua kwamba hamjafikia hatua ya kutunga Sheria ya Uhuru wa Habari, Uhuru wa Taarifa kwa wananchi, lakini mbele zinatangulia sheria nyingine ambazo bado zina mazonge mazonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili nisiuziwe mbuzi kwenye gunia, nitaomba nikae kwanza, nisome jedwali la Serikali ambalo nimeletewa sasa hivi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, jedwali hilo la marekebisho ya Serikali tulishapewa, kwa hiyo, ulitakiwa uwe umeshalisoma, ndiyo uje utoe marekebisho yako.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikuambie mambo mawili tu.

La kwanza, Wabunge kutambua kwamba leo kwenye Orodha ya Shughuli za leo kuna hii Miswada hii, unatambua unapoingia Bungeni kwenye Orodha ya Shughuli. Kwa hiyo, maana yake ni nini, Kanuni za Bunge, ilipaswa mimi niache kipindi cha maswali niende nikatafute hivi sheria iliyobaki kiporo kwa sababu haikukamilika wakati huo, muda mrefu kweli miezi mingi jedwali la Serikali liko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka hii hoja na huku siyo kutendeana haki, Mheshimiwa Wenje amepata dharura kwa sababu nakuwa *caught by surprise,* unafika hapa unaambiwa kuna jedwali la Wenje, *caught by surprise!* Kwa hiyo, katika mazingira kama haya ndiyo maana nikasema, ili nisionekane…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie…

**MWENYEKITI:** Muda umeishaisha. Mheshimiwa Mnyika, naomba nikueleze hivi…

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** *Okay*, kwa sababu muda umeisha, wanaoipiga kura wanataka kupitisha wapige kura tu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, naomba ukae. Naomba nikueleze hivi, mabadiliko ya ratiba hii, Kikao cha Kamati ya Uongozi kilifanyika siku ya Jumapili na mwakilishi wa Kambi ya Upinzani alikuwepo! Ndiyo!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mtasema…

**MWENYEKITI:** Naomba tupige kura…

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mtasema kaa chini, lakini ipo siku wananchi huko mtaani watawaambia kaeni chini. Huku ndani semeni tu kaeni chini…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, naomba ukae! Mheshimiwa Mnyika, heshimu Kiti!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naheshimu Kiti chako. Waambie hao wanaozomea na wenyewe waheshimu Kiti chako, waache kuzomea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, naomba ukae!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, waambie wanaozomea waache kuzomea.

**MWENYEKITI:** Nakuomba ukae! Nakuomba ukae! Mimi sijakupa ruhusa ya kuongea. Heshimu Kiti, naomba ukae! Mheshimiwa Mnyika, kaa!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitakaa, lakini naomba Kiti kiwaambie watu wasizomee.

**MWENYEKITI:** Kaa Mheshimiwa Mnyika! Naomba ukae! Mimi nakuheshimu, hebu kaa, heshimu hiki Kiti!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Lakini naomba uwaambie hao waache kuzomea.

**MWENYEKITI:** Nasema kaa! Mwanasheria Mkuu wa Serikali!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Mheshimiwa Mnyika amesema, lakini ukweli ni kwamba wasiwasi ambao ameuonesha, Serikali imeshaufanyia kazi kupitia hili jedwali ambalo tuliwasilisha mbele ya Bunge hili tukufu kwenye Bunge la mwezi Novemba mwaka jana. Atakapoisoma hii, naamini atakubaliana tu na mapendekezo haya yaliyoletwa na Serikali. Kwa hiyo, naomba tuendelee na Ibara hii kwa kuzingatia marekebisho haya yaliyoletwa na Serikali.

**MWENYEKITI:** Sasa nitawahoji…

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeyasoma marekebisho ya Serikali, mimi ndiyo nimetoa hoja, naomba kuhitmisha…

**MWENYEKITI:** Sijakuita Mheshimiwa Mnyika, mimi sijakuita. Kwa hiyo, sasa jieleze!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba niyasome marekebisho yaliyoletwa na Serikali, namba 4 inasema:-

"*A Director/Manager, Controller or any other person who is concerned with management of any communication media allow or cause to be published false official statistical information or broadcasts any program about data collection activity that have been undertaken or is being undertaken by the Bureau and as a result of each causes any person or persons to abstain from participating in the data collection activity or cooperating with officers of the Bureau commits an offense and shall be liable to a conviction to a fine of not less than 10 million shillings or imprisonment for a term of not less than three years of both.* Kwa yeyote anayeelewa hiyo lugha, atajua kwamba mzigo wa adhabu, mzigo wa makosa mwelekeo ni ule ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba 5, *an agency or a person who publish or communicate official statistical information which may result in destruction of facts commit an offense and shall be liable on conviction to a fine not less than ten million shillings or to imprisonment for a term not less than three years or both.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unaweka misingi hii kwenye Sheria ya Takwimu, bado hujatunga Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari, hujatunga Sheria ya Uhuru wa Taarifa, wananchi, wadau wa habari, wana malalamiko. Katika mazingira kama haya, Sheria ya Takwimu ina vifungu na vifungo namna hii, wadau tutakubaliana kwamba hamuwezi kuruhusiwa mkaleta hata Muswada wa Huduma za Habari kwa Hati ya Dharura; na Muswada wa Uhuru wa Taarifa kwa Hati ya Dharura. Kwa sababu kama kwenye takwimu iko namna hii. Itakuwaje huko mbele. Kwa hiyo, kama mnataka kupitisha, pitisheni tu. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri. Tunapotunga sheria tuwe *balanced*. Muda mfupi uliopita alikuwa ana-*crusade* dhidi ya wafanyakazi/watumishi wa *Bureau* waweze kuwajibika kisheria. Nikampelekea kifungu cha 37 cha sheria hii moja inavyoonesha jinsi ambavyo watumishi wa *Bureau* wanavyowajibika pia

kushitakiwa Mahakamani kwa makosa wanayofanya. Sasa inapofika watu hawa wanaohusika nao na makosa wafanye, hataki wawajibishwe kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba tuiache hii sheria ifuate mkondo, kwa sababu kila haki, kila mtu anayetekeleza wajibu wake, ana wajibu wa kuwajibika. Ndicho ambacho naomba kushauri Waheshimiwa Wabunge kwamba kila anayetekeleza majukumu yake, masuala na jinsi yalivyokuwa kwenye Muswada wa Serikali ilikuwa ni kampuni nzima, lakini sasa katika mabadiliko baada ya Serikali kusikiliza hoja za Wabunge, ikaleta mabadiliko ikasema sasa ni *individual person*, mwajiriwa wa ile kampuni. Na sisi wote tunajua kuna *abuse,* watu wanaandika habari hovyo hovyo hapa; na masuala ya *information* yanaweza yakasabisha hata Taifa likaenda kwenye uharibifu, na tuliona yaliyotokea hata Rwanda na ni kwa sababu ya *information*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi habari za *Open Government Partnership* haiendi *to the extent* kwamba sasa kila kitu kinakuwa ruhusa; na yeye mwenyewe amesema kwamba hata kwenye chama yapo mambo ambayo ni *classified* ambayo hayawezi kwenda nje ya nanii.

Kwa hiyo, ni lazima kuwe na *accountability*, yaani mimi nawezaku-*claim* haki yangu, lakini na mimi nawajibika nje ya haki nyingine aidha ya jamii au ya *individual*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiisoma Ibara ya 30 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, muda hatuna, lakini Mheshimiwa na Wabunge wengine waende wasome Ibara ya 30 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mabadiliko ya Serikali kama yalivyoletwa kwenye jedwali hili kuhusiana na kifungu hiki ndiyo yaidhinishwe na Bunge kuwa sheria. Naomba kushauri.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mwandishi wa habari, naomba ku-*declare interest*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilikuwa napenda kupata ufafanuzi kwa Serikali kwa mabadiliko haya. Tumetoka kupitisha kifungu cha kumlinda mtu ambaye atatoa takwimu au atakosea kwa nia njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nataka Serikali iniambie je, huyu ambaye aidha ametangaza au amechapisha hiyo taarifa, lakini amepewa taarifa isiyo sahihi na huyo mtumishi, huyo analindwa vipi? Kwa sababu yeye ameenda, ametafuta taarifa, lakini aliyempa ndiye amekosea akachapisha. Je, yeye analindwa vipi? Bado ataenda kuhukumiwa kwa kosa ambalo sio la kwake, amepewa taarifa isiyo sahihi? Je, Serikali hili ililiangalia vipi?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ataeleza huko Mahakamani au Polisi atakapohojiwa. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 38

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya*

*Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 39

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya BungeZima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 40

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake))*

Jedwali la 1

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kwa niaba ya Mheshimiwa Wenje, naomba kuondoa kwa sababu imetosha.

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 2

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 3

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*
*(Bunge lilirudia)*

***Muswada wa Sheria ya Takwimu wa Mwaka 2013***
***[The Statistics Bill, 2013]***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Takwimu wa mwaka 2013 *(The Statistics Act, 2013)* kifungu kwa kifungu na kukubali pamoja na marekebisho. Naomba kutoa hoja kwamba Muswada huo sasa ukubaliwe rasmi. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu)*

**MWENYEKITI:** Muswada wa sheria hii umeishapitishwa na kuungwa mkono. Sasa, naipongeza Serikali, kwa hiyo, tuliyokuwa nayo tumemaliza. Katibu!

***Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi wa mwaka 2014***
***[The Tax Administration Bill, 2014]***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hunioni kabisa!

**MWENYEKITI:** Waziri!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Sionekani muda wote huo?
**MWENYEKITI:** Subiri nikuone ndiyo…

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Sasa huoni? Hauna macho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali, naomba ukae kwa sababu sijakuona. *(Kicheko)*

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Hauna macho au?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali, naomba ukae!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi *(The Tax Administration Act, 2014)* kifungu kwa kifungu na kukubali pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Muswada huo sasa ukubaliwe rasmi. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu)*

**MWENYEKITI:** Muswada huu umepita, kwa hiyo, naipongeza sana Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile hatuna muda wa kutosha kusoma Azimio. Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.25 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**HOJA ZA SERIKALI**

**A Z I M I O**

**Azimio la Kuridhia Makubaliano ya Msingi ya Ushirikiano Katika Bonde la Mto Nile *(Agreement on the Nile River Basin Co-operative Framework – CFA)***

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Azimio la Bunge kuhusu Makubaliano ya Msingi wa Ushirikiano katika Bonde la Mto Nile *(Agreement on the Nile River Basin Co-operative Framework – CFA)* na hatimaye liridhie Mkataba wa Kuanzisha ushirikiano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni miongoni mwa nchi 11 zilizomo katika Bonde la Mto Nile. Bonde hilo lina jumla ya kilometa za mraba milioni tatu mia moja kumi na mbili elfu mia tatu sitini na tatu na idadi ya wakazi wapatao milioni mia tatu. Kwa pamoja nchi hizo zinajulikana kama nchi za Bonde la Mto Nile. Eneo linalomilikiwa na kila nchi katika Bonde hilo ni Tanzania asilimia 3.73, Rwanda asilimia 0.65, Burundi asilimia 0.44, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo asilimia 0.69, Misri asilimia 9.52, Ethiopia asilimia 11.5, Eritrea asilimia 0.81, Kenya asilimia 1.62, Uganda asilimia 7.56, Jamhuri ya Sudani asilimia 43.95 na Jamhuri ya Sudani Kusini asilimia 19.54. Kwa sasa nchi ya Eritrea ni msikilizaji au *observer* katika ushirikiano wa Nchi za Bonde la Mto Nile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila nchi katika Bonde la Mto Nile inachangia na kutumia sehemu ya maji shirikishi ya Bonde hilo. Inakadiriwa kwamba Tanzania inachangia asilimia 28 ya maji shirikishi yote yanayoingia kwenye Ziwa Victoria ambalo ndilo chanzo kikuu cha maji ya Mto Nile na Bonde lake lote.

Kutoka eneo la Tanzania maji shirikishi yanayoingia katika Ziwa Victoria hutoka kwenye Mito ya Kagera, Mara, Mori, Simiyu, Isanga, Imbarageti na Gurumeti na hatimaye kuingia katika Mto Nile. Inakadiriwa kwamba hivi sasa Tanzania inatumia kiasi cha mita za ujazo bilioni 0.072 ya maji yote ya Bonde la Mto Nile kwa mwaka, ambayo ni sawa na asilimia 0.01 ya maji yote ya Mto Nile.

Maji ya Bonde la Mto Nile hutumika kwa shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na maji ya majumbani, kilimo cha umwagiliaji, uzalishaji umeme, viwanda, uvuvi na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kusimamia na kudhibiti matumizi ya rasilimali za maji za Bonde la Mto Nile, mwaka 1929 Serikali za Uingereza na Misri ziliingia Mkataba kuhusu matumizi ya maji ya Mto huo (*The Nile Waters Agreement),* ambapo Misri iliruhusiwa kutumia maji mita za ujazo bilioni arobaini na nane kila mwaka. Kiwango hicho kiliongezwa hadi kufikia mita za ujazo bilioni hamsini na tano nukta tano mwaka 1959. Mwaka huo nchi za Uingereza na Sudani ziliingia mkataba ambapo Sudani iliruhusiwa kutumia mita za ujazo bilioni kumi na nane nukta tano za maji ya Mto Nile.

Mikataba hiyo ambayo haikuzingatia mahitaji ya maji na maslahi ya nchi nyingine za Bonde hilo ilifanya kiasi cha maji ya Mto Nile kilichoruhusiwa kutumiwa na nchi za Misri na Sudani kuwa kwa pamoja mita za ujazo bilioni sabini na nne, sawa na asilimia 87 ya maji yote ya Mto Nile, ambayo inakadiriwa kuwa mita za ujazo bilioni themanini na tano.

Ukizingatia kuwa asilimia 10 ya maji yote ya Mto Nile hupotea kama Mvuke, basi nchi zote zilizobaki ziliachiwa asilimia tatu tu ya maji yote ya Mto Nile kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuwa na chombo cha kudumu cha ushirikiano katika nchi za Bonde la Mto Nile kitakachoratibu na kusimamia matumizi ya uwiano na maendeleo ya rasilimali za maji kwenye Bonde hilo, nchi hizo kwa pamoja, ama kwa makundi na kwa wakati tofauti, zilichukua hatua mbalimbali za ushirikiano juu ya matumizi endelevu na yenye manufaa kwa Bonde lote la Mto huo. Hatua hizo ni pamoja na kutekeleza

Mradi wa Kukusanya Takwimu za Kihaidrolojia na Kimtrolojia *(Hydromet Survey)* na kuandaa mizania ya rasilimali za maji katika nchi za Maziwa Makuu.

Nchi zilizohusika katika mradi huo wa *hydromet* ni Tanzania, Kenya, Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Rwanda na Burundi. Hili ilikuwa mwaka 1967, baadaye kuunda Kamati ya Ushirikiano wa Kiufundi na Maendeleo ya Utunzaji wa Mazingira katika Bonde la Mto Nile *(TECO-Nile)* mwaka 1992 na kuunda chombo cha mpito cha ushirikiano katika Bonde hilo la *Nile Basin Initiative* mwaka 1999 na baadaye makubaliano ya msingi wa ushirikiano wa nchi za Bonde la Mto Nile *(The Nile River Basin Co-operative Framework Agreement, 2009)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko la Azimio hili ni umuhimu uliojitokeza kwa nchi za Bonde la Mto Nile kuwa na ushirikiano madhubuti na wa kudumu kwa kuhifadhi, kuendeleza, kusimamia na kutumia kwa njia endelevu rasilimali za maji ya Bonde hilo kwa faida ya nchi zote hizo zilizopo katika Bonde la Mto Nile. Umuhimu huo ulitokana na nchi nyingi wanachama wa Bonde hilo kuipinga mikataba ya mwaka 1929 na mwaka 1959 iliyohusu matumizi ya maji ya Mto Nile iliyofikiwa kati ya Serikali ya Uingereza na Serikali za Misri na Sudani.

Kwa kuzingatia umuhimu huo, tamko la Wabunge wa Nchi za Bonde la Mto Nile *(Nile Basin Parliamentary Forum),* lililotolewa katika mkutano wao wa tarehe 6 hadi 7 Julai, 2012, kuwa nchi wanachama ziharakishe uundwaji wa chombo cha kudumu cha ushirikiano kinachoelezwa kwenye makubaliano hayo ya msingi wa ushirikiano wa Nchi za Bonde la Mto Nile ilitolewa. Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliwakilishwa na Wabunge wawili kwenye mkutano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kikao cha Baraza la Mawaziri wa Maji wa Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu cha tarehe 28 Februari, 2013, chini Uenyekiti wa Tanzania, ilikubalika kwamba, *CFA* iridhiwe ili Kamisheni ianzishwe mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifungu muhimu vya Mkataba: Makubaliano ya Msingi ya Ushirikiano Katika Bonde la Mto Nile *(CFA)* yana jumla ya vifungu arobaini na tano. Vifungu vyote, isipokuwa kifungu kidogo cha 14(b) vimeafikiwa na wanachama wote wa nchi hizo. Baadhi ya vifungu hivyo ni kama ifuatavyo:-

Moja, kifungu namba nne, matumizi yenye uwiano sawa na ya haki *(equitable and reasonable utilization)*.

Nchi za Bonde la Mto Nile zitatumia rasilimali za maji katika mfumo wa Mto Nile ndani ya mipaka yao katika hali ya usawa na uwiano. Rasilimali hizo zitatumiwa na kuendelezwa na nchi hizo kwa lengo la kuhakikisha matumizi endelevu na yenye manufaa kwa kuzingatia maslahi ya nchi husika na mifumo thabiti ya kulinda rasilimali hizo. Kila nchi katika Bonde la Mto Nile, ina haki ya matumizi endelevu yenye uwiano sawa na ya haki.

Pili, kifungu namba tano, wajibu wa kila nchi kuzuia madhara makubwa kwa watumiaji wengine wa rasilimali za maji katika Bonde la Mto Nile.

Nchi za Bonde la Mto Nile zitawajibika kuchukua hatua muafaka kuzuia athari kwa nchi nyingine katika matumizi ya rasilimali za maji katika Bonde hilo. Iwapo nchi moja itasababisha athari kwa nchi nyingine kinyume na makubaliano haya, nchi iliyosababisha athari hiyo itachukua hatua mahususi kwa kuzingatia kifungu namba nne ili kuwasiliana na nchi athirika katika kuondoa au kuzuia athari hiyo. Vilevile majadiliano yatafanyika kuhusu suala la fidia endapo itaonekana kuna umuhimu wa kufanya hivyo.

Tatu, kifungu namba 11, kuzuia na kupunguza uwezekano wa kuleta madhara.

Katika kifungu hiki nchi za Bonde la Mto Nile zitafanya kila jitihada kuchukua hatua muafaka kwa nchi moja moja au inapoonekana inafaa kwa ushirikiano na nchi inayoweza au zinazoweza kuathirika na hivyo kuchangia gharama za kuzuia na au kupunguza madhara kwa nchi nyingine katika Bonde hilo, ikiwa ni pamoja na madhara yanayosababishwa na binadamu au maafa asilia kama vile mafuriko, magugumaji, magonjwa yatokanayo na maji, mmomonyoko wa ardhi, ukame au hali ya jangwa. Nchi za Bonde zitatekeleza kifungu hiki kulingana na mwongozo utakaotolewa na Kamisheni ya Bonde la Mto Nile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu Namba 13 ni cha kulinda Bonde la Mto Nile na miundombinu yake wakati wa migogoro ya vita ya kutumia silaha. Kila nchi katika Bonde inawajibika kulinda na kuhakikisha kuwa miundombinu, mitambo na vifaa mbalimbali vilivyosimikwa kwenye Bonde hilo vinapewa ulinzi kwa kuzingatia misingi ya Sheria za Kimataifa zitumikazo wakati wa vita na migogoro ya kutumia silaha.

Tano, Kifungu Namba 14, Usalama na Haki ya Kutumia Maji. Kwa kuzingatia vifungu namba nne na namba tano, Nchi za Bonde la Mto Nile, zinatambua umuhimu wa usalama na haki ya kutumia maji kwa kila nchi; na kwamba ushirikiano katika kusimamia na kuendeleza maji ya mfumo wa Mto Nile utawezesha kila moja ya nchi hizo kufikia malengo ya usalama wa maji na manufaa mengineyo. Kwa hiyo, Nchi za Bonde la Mto Nile zinakubaliana kuwa:-

(i) kushirikiana na kuhakikisha kuwa Mataifa yote yanafanikiwa katika kufikia na kuendeleza usalama wa maji; na

(ii) kutoathiri kwa kiasi kikubwa usalama wa maji wa nchi nyingine yoyote ya Bonde la Mto Nile *(not to significantly affect the water security of any other Nile Basin State)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu namba 17, Muundo wa Kitaasisi. Itaundwa Kamisheni ya Bonde la Mto Nile ambayo itakuwa na vyombo vya kitaasisi vifuatavyo:-

(a) Mkutano wa Wakuu wa Nchi. Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali utawashirikisha Marais wa Nchi na Serikali katika Bonde la Mto Nile. Mkutano wa Marais utatayarisha sheria na taratibu zake na utakuwa ndiyo chombo cha juu cha kuandaa Sera za Kamisheni hiyo.

(b) Baraza la Mawaziri. Kila nchi mwanachama itawakilishwa kwenye Baraza hilo na Waziri mwenye dhamana ya usimamizi wa rasilimali za maji. Baraza litakutana mara moja kila mwaka au kwa dharura kama itabidi. Baraza limepewa mamlaka na majukumu kama ilivyooneshwa katika Kifungu cha 24 cha makubaliano haya.

(c) Kamati ya Ushauri wa Kitaalam. Kamati itakuwa na Wajumbe wawili kutoka kila nchi wanachama ambao ni Maafisa wa ngazi za juu *(Senior Officials)*. Wajumbe hao wanaweza pia kuambatana na wataalam wengine kama kuna majadiliano yanayohitaji utaalam zaidi. Kamati hii itakutana mara mbili kila mwaka au kwa dharura kama inabidi. Mamlaka na majukumu ya kamati hiyo yanaoneshwa katika Kifungu cha 26 cha Mkataba huu.

(d) Kamati za Ushauri wa Kisekta. Baraza la Mawaziri linaweza kuunda Kamati za Ushauri za Kisekta kushughulikia masuala mahususi ya Kisekta ndani ya Kamisheni. Kamati za Ushauri wa Kisekta zitakuwa na Mjumbe mmoja kutoka kila Nchi ya Bonde la Mto Nile atakayekuwa ni mtaalam katika nyanja husika. Kamati hizi zitaongozwa chini ya sheria na taratibu zinazotumiwa na Kamati ya Ushauri wa Kitaalam. Mamlaka na majukumu ya Kamati hizi yanaoneshwa katika Kifungu cha 28 cha makubaliano.

(e) Sekretarieti. Sekretarieti itakayoongozwa na Katibu Mtendaji ambaye atachaguliwa kwa kipindi cha miaka mitatu na Baraza la Mawaziri itaundwa. Katibu Mtendaji atawajibika kwa Baraza la Mawaziri kupitia Kamati ya Ushauri wa Kitaalam. Katibu Mtendaji na Maafisa wengine wa Sekretarieti watapewa marupurupu na kinga za kidiplomasia zinazostahili kwa utendaji wa kazi zao katika Nchi za Bonde la Mto Nile.

Ofisi ya Sekretarieti itakuwa katika Makao Makuu ya Kamisheni. Majukumu ya Katibu Mkuu pamoja na Sekretarieti hiyo yameoneshwa katika Kifungu Namba 30 cha Makubaliano.

Saba, Usalama na Haki ya Kila Nchi Mwanachama Kutumia Maji. Kwa kuzingatia vifungu namba 4 na namba 5 vya makubaliano haya, nchi za Bonde la Mto Nile zinatambua umuhimu wa usalama na haki ya kila nchi mwanachama kutumia maji. Nchi hizo pia zinatambua kwamba ushirikiano katika kusimamia na kuendeleza maji ya mfumo wa Mto Nile utaweza kufikiwa kwa malengo ya Usalama wa Maji na manufaa mengine; hivyo, kama ilivyoelezwa kwenye Kifungu Namba 14(a), Nchi za Bonde la Mto Nile zinakubaliana kushirikiana katika kuhakikisha kuwa nchi zote zinakuwa na usalama wa maji wakati wote *(to work together to ensure that all states achieve and sustain water security)*.

Kifungu Namba 14(b) ambacho kinasema, kutoathiri kwa kiasi kikubwa usalama wa maji wa nchi nyingine yoyote ya Bonde la Mto Nile *(not to significantly affect the water security of any other Nile Basin State)*. Kutokubalika kwa Kifungu Namba 14(b) cha Makubaliano hayo kunasababisha nchi za Misri na Sudani kutosaini Mkataba huo hadi sasa. Nchi hizo zinataka kuendelea kutumia maji mengi zaidi kama zilivyopewa kupitia Mikataba ya mwaka 1929 na 1959. Misri na Sudani zinataka Kifungu Namba 14(b) kisomeke kama ifuatavyo: "*Not to adversely affect the water security and current uses and right of any other Nile Basin State.*" Nami nataka kurudia hapa; *not to adversely affect the water security and current uses and rights of any other Basin State,* kwa maana zinataka kubaki na makubaliano ya awali; jambo linalopingwa na nchi nyingine zote za Bonde la Mto Nile ambazo haziitambui Mikataba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya kuridhia Makubaliano ya Msingi ya Ushirikiano. Katika mchakato ya majadiliano ya kuunda chombo cha kudumu cha ushirikiano, Tanzania na nchi nyingine zimeafiki kuridhia makubaliano husika ambapo matokeo yake ni pamoja na:-

Moja, kuzihamasisha nchi nyingine zisaini *CFA* ili ziridhie makubaliano hayo, ambapo hadi sasa nchi za Ethiopia na Rwanda zimesharidhia Makubaliano hayo. Nchi nyingine zipo katika hatua mbalimbali za kuridhia kutegemeana na utaratibu wa Katiba zao.

Pili, kuanzishwa Kamisheni ya Bonde la Mto Nile itakayokuwa na jukumu la kutekeleza shughuli mbalimbali za ushirikiano.

Tatu, kuongeza kwa kiwango cha elimu na ujuzi kwa wananchi kutokana na utekelezaji wa miradi katika Bonde kwa kutumia teknolojia za kisasa.

Nne, kuongezeka kwa ajira kutokana na kutekelezwa kwa miradi mbalimbali katika Bonde.

Tano, kudhibitiwa kwa uharibifu na uchafuzi wa mazingira katika Bonde hilo.

Sita, kushiriki katika ufumbuzi wa migororo ya matumizi ya rasilimali za maji ili kuimarisha ujirani mwema na amani katika Bonde la Mto Nile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kuridhia. Kila Nchi Mwanachama itaridhia makubaliano hayo kwa mujibu wa Katiba ya nchi husika. Bunge la Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania ndiyo chombo chenye mamlaka ya kuridhia Makubaliano hayo kwa Tanzania. Hivyo, naliomba Bunge kuridhia makubaliano haya kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu gharama za kuridhia Makubaliano. Hapatakuwa na gharama za rasilimali fedha katika kuridhia Makubaliano hayo, isipokuwa wakati wa utekelezaji wake fedha zitatakiwa kutengwa kila mwaka katika Bajeti ya Serikali kwa ajili ya shughuli zifuatazo:-

(i) Mchango wa kila mwaka wa uanachama kwa kiwango kitakachopangwa na kukubalika na nchi wanachama na kwa sasa mchango huo ni Dola za Kimarekani 1,037,037.

(ii) Gharama za kutekeleza Miradi ya Pamoja itakayokubaliwa na nchi wanachama.

(iii) Kuandaa na kuhudhuria Mikutano ya Kamisheni.

Saba, ushirikishwaji wa wadau. Katika kuandaa Azimio hili wadau walioshirikishwa ni pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Wizara za Sheria na Katiba, Wizara ya Fedha, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi na Baraza la Usimamizi wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ratiba ya utekelezaji; hadi sasa nchi mbili kati ya nchi 11 ambazo ni Ethiopia na Rwanda zimekwisharidhia Makubaliano ya Kuanzisha Ushirikiano wa Bonde la Mto Nile na nyingine isipokuwa Misri na Sudani zipo katika hatua mbalimbali za kuridhia. Tanzania ikiridhia Mkataba huo itaweza kuongeza idadi ya nchi zilizoridhia ili kukaribia kufikia lengo la theluthi mbili ya nchi wanachama wanaotakiwa kuridhia ili Kamisheni ianze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, baada ya maelezo haya ya utangulizi, naomba sasa niwasilishe Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Ushirikiano katika Bonde la Mto Nile kama ifuatavyo:-

Azimio la Bunge la Kuridhia Mapendekezo ya Makubaliano ya Msingi ya Ushirikiano katika Bonde la Mto Nile.

KWA KUWA Bonde la Mto Nile lina jumla ya kilometa za mraba 3,112,363 na idadi ya wakazi wapatao milioni 300;

NA KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa nchi 11 zilizomo katika Bonde la Mto Nile zinazojulikana kama nchi za Bonde la Mto Nile ambazo ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rwanda, Burundi, Misri, Ethiopia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Eritrea, Kenya, Uganda, Jamhuri ya Sudani na Jamhuri ya Sudan Kusini;

NA KWA KUWA kila nchi katika Bonde la Mto Nile inachangia na kutumia sehemu ya maji shirikishi ya Bonde hilo na Tanzania inachangia maji shirikishi yanayoingia kwenye Ziwa Victoria ambalo ndilo chanzo kikuu cha maji ya Mto Nile na Bonde hilo kwa ujumla;

NA KWA KUWA Tanzania kwa kutambua umuhimu wa kusimamia matumizi ya uwiano endelevu wa rasilimali za maji kwenye Bonde hilo ilishirikishwa katika Mradi wa kukusanya takwimu za kihaidrolojia na kimetrolojia, kuunda mizania ya rasilimali za maji katika nchi za Maziwa Makuu, kuunda Kamati ya Ushirikiano ya Kiufundi ya Maendeleo ya Utunzaji wa Mazingira katika Bonde la Mto Nile, kuunda chombo cha mpito cha ushirikiano na kuwa na makubaliano ya msingi ya ushirikiano wa Bonde la Mto Nile;

NA KWA KUWA wakati wa ukoloni, Serikali ya Uingereza, Misri pamoja na Sudani ziliingia mkataba kwa kila nchi kugawana kiasi cha maji na mikataba hiyo haikuzingatia mahitaji ya maji na masilahi ya nchi nyingine katika Bonde hilo;

NA KWA KUWA maji ya Bonde hilo yanatumika katika shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na majumbani, kilimo cha umwagiliaji, uzalishaji wa umeme, viwanda, uvuvi na utalii na makubaliano ya msingi ya ushirikiano katika Bonde hilo yatasaidia katika kuleta usawa kwenye matumizi na uwiano wa kupata maji katika nchi zote za Bonde hilo;

NA KWA KUWA Tanzania itanufaika na makubaliano hayo kwa kupata matumizi sawa na ya haki na pia uendelezaji na utumiaji wa rasilimali za maji kuzuia madhara makubwa kwa watumiaji wengine wa rasilimali hizo, kulinda Bonde na miundombinu yake wakati wa migogoro na vita vya kutumia silaha na usalama wa haki ya kutumia maji;

NA KWA KUWA kuridhiwa kwa Mkataba huu na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kunaipa nchi yetu mgawanyiko mzuri wa rasilimali za maji pamoja na utunzaji wa rasilimali hii na kuwezesha uanzishwaji wa chombo cha kudumu cha usimamizi wa rasilimali za Bonde la Mto Nile;

HIVYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu na faida za Makubaliano haya kwa Jamhuri ya Muungano, Bunge katika Mkutano wake wa Kumi na Tisa na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, linaazimia kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Makubaliano ya Msingi na Ushirikiano katika Bonde la Mto Nile *(Agreement on the Nile River Basin Co-operative Framework - CFA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Naomba sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati iliyojadili Azimio hili. Mheshimiwa Prof. Msolla!

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba niwasilishe maoni na ushauri kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Malibaliano ya Ushirikiano katika Bonde la Mto Nile *(Agreement on the Nile River Basis Coo-perative Framework - CFA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 21 Oktoba, 2014, Waziri wa Maji, Mheshimiwa Prof. Jumanne Abdallah Maghembe (Mbunge) aliwasilisha mapendekezo ya Azimio tajwa mbele ya Kamati. Aidha, Kamati ilipata fursa ya kujadiliana na wadau mbalimbali kuhusu mapendekezo ya Azimio hilo na Kamati ilizingatia maoni na ushauri kutoka kwa wadau hao.

Mambo ya msingi yaliyozingatiwa na Kamati. Katika kuhakikisha kuwa kazi uliyoipa Kamati inakuwa na tija na kuzingatia matarajio ya wananchi, Kamati ilitaka kujiridhisha kwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

Moja, chimbuko la uamuzi wa kusaini Makubaliano hayo. Wizara iliieleza Kamati kwamba, Tanzania ni miongoni mwa nchi 11 zilizomo katika Bonde la Mto Nile na zinajulikana kama nchi za Bonde la Mto Nile. Nchi hizo zinajumuisha nchi za Tanzania, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Misri, Ethiopia, Eritrea, Kenya, Uganda, Jamhuri ya Sudani na Jamhuri ya Sudani Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Wizara yalionesha kuwa karibu nchi zote katika Bonde la Mto Nile, zinachangia na kutumia sehemu ya maji shirikishi ya Bonde hilo. Tanzania inakaribia kuchangia asilimia 28 ya maji yanayoingia kwenye Ziwa Victoria ambacho ndicho chanzo cha *White Nile* iliyo mchangiaji muhimu wa maji katika Mto Nile Mkuu. Aidha, Tanzania inakadiriwa kutumia kiasi cha mita za ujazo zipatazo bilioni 0.072 za maji kwa mwaka, ambayo ni sawa na asilimia 0.1 tu ya maji yote ya Mto Nile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilizingatia maelezo kwamba, wakati wa ukoloni nchi ya Uingereza ambayo ndiyo ilikuwa mtawala wa Tanganyika na Uganda, ilisaini Mikataba miwili mwaka 1929 na mwaka 1959 na nchi za Sudani na Misri kuhusu matumizi ya maji ya Mto Nile, yaani *The Nile Waters Agreement.*

Mikataba hiyo ilizipa haki matumizi ya maji nchi za Misri kutumia mita za ujazo bilioni 55.5 na Sudani mita za ujazo bilioni 18.5 kwa mwaka. Kiasi hiki cha maji kilichotengwa kwa ajili ya nchi hizi mbili ni sawa na asilimia 87 ya maji yote ya Mto Nile, yaani mita za ujazo bilioni 85. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa, kiasi cha maji cha Mto Nile kinachopotea kwa njia ya mvuke, yaani *evaporation,* ni asilimia 10. Hii ina maana kwamba, ni kiasi cha asilimia 3 tu ya Mto Nile kinachobaki kwa matumizi ya nchi tisa zilizobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine muhimu ambalo Kamati ilielezwa ni kwamba, nchi nyingi za Bonde la Mto Nile ikiwemo Tanzania, hazijaridhika na Mikataba hiyo iliyosababisha uwiano usio sawa wa matumizi ya maji ya Mto Nile. Hili ndiyo chimbuko la nchi mbalimbali za Bonde la Mto Nile kuandaa Azimio la Kuanzisha Makubaliano ya Msingi ya Ushirikiano wa Nchi za Bonde la Mto Nile kwa nia ya kurekebisha hali iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutimiza azma ya nchi nyingi za Bonde la Mto Nile ya kupata usawa na haki ya matumizi ya rasilimali ya maji ni muhimu Bunge lako Tukufu liridhie Mkataba huu ili kuipa nchi yetu mgawo mzuri wa rasilimali muhimu ya maji, kuhakikisha utunzaji wake pamoja na kuwezesha uanzishaji wa chombo cha kudumu, yaani Kamisheni ya Bonde la Mto Nile *(Nile Basin Commission),* itakayosimamia rasilimali za Bonde la Mto Nile.

Madhumuni na faida zitakazopatikana kutokana na kuridhia Makubaliano ya Msingi ya Ushirikiano katika Bonde la Mto Nile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Azimio hili ni Kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Makubaliano ya Msingi ya Ushirikiano katika Bonde la Mto Nile ili kupata matumizi sawa na ya haki ya rasilimali za maji ya Mto Nile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni na faida zitakazopatikana kwa kukubali Mkataba unaopendekezwa ni kama ifuatavyo:-

Moja, kuwepo kwa makubaliano yatakayohakikisha nchi washiriki wa Bonde la Mto Nile zinapata matumizi ya haki na yenye uwiano ya rasilimali ya maji ya Mto Nile. Matumizi hayo ni

pamoja na uzalishaji umeme, kilimo cha umwagiliaji, uvuvi, ufugaji na matumizi ya maji majumbani.

Pili, kuundwa kwa Kamisheni ya Bonde la Mto Nile ambacho kitakuwa chombo cha ushirikiano wa kudumu chenye nguvu ya kisheria.

Tatu, kuimarisha ushirikiano wa kijamii, kiuchumi na kiutamaduni na kuongeza ajira katika nchi za Bonde la Mto Nile.

Nne, kuwezesha matumizi endelevu ya Mto Nile kwa kutunza mazingira yake; na

Tano, kuundwa kwa chombo cha kutatua migogoro ya maji pindi inapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujadili Azimio hili kama lilivyowasilishwa na Wizara na kwa kuzingatia maoni ya wadau, Kamati iliridhika na sababu zilizotolewa na Serikali na hivyo kuliomba Bunge lako Tukufu likubali kuridhia Azimio la Kuanzisha Mkataba wa Makubaliano ya Msingi ya Ushirikiano katika Bonde la Mto Nile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwa mstari wa mbele katika kuandaa Mkataba huu wa ushirikiano tangu hatua za awali mwezi Januari, 1997 wakati jopo la Wataalamu (*Panel of Experts*), lilipoundwa. Aidha, kuanzia mwaka 2003 hadi mwisho wa majadiliano mwezi Mei, 2010, Tanzania ilikuwa Mwenyekiti wa nchi saba za Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Ethiopia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, kwa ngazi za Wataalamu na Mawaziri wa Maji katika Baraza la Mawaziri wa Nchi za Bonde la Mto Nile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia juhudi hizi, Tanzania ingepaswa kuwa ya kwanza kuridhia Mkataba huu; hivyo basi, Kamati yangu inalishauri Bunge lako Tukufu, liridhie Azimio hili ili kufanikisha mchango huu muhimu kutoka kwa Serikali yetu ya Tanzania.

Pamoja na umuhimu wa kuridhia Azimio hili, Kamati inaishauri Serikali kuwa na mikakati thabiti ya utekelezaji wa Mkataba huu pindi utakaporidhiwa na nchi washirika.

Mikakati hiyo ni pamoja na ifuatayo:-

Moja, kujenga uwezo wa kitaasisi na rasilimali watu hususan vijana ili kuhimili ushindani katika nafasi za Kamisheni ya Bonde la Mto Nile pindi itakapoundwa. Aidha, uwezo wa rasilimali watu ujikite katika nyanja mbalimbali za utaalamu wa maji, mazingira, sheria, lugha za kigeni hususan kiarabu na uwezo wa kistadi wa kujadiliana.

Pili, kuwa tayari kutoa mchango wa kila mwaka wa wanachama kwa kiwango kitakachopangwa na kukubalika na nchi wanachama ili kuendesha Taasisi itakayoundwa.

Tatu, kujiandaa kwa majidiliano ya kutumia maji kwa haki na usawa kwa kuhakikisha tafiti za kisayansi zinafanyika ili kujua mahitaji yetu ya maji kwa sekta muhimu za kiuchumi na kijamii. Mahitaji hayo yawekwe wazi kwa nchi wanachama wa Bonde la Mto Nile.

Nne, kuandaa mipango madhubuti ya pamoja ya maji na utekelezaji wake upewe kipaumbele kwa kutengewa bajeti ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijiografia Tanzania ipo ukanda wa juu *(upstream)* wa mifumo ya maji na hivyo kuwa na maji mengi ambayo ni shirikishi kuliko nchi nyingine yoyote katika Bara la Afrika. Nchi yetu inachangia asilimia 60 kwenye Ziwa Nyasa, asilimia 28 kwenye Ziwa Victoria

na asilimia 60 kwenye Ziwa Tanganyika. Kamati inaishauri Serikali yetu kujiwekea mikakati ya namna ambavyo nchi yetu itanufaika na maji shirikishi *(transboundary waters)*. Kamati inashauri mikakati hiyo iwe ni pamoja na:-

Moja, kuimarisha Kitengo cha Maji Shirikishi katika Wizara ya Maji kwa kukipatia wataalamu wa kutosha na wenye weledi wa masuala ya maji shirikishi; na

Mbili, kuwa na wataalamu wa masuala ya rasilimali za maji kwenye Balozi zetu za Misri na Uganda ili kuhakikisha taarifa zote muhimu kuhusu shughuli zinazofanyika katika Bonde la Mto Nile zinapatikana kwa haraka na kwa uhakika. Hii ni kutokana na ukweli kuwa, Nchi ya Misri, ambayo ndiyo mpingaji mkuu wa Mkataba huu, ina Wataalamu Wakazi *(Resident Experts)* katika Miji ya Jinja na Kampala kuanzia mwaka 1959.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Kuanzisha Makubaliano ya Msingi ya Ushirikiano katika Bonde la Mto Nile una jumla ya vifungu 45. Vifungu vyote isipokuwa kifungu cha 14(b), vimeafikiwa na Nchi Wanachama. Kifungu hiki kinachotamka: "*Kutoathiri kwa kiasi kikubwa usalama wa maji wa nchi nyingine yoyote ya Bonde la Mto Nile (Not to significantly affect the water security of any other Nile Basin State)*, bado hakijaafikiwa na Nchi za Misri na Sudani.

Nchi hizi hususan Misri, zinasisitiza kuendelea kutumia maji mengi kuliko nchi nyingine Wanachama kama ilivyotamkwa katika Mikataba iliyosainiwa baina ya nchi hizo na Uingereza. Nchi hizo zinataka Kifungu 14 (b) kisomeke: "*Kutoathiri usalama wa maji wa nchi nyingine yoyote ya Bonde la Mto Nile na haki na matumizi ya sasa yaendelee* (*Not to adversely affect the water security and current uses and rights of any other Nile Basin State).*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi chote cha majadiliano kuhusu Mkataba huu, Nchi Wanachama zimekuwa zikitambua umuhimu wa Mto Nile kwa nchi za Misri na Sudani, kwa kuzingatia kwamba, nchi hizo hazina vyanzo mbadala vya maji. Hata hivyo, hali hii haiwezi kuwa kigezo cha kuzipa nchi hizi ukiritimba wa haki ya kutumia maji ya Mto Nile zaidi ya nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili ambalo Bunge lako linaombwa kuridhia, linaainisha usalama na haki ya kutumia maji pamoja na wajibu na misingi inayozuia nchi moja kuathiri nchi nyingine mwanachama. Msimamo unaooneshwa na nchi za Misri na Sudani, hususan Misri kutaka Mkataba huu usiathiri kiwango cha matumizi ya maji na haki walizonazo kwa sasa, yaani *current uses and rights,* ni kutaka kuzirudisha Nchi Wanachama wa Bonde la Mto Nile kwenye Mikataba ya Kikoloni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu cha 17 kinachozungumzia Muundo wa Kitaasisi wa Kamisheni ya Bonde la Mto Nile itakayoundwa chini ya Mkataba huu, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Kifungu cha 17 (a) cha Mkataba huu kinatamka kwamba, Mkutano wa Wakuu wa nchi ndiyo utakuwa chombo cha juu cha kuandaa Sera za Kamisheni. Kamati inashauri kuwa, kwa kuwa hili ni jukumu la kiutendaji, jukumu hili lifanywe na Kamati za Ushauri wa Kisekta na Mkutano wa Wakuu wa nchi uwe chombo cha kupitisha Sera hizo.

(ii) Pamoja na Vyombo vya Kitaasisi vilivyotajwa katika kifungu hiki, Kamati inashauri Muundo huu wa Taasisi ujumuishe Kamati ya Wabunge kutoka nchi za Bonde la Mto Nile (*Nile Basin Parliamentarians Forum*) ili kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuipa Kamati yangu jukumu la kujadili Azimio hili na hatimaye kuwasilisha maoni na ushauri kuhusu Azimio la Bunge na Mapendekezo ya Kuridhia Makubaliano ya Msingi ya Ushirikiano katika Bonde la Mto Nile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa ushirikiano mkubwa walioutoa wakati wa kujadili Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru kwa dhati Waziri wa Maji, Mheshimiwa Prof. Jumanne Abdallah Maghembe (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Amos Makalla (Mb) na Watendaji wote wa Wizara, kwa ushirikiano walioipa Kamati ilipokuwa ikijadili Azimio hili. Aidha, kipekee kabisa, namshukuru Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya (Mb), kwa ushirikiano aliouonesha akiwa kama mdau muhimu wa Mkataba huu wa Makubaliano ya Msingi ya Ushirikiano katika Bonde la Mto Nile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru wewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuipatia Kamati yetu maelekezo mbalimbali ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Kamati, Ndugu Grace Bidya na Msaidizi wa Kamati, Ndugu Sophia Vumbi, kwa kuratibu vema shughuli zote za Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa ninamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani!

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Awali ya yote, napenda kutambua uwepo wa Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais, ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Kitope, maarufu kwa kuchukua vijana kutoka Tanzania Bara na kuwapeleka Zanzibar kuandikishwa kwenye Daftari la Wapiga Kura. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio la Mkataba wa Kuridhia Mkataba wa Ushirikiano wa Nchi Wanachama wa Bonde la Mto Nile, yanayotolewa chini ya Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2013.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rukia, subiri kuna Mwongozo. Mheshimiwa *Chief Whip!*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni zetu, Mbunge haruhusiwi kusema maneno ambayo hana uhakika nayo. Kwa jinsi ninavyoelewa na uhakika nilionao, chaguzi zote katika nchi yetu ya Tanzania zinaongozwa kwa Sheria na Katiba. *(Makofi)*

Wapiga kura wote wamekuwa wakiandikishwa kwenye madaftari na madaftari hayo wanaya-*display* ili kuwaorodhesha wapiga kura. Wale ambao siyo wapiga kura mara zote kama wameorodheshwa kwenye daftari na siyo wapiga kura halali, Tume zimekuwa na muda wa kutoa maelezo hayo.

Ninaomba Mheshimiwa Mbunge afute kauli yake hiyo, kama hataki kufuta basi Kiti chako na Ofisi yako kimwombe alete ushahidi ndani ya Ofisi ya Bunge wa jambo hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rukia, ninaomba ufute maneno uliyoanza nayo ili twende vizuri.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafuta kauli yangu, lakini *message sent*. *(Makofi)*

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Azimio la Mkataba wa Kuridhia Mkataba wa Ushirikiano wa Nchi Wanachama wa Bonde la Mto Nile, yanatolewa chini ya Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bonde la Mto Nile lina wakazi milioni 160 katika eneo la ukubwa wa kilomita za mraba milioni 3.1, ikiwa ni pamoja na Maziwa yenye ukubwa wa kilomita za mraba 81,500 na chepechepe au oevu *(swamps)* zenye ukubwa wa kilomita za mraba 70,000, kulingana na takwimu za Mpango wa Bonde la Mto Nile, chombo kilichoanzishwa na Mataifa yanayotumia Mto Nile kwa ufadhili kutoka kwa wahisani mbalimbali ili kuwa na sera zinazofanana kuhusu Mto Nile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siasa za maji katika Bonde la Mto Nile, ni utafiti uliofanywa na *European Union Institute for Security Studies* na kuandikwa na *Any Freitas* Mei, 2013 chini ya Jarida la *Alert Issues*. Siasa za maji kutoka katika Bonde la Mto Nile ni siasa zinazofanywa na nchi za juu kwa maana ya Mto Nile unapotokea, yaani Burundi, Rwanda, Tanzania, Uganda, Kenya na Ethiopia na nchi za chini maana Mto Nile unapopitia wakati unaingia Bahari ya Mediterranean, yaani Sudani na Misri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji ya Mto Nile, matumizi na utawala wa maji limekuwa ni zoezi tete. Kwa miaka mingi hadi sasa hakujawahi kuwepo na makubaliano ya pamoja kwa nchi watumiaji wa maji ya Mto Nile juu ya dira na jinsi ya matumizi ya maji ya Mto huo.

Kumekuwepo na juhudi kadhaa za kuweka utaratibu lakini takribani zote zimebakia kwenye makaratasi tu. Utaratibu unaotumika ni ule wa Mkataba wa mwaka 1929 wa Misri kutumia maji ya Mto Nile yenye ujazo wa si chini ya kilomita 48 kwa mwaka, wakati Sudani ilipangiwa kutumia kilomita za ujazo nne na kilomita za ujazo 32 hazikupangiwa nchi yoyote.

Mkataba huu haukuzifikiria nchi zingine ambazo Mto Nile unatokea na pia ulipiga marufuku kwa nchi zingine zinazozungukwa na vyanzo vya maji vya Mto Nile, yaani Afrika ya Mashariki, kujenga kitu chochote cha maendeleo kitakachotumia maji ya Mto huo bila ya ridhaa ya Misri na Sudani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kufanya tafakuri ya Azimio lenyewe naomba kwanza kuangalia taarifa iliyotolewa kwenye Jarida la *World Bulletin* kuhusu mapatano au makubaliano ambayo Tanzania ilikuwa ikisisitiza kuhusu matumizi ya rasilimali ya maji ya Mto Nile, kama yalivyotiwa saini mwaka 2010 na Nchi Wanachama nchini Uganda na kujulikana kama Makubaliano ya Entebe.

Makubaliano hayo yalilenga kuondokana na Mkataba wa Kikoloni ambao ulitoa haki kubwa ya matumizi ya maji ya Mto Nile kwa nchi za Misri na Sudani. Kwa makusudi, nchi zote za Misri na Sudani zilikataa kusaini Makubaliano hayo mapya ya matumizi ya maji ya Mto Nile, kwa kuhofia kuwa yataathiri Mkataba wa Kikoloni uliokuwa unawapa haki kubwa ya matumizi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Mwakilishi wa Uganda katika Timu ya Wataalam ya *Nile Basin Initiative*, Bwana Callist Tindimugaya, anasema kuwa; "*Tanzanian Foreign Minister, Bernard Kamillius Membe has called for a review of the CFA to consider Egypt's water needs. Tanzania was the one pushing for the agreement; it would be a surprise to see them backtracking now.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje, Mheshimiwa Bernard Membe ni kwamba Tanzania inajihisi vibaya sana kwa sura inayotoa haki sawa kwa matumizi ya rasilimali ya maji kwa nchi mwanachama; hivyo, inaona ni bora sura hiyo irejeshwe ili nchi ya Misri iweze kupata haki zaidi ya matumizi ya maji kwa kuwa wao wako jangwani zaidi ukilinganisha na Mataifa mengine wanachama. Ushauri au ushawishi huu wa Mheshimiwa Membe ulipigwa vita vikali na Wawakilishi wa Sudani ya Kusini na Uganda. Japokuwa Sura ya 36(1) ya Mkataba inatoa haki kwa nchi wanachama kushauri marekebisho yoyote katika Mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya msingi hapa ni je, ushawishi huu Mheshimiwa Membe ulikuwa ni kwa kuiwakilisha Tanzania au ulikuwa ni ushawishi wake yeye binafsi kwa mapenzi yake kwa Misri?

Ni ukweli kwamba Tanzania kama nchi matumizi ya maji ya Ziwa Victoria kwa matumizi ya kiuchumi bado ni madogo sana kwa kulinganisha na nchi wanachama. Hii inaweza kuwa inatokana na Mkataba huo kandamizi wa kuwapa Misri na Sudani haki kubwa au ni kutokana na kushindwa kwetu kutumia rasilimali hii kutokana na kutokuwa wabunifu au kukosa dira kwenye matumizi ya maji ya Maziwa yaliyotuzunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba huu mpya wa Ushirikiano unaoridhiwa na Bunge lako katika sehemu ya kwanza inayohusu Kanuni za Ujumla za Mkataba, Ibara ya 3 (1) inasema kuwa; "…, *mutual benefit and good faith in order to attain optimal utilization and adequate protection and conservation of the Nile River Basin and to promote joint efforts to achieve social and economic development.*" Aidha, Ibara ya 3(6) inaonyesha kuwa, kila nchi wanachama ina haki ya kutumia maji yaliyo ndani ya mipaka yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani haipingani kabisa na Mkataba huu bali inapongeza kwani kwa kipindi kirefu kimekuwa ni kilio cha baadhi ya nchi mwanachama kuwa pindi watakapokutumia maji ya Mto Nile, watakumbana na vitisho vya nchi zilizokuwa na haki zaidi kwa mujibu wa Mkataba wa Kikoloni na hivyo kukutana na kitisho cha kutumia nguvu za kijeshi. Hivyo basi, kama Tanzania, ni muda mwafaka sasa kuhakikisha tunatenga rasilimali ya kutosha ili maeneo makame ambayo yamelizunguka Ziwa Victoria yaweze kutumia maji hayo kwa shughuli za kijamii na za kiuchumi kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji wa Tume ya Pamoja ya *Nile River Basin*. Sehemu ya III ya Itifaki inaeleza juu ya uanzishwaji wa Kamisheni ya Pamoja ya Nchi za Bonde la Mto Nile. Kwa kuwa Mkataba wa Ushirikiano umeshasainiwa na nchi wanachama karibu wote isipokuwa nchi za Sudani na Misri, lakini kwa safari ya Kamati iliyofanywa hivi karibuni nchini Sudani, ni dhahiri ushawishi huo unaweza kuzaa matunda na nchi hiyo ikasaini Mkataba wa Ushirikiano na hivyo kubakiwa na Mwanachama mmoja tu ambaye ni Misri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yetu kuwa ushawishi kama ulivyofanyika kwa Sudani uendelee kufanyika kwa Misri na mwishowe Tume ya Pamoja itaundwa na itafanya kazi kama Mkataba unavyoeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Kilimo inatumia takribani asilimia 75 ya maji yote kutoka kwenye Bonde la Mto Nile, kwa nchi za Misri na Ethiopia zinatumia takribani asilimia 86 ya

maji yote na Sudani inatumia asilimia 94. Kwa nchi hizi mbili za Sudani na Misri zinategemea sana kilimo cha umwagiliaji na kwa mabadiliko haya ya tabia nchi ambayo hata nchi kama Tanzania inatakiwa ianze kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji, jambo ambalo ni dhahiri maji ya Ziwa Viktoria yataanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ni je, nchi washirika hawa zitakubali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kwamba nchi hizo wanachama, zimekataa kutia saini makubaliano ambayo Bunge hili linayaridhia. Aidha, juhudi zote za nyuma za ushirikiano juu ya matumizi endelevu ya maji ya Mto Nile zimekuwa zikipingwa na nchi hizo kuwa lengo la ushirikiano wa nchi wanachama umeshindwa eti kuzingatia haki ya kihistoria juu ya matumizi ya maji ya Mto Nile kwa nchi za Misri na Sudani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 14 ya Mkataba inayohusu usalama wa maji, sehemu ya (b) imewekewa * na kuelezwa kuwa ufumbuzi wa kifungu hicho utapatikana kwa Tume ya Bonde kukutana ndani ya miezi sita baada ya kuanzishwa na huo ulikuwa uamuzi wa Kikao cha Baraza la Mawaziri *(Ministerial Council - COM),* kilichofanyika Kinshasa, DR Congo, mwezi Mei, 2009. Ni dhahiri kuwa, kifungu hicho kilikuwa na utata miongoni mwa Nchi Wanachama na ni nchi gani walikuwa wanapinga uwepo wa kifungu hicho?

Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kupata maelezo ya kifungu hicho ili kujiridhisha bila mashaka yoyote wakati wa uridhiwaji wa Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kurejea katika wasilisho la Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya lenye kichwa cha habari kuwa "Mto Nile: Daraja la Umoja na Ushirikiano" kama alivyolitoa katika Kongamano la Nne la Maendeleo ya Bonde la Mto Nile.

Ni ukweli na kwa Mkataba unaotakiwa kuridhiwa ni dhahiri Mto Nile utakuwa ni daraja la kuzivusha nchi wanachama katika kuwa na ushirikiano imara na mwishowe kwa mapenzi ya mpango mzima wa Mwenyezi Mungu, kuelekea kwenye umoja wa nchi hizo bila ya kujali rangi na dini za wananchi wa nchi wanachama.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa maelezo kuhusu kuridhiwa kwa Mkataba wa Mwaka 1997 *(The Law of the Non-Navigational Uses of International Watercourses)*. Mkataba unaosisitiza kuwa nchi wanachama kutumia vyanzo vya maji kwa usawa na uendelevu na pia kuweka mifumo na njia za kufuata wakati wa kupanga *schemes* ambazo zinaweza kuwa na madhara kwa watumiaji wengine. Aidha, nchi wanachama za Sudani na Misri zinasisitiza uwepo wa kifungu kipya chenye Mkataba wa Ushirikiano *(Cooperative Framework Agreement - CFA)*, kinachosema kwamba, *non to adversely affect the water security in the current users and rights of the other Nile Basin States*.

Kifungu hiki cha Itifaki mpya kimesababisha msuguano kuhusu usalama wa maji. Matumizi ya maji ya nchi zinazotumia Mto huo kwa muda mrefu yamekuwa yakidhibitiwa na Mkataba wa Kikoloni uliosainiwa kwa niaba yao na Uingereza mwaka 1929 na kupitiwa upya mwaka 1954. Nchi zingine wanachama zimepinga vikali mabadiliko ambayo yanapendekezwa kwa pamoja na Mataifa hayo ambayo yamekuwa mnufaikaji mkubwa wa maji ya Mto Nile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba mshikamano kati ya nchi za juu ambazo ni chanzo cha maji yenye Bonde la Mto Nile na mshikamano wa nchi za chini ambazo ni wanufaikaji wakubwa wa maji ya Mto Nile na kwa hiyo, kwa kuwa makundi mawili yanayokinzana ni kuweka rehani ushirikiano huu. Hivyo, ni wajibu wetu kusimamia haki katika sakata hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Msemaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Hilda Ngoye!

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia machache kuhusu Azimio hili ambalo tutalipitisha hivi punde. Kwanza kabisa, naunga mkono Makubaliano ya Msingi ya ushirikiano katika Bonde la Mto Nile. Vilevile naomba niipongeze Serikali sasa kwa kuonesha utayari wake wa kulileta Azimio hili mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka katika kipindi cha Bunge lililopita, Azimio hili ilikuwa liletwe na tulishuhudia mara mbili likiahirishwa. Leo kwa furaha kubwa ninafurahi kuona Serikali sasa imekuwa tayari kulileta Azimio hili ambalo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naelewa kwamba kwa kuwa sisi kama Tanzania ambao tulikuwa kama tunaongoza haya majadiliano, katika kufikia muafaka baina ya nchi washirika, nilitazamia kama Kamati ilivyosema kwamba sisi tungekuwa wa kwanza kuridhia Azimio hili. Tumetanguliwa na zile nchi mbili za Rwanda na Ethiopia basi na sisi kutokana na sasa kuridhia Mkataba huu, ninaomba tuendelee kuhamasisha nchi nyingine ambazo nazo pia zinatakiwa ziridhie Mkataba huu hasa nchi ya Misri ambayo kidogo ina vikwazo na vilevile nchi ya Sudani. Tukifanya hivyo basi hayo maendeleo tunayotaka tuyafanye yatakuja kwa haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoambiwa, nchi yetu inachangia kwa kiwango cha asilimia 28 cha maji ndani ya Mto Nile. Siyo kiwango kidogo ni cha kutosha, lakini inasikitisha kuambiwa kiwango cha maji tunayoyatumia ni kama asilimia moja tu. Hiki ni kiwango kidogo sana na tunastahili kupata kiwango kikubwa kwa uwiano kama Azimio hili linavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba mingi sana ya wakoloni hasa hii Mikataba inayohusu Maji Shirikishi *(Trans-boundary Waters)*, imekuwa na matatizo sana, hata huko Nyasa tunaposikia migogoro hii ni Mikataba mibovu ya Kikoloni. Sasa wenzetu wanapoing'ang'ania mikataba mibovu kama hiyo mimi siwaelewi hata kidogo, ile ilikuwa mikataba ya kuturudisha nyuma, yenye upendeleo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninapongeza nchi hizi washirika kwa kukaa chini na kufikiri vizuri. Ninaipongeza Tanzania kwa kuwa ilikuwa ikiongoza majadiliano haya. Kwa hiyo, nafikiri ni wakati mwafaka sasa tukubaliane kwa haraka hili Azimio tulipitishe na mambo mengine yaanze kufanyika kwa haraka iwezekanavyo, ambayo ni uanzishaji wa Kamisheni itakayosimamia utekelezaji wa masuala yote ambayo yameainishwa ndani ya Azimio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mahitaji yetu ya maji ya Mto Nile, hakuna ambaye atabisha, tunahitaji sana kilimo cha umwagiliaji. Ukienda Mikoa ya Kanda ya Ziwa au Kanda ya Kati, tungetaka tuyatumie yale maji ili watu tumwagilie mashamba tupate chakula cha kutosha. Unazungumzia njaa katika nchi ya Tanzania haieleweki, unapokuwa umezungukwa na maji mengi. Kwa hiyo, kilimo cha umwagiliaji endapo hili litatekelezeka na Kamisheni yetu itakayoundwa ikaweka mipango mizuri katika Sekta ya Kilimo, hakika tutafaidika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya umeme, wenzetu Misri wanafaidika sana, Uganda huko wanafaidika sana, sisi hatufaidiki na tunaihitaji miradi mingi ya umeme; lazima tuipate. Sasa hivi tunaangalia miradi ambayo tunayo ni mchache kabisa, lakini kama tungepata uwezo wa kuchimba mabwawa makubwa kama ambavyo wanafanya wenzetu huko Misri, wanahangaika sasa hivi na kuna minong'ono inasema kwamba hivi sasa kuna harakati

zinazoendelea za kuchimba mabwawa makubwa ili waweze kuzalisha umeme, mabwawa ya umwagiliaji. Sisi hatuna nafasi hiyo kwa nini? Lazima tuwe na uwiano unaofanana katika matumizi ya maji ya Mto Nile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida nyingine ni ya hifadhi ya mazingira. Kuna miradi mingi sana, hata Mataifa mbalimbali yangependa kuwekeza kwenye Miradi ya Mazingira ili kuleta uendelevu wa matumizi ya maji ya Mto Nile, uendelevu wa Ziwa Viktoria, hiyo tunaihitaji. Tukiwa na Kamisheni hiyo inayosimamia masuala haya, basi nina uhakika tutafaidika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka vilevile tuangalie masuala haya ambayo tunayazungumzia sasa hivi; kwa mfano, utekelezaji utakapoanza kutekelezwa chini ya Kamisheni, naomba kwa upande wa mazingira tukitumie chombo cha *NEMC* nacho kiwekwe katika maeneo ya kusimamia katika suala la mazingira, Kamisheni hiyo itakapoanza kufanyakazi. *Vice President Office* vilevile Mazingira iwe na wajibu mkubwa katika suala hili la mazingira. Maana tunachozungumzia hapa vilevile ni uendelevu. Hii miradi ni lazima iwe endelevu na ili iwe endelevu, maji yawe endelevu, lazima tuyahifadhi na tuyahifadhi kwa kuyatunza kwa kubuni Miradi ya Mazingira. Kwa hiyo, taasisi hizi ninazozitaja ni lazima nazo zishirikishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara nyingine ambayo itafanya kazi kubwa ni ile ambayo itafanya kazi urajibishi. Maendeleo ya Jamii nayo itapaswa iwaelimishe wananchi walielewe hili suala vizuri. Vilevile hata kwenye nchi jirani, wenzetu katika nchi zao, wajaribu kuwaelimisha wananchi umuhimu mkubwa kabisa wa kuwa na chombo hiki ambacho tunataka kukianzisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona hili niliseme kwa sababu tunahitaji maandalizi, tusiende pupa. Maandalizi ni pamoja na kuwaandaa wataalam ambao watafanya kazi katika chombo hiki tunachokiunda. Kwa hiyo, wataalam hao kama tutawaandaa kuanzia sasa watafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Azimio hili, naomba tuliridhie Wabunge wote kwa sauti kubwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa ninamwita Mheshimiwa Pauline Gekul, atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa!

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Nami nitoe mchango wangu kidogo katika Azimio ambalo lipo mbele yetu.

Awali ya yote, niunge mkono Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani. Vilevile niunge mkono mapendekezo na maoni yaliyotolewa na Kamati iliyoshughulikia Azimio hili na hususan pendekezo ambalo wamelitoa mwishoni mwa kitabu chao kwamba Mkutano wa Wakuu wa Nchi usiwe mkutano au kikao cha kuandaa sera, bali wao wapitishe. Wabunge wa nchi wanachama waweze kuangalia hizo sera vizuri na *Technical Committee* pia iweze kuangalia hizo sera vizuri, badala ya kuwaachia Wakuu wa Nchi Wanachama wakatunga sera na wao pia wakaridhia. Kwa hiyo, hili ni la msingi sana, naamini Serikali wataleta marekebisho au watakubaliana na Maoni ya Kamati, kwa sababu ni jambo la msingi na ni jambo ambalo wamelishauri vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nilikuwa najiuliza hili Azimio tunaliridhia kwa kitu gani hasa; kwa sababu nikiangalia ni suala zima la sisi kubariki maji ambayo tunaya-*own* kwa asilimia 28 katika Ziwa Victoria wenzetu kuyatumia? Wakati huo matumizi yetu msemaji aliyepita anasema ni asilimia moja, siyo asilimia moja, ni 0.1, *almost* asilimia sifuri kabisa. Kwa maana hiyo

nilikuwa najiuliza hivi unaliunga hili Azimio kwa maana ya kwamba Watanzania tunaowawakilisha katika Bunge hili wao wametosheka na maji au ni huu urafiki ambao tunasema tunauendeleza wakati Watanzania asilimia kubwa hawana maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi nilipopitia hili Azimio nimelisoma kifungu kwa kifungu, lakini kwa jicho la uwakilishi wa Wananchi. Kwamba, ni kweli sisi ni sehemu ya juu kabisa katika nchi katika kutunga na kupitia haya Maazimio na vitu kama hivyo, lakini je, kwa jicho la kizalendo wananchi wetu wamenufaika vipi?

Nilikuwa najiuliza hawa wenzetu wa Misri na Sudani ambao mwaka 1929 Waingereza waliwapa *mandate* ya kutumia maji hayo kwa asilimia kubwa kwa sababu mbalimbali, lakini wengine ambao wapo kwenye jangwa na Waziri wa Mambo ya Nje ame-*support* kwamba waendelee kupewa haya maji, hawa wanalalamika na waendelee kusimamia msimamo wao kwenye Kifungu cha 14(b) kwamba muamue msiamue sisi tunahitaji tuendelee kutumia hii *rate* ambayo tulishakuwa *provided* kipindi hicho. Hawa wanatetea matumizi yao ya asilimia 86 na kuendelea na asilimia 90 ya matumizi ya maji, lakini *providers* wa maji haya ni sisi, wakati huo sisi ambao tuna-*provide* tunatumia asilimia 0.1.

Hivi kwa jicho la uwakilishi naweza nikasimama nikaunga kwa asilimia zote kweli wakati nikijua kuna akinamama wanachota maji makorongoni, kuna wafugaji ambao mpaka leo hawana malambo ng'ombe wao wanakunywa maji ya mvua ikinyesha na kama kuna mahali wamechimba kokoto watu wakaacha yale mashimo basi maji yakikusanyika kule ndiyo wataogea, watafulia na watapikia? Sisi ambao ni wawakilishi tunaunga mkono kitu kama hiki ambacho kimeletwa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana mimi ningependa kufahamu kuna lingine zaidi ya urafiki tu na ujirani mwema kwamba na sisi zamani hizo tulikuwa ndiyo tuna-*head* sijui kitu gani, hizi nchi tulikuwa tunaunganisha, sisi ndiyo kama waanzilishi wa mambo haya; *for what use?* Asilimia 57 ya Watanzania ndiyo wana maji na wakati huo huo asilimia kama 14, 20 sasa zimepanda za Watanzania ndiyo wana umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaporidhia kitu kama hiki ni lazima uridhishwe vizuri, uelewe hivi kuna nini au tunabariki tu kwa sababu na sisi ni *fashion* basi unajua kwenye kuungana huko na sisi tuwepo tuonekane. Binafsi, kwa sababu ninafahamu chanzo cha Mto Nile kinatokana na nchi yetu pia Tanzania, Ziwa Victoria zaidi ya asilimia 24 tunamiliki yale maji, wakati huo sisi Watanzania hatujafaidi hayo maji ipasavyo, ndipo ambapo mimi naanza kupata wasiwasi juu ya Serikali, kwamba, mnapotuletea vitu kama hivi wenzetu hivi ni kwa sababu ninyi mmeshindwa kutumia haya maji?

Mara nyingi tukisema wenzetu kama vile mmepoteza uelekeo mnakuwa wakali kwa sababu gani? Kwa nini mnakuwa wakali wakati mnajua watu wenu?

Mheshimiwa Waziri wa Maji unafahamu asilimia 99 ya maswali tunayouliza asubuhi humu ndani ni kuhusu maji. Miradi mliyotuanzishia ya *World Bank* sijui kitu gani imekwama. Hivi tunavyoongea Mheshimiwa Waziri wa Maji na ukaze macho uniangalie, Wakandarasi wako hawajalipwa, Miradi ya Maji imesimama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul ongea na Kiti.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sawa.

Wakandarasi hawajalipwa, hawana pesa, Miradi ya Maji imesimama. Ukienda Babati, Mheshimiwa Naibu Waziri umetembelea, umeona vile visima vyote ambavyo mmechimba,

kingine mpaka milioni 800 hakina maji, Wakandarasi hawalipwi, wananchi hawana maji. Halafu Wabunge tunakuja hapa tunakaa siku ya leo tunajadili hiki kitu kwamba wengine huko Misri wapewe, Ethiopia wapewe na wengine ambao hata hawajaridhia Kifungu cha 14(b), hawajasaini huu Mkataba, hawajaridhia huu Mkataba, hivi sisi tuna haraka gani? Tunakimbilia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine tunapoleta Serikali labda ina mambo yake ambayo yako *hidden* kabisa hawasemi waziwazi. Tungekuwa tunasema waziwazi mimi ningeuliza hivi hawa tunaowa-*provide* maji wanatuchangia kitu gani? Tunapata nini? Hawa wanaotumia haya maji ya Mto Nile kwa asilimia 90 na sisi ndiyo tuna-*own* Ziwa na hayo maji mengi yapo kwetu wanatulipa nini mpaka turidhie, watatusaidia kutufikishia maji kwa Wananchi wetu? Msipoyajibu haya na msipokuwa wazi kama Serikali, msitegemee Wabunge wataendelea kuwa *rubber stamp* kila siku watapitisha mambo yenu mnayotaka kama Serikali kwa sababu mnataka kuyapitisha.

Mwisho, kwa sababu ya muda ni ile tozo. Wewe pata picha kwanza maji ya kwetu, lakini bado tunatoa milioni 253 kila mwaka kama ada! Ninasikitika tu picha ya nchi yetu siyo nzuri sana hasa kwenye *Association* kama hizi au kwenye Jumuiya kama hizi.

Tumeungana na nchi za Maziwa Makuu, hatulipi ada, hata hii mliyopitisha hapa dola laki moja na elfu thelathini na saba hamtalipa, ni kama fasheni tu tutaweka. Vilevile *rationale* ya kulipa milioni 250 huko ambako tuna-*provide* sisi maji halafu tukalipe na milioni 250 wakati watu wetu hawana maji mimi ndiyo sielewi hapo sasa! Kama ni hiyo *equation* kwenye akili yangu ndiyo hai-*balance* kabisa, kwa sababu kwanza maji tumeshawapa sawa na hiyo ada milioni 250 Watanzania hawawaelewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umeisha, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kabla sijamwita Mheshimiwa David Mwakyusa, naomba nitoe tangazo hili; tangazo la Kikao cha Kamati ya Uongozi. Mkurugenzi Msaidizi wa Shughuli za Bunge, anaomba niwatangazie Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi kuwa kutakuwa na Kikao leo Alhamisi saa 12.30 jioni katika Ukumbi wa Spika, Wajumbe wote hudhurieni bila kukosa.

Mheshimiwa Profesa Mwakyusa, atafuatiwa na Mheshimiwa Masoud!

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nichangie machache katika itifaki ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama ili kuunga mkono hoja. Pia ningesema kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati iliyochambua Muswada huu na nakubaliana na yote ambayo tuliyafanyia kazi na kuyaleta mbele ya Bunge kwa niaba ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1961 tarehe 9 Disemba tulipata uhuru. Siku nane kabla ya siku hiyo, Mwalimu Nyerere wakati huo bado hajakabidhiwa nchi, alitamka kwamba nchi yetu itakapopata uhuru aliita Tanganyika; Tanganyika itakapopata uhuru haitarithi Mikataba yoyote ambayo tutaona haina manufaa kwetu au haina tija kwetu. Hiyo imeitwa ni *The Nyerere Doctrine* na imesaidia nchi nyingi sana ambazo zilianza kupata uhuru wakati ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Mikataba tunayozungumza ni ile ambayo haina tija kwa nchi. Kama tulivyosema kwenye ripoti yetu, mwaka 1929 na baadaye mwaka 1959, Uingereza ikiwa ndiyo mtawala wetu kikoloni ikaingia mkataba na Sudani na Misri na tumepewa takwimu hapo ambazo mwisho wa siku ni kwamba 87% ya maji yote ya Mto Nile ilikuwa yatumike na nchi

hizi mbili. Tumeeleza kwamba 10% ya maji yanapotea kwa njia ya mvuke. Kwa hiyo, nchi nyingine hizi za *upstream* zilibakiwa na 3% na sisi katika kuchangia 28% tunabaki na 0.1%. Kwa vyovyote vile hii haikubaliki na nashukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani amekubaliana na sisi na nashukuru Mama Gekul pia amekubaliana na sisi. Alitoa maangalizo ambayo tutayafanyia kazi lakini kiujumla alitaka kusema kwamba anaunga mkono hoja lakini muda ukawa umekwisha. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika mchakato mzima mpaka kutufikisha hapa tulipo katika ngazi za wataalam, lakini katika *Ministerial Committee*. Hapa nitambue mchango wa Profesa Mwandosya ambaye alikuwa Mwenyekiti wa mchakato mzima huu. Kwa sisi ambao tulikuwa tumeshika bango toka mwanzo, nchi nyingine kama tulivyosema, ni nchi mbili tu ambazo mpaka sasa zimeridhia Mkataba huu, nchi zilizobaki tunaamini wanaangalia na kuchungulia na kujiuliza Tanzania vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa swali aliloluliza Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwamba, je, tuna uhakika gani kwamba nchi hizi zitakubali kusaini? Tuna imani kwamba sisi tukisaini nchi nyingine zote zitafuata na zitasaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ripoti yetu pia tumezungumza kwamba Sudani sasa hivi haina ukali wa msimamo kama ilivyokuwa mwanzo. Moja ni kwamba Sudani sasa zimekuwa nchi mbili na *South Sudan* ni moja ya nchi katika hii *framework* tunayoizungumzia, wao hawana matatizo kabisa. Kamati yetu ilikwenda kutembelea nchi ya Sudan na kule karibu kila kitu ni Nile, umwagiliaji, kilimo na kadhalika. Tulikwenda kutembelea bwawa ambalo wanatengeneza umeme na umwagiliaji linaitwa Meroe, ni moja ya mabwawa makubwa hapa duniani. Tukawauliza kama walipata kibali kutoka Misri maana Misri ndiyo bado wana msimamo mkali, wakasema hapana na wanatarajia kujenga mabwawa mengine saba. Kwa hiyo, tuna imani kwamba haitachukua muda Sudani pia ikasaini na atabaki mtu mmoja tu ambaye ni *Egypt,* mategemeo yetu ni kwamba mambo yatakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumetoa angalizo na kutoa ushauri ambao nakubaliana nao. Itifaki hii ikipitishwa tutakapounda hii Kamisheni sisi pia tujitayarishe kama nchi kwa kila hali kwa maana ya rasilimali watu ambao wataweza ku-*compete* na wenzetu na sisi tuweze kuwa na usawa katika kuendesha hii Kamisheni. Sisi katika hii Itifaki hatusemi kwamba wenzetu walio *downstream* wasipate maji, hapana! Ni binadamu wenzetu, hawana vyanzo vingine vya maji lakini tunachosema kuwe na usawa na sisi tufaidike na maji ambayo mazingira yako chini yetu, tunaangalia mazingira ili vyanzo visikauke, lakini isiwe sisi tu tuwe watu wa kutengeneza maji halafu mtumiaji awe mwingine na tukitaka kuyatumia tuombe ruksa kutoka kwao, hii tunasema hapana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakumbuka kwamba miaka kadhaa iliyopita tulipothubutu na kuanza kuchukua maji tuyapeleke Tabora tulinuniwa sana na wenzetu wa *downstream* lakini tukapiga moyo konde na tunaendelea. Haya ndiyo tunasema kwamba tusikaushe Nile lakini na sisi tufaidike na hayo maji na katika kutunza vyanzo vya Mto Nile isiwe sisi tu ndiyo tunatumia pesa zetu na rasilimali, ni lazima bonde zima mpaka kule Misri waweze kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa, sina uhakika kwamba maji yanafika Alexandria yanamwagika katika Bahari ya Mediteranean. Tunaambiwa kwamba wenzetu wanajenga bomba la kupita chini ya Mediteranean kwenda Sinai ambayo iko upande wa pili, ili watumie hayo maji kwa umwagiliaji. Haya ndiyo tunasema kwamba siyo haki kwamba sisi tunahitaji maji halafu wenzetu wanakwenda kutumia katika sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja na nasema ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataala* kunijalia uzima na afya njema nikisimama kuchangia Azimio lililo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusema kwamba tumechelewa kuridhia lakini kumbe kulikuwa kuna mambo mengi ambayo yalitupasa tuangalie kwa umakini mkubwa kabla ya kuweza kufikia hii *ratification.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mtoa Hoja alivyoeleza, Tanzania sisi katika vyanzo vyetu tunachangia 28% lakini matumizi yake ni 0.1% lakini wakati huo huo Misri wanatumia maji yale kwa zaidi ya 80%. Hapa kidogo mimi napata mashaka, Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho atuambie sasa sisi na awaridhishe Watanzania, katika urefu wa Mto huu Nile ambao una urefu wa kilometa 6,853 kuanzia chanzo chake kwenye Ziwa Victoria mpaka *pouring point* Misri kabisa kule, je, sisi tuna kilometa ngapi za kwetu? La kwanza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, napata mashaka kwamba wenzetu Misri kwa mujibu wa Mkataba wa mwaka 1929 na 1959 Waingereza walitoa fursa na kuipa nguvu Misri kutumia maji mengi sana ya Mto Nile. Mheshimiwa Waziri sisi Tanzania leo tukiridhia Azimio hili na Mkataba mpya ukaanza kutekelezwa na Mkataba wa 1929 na 1959 unaompa nguvu Misri ambapo moja ya masharti na fursa waliyopewa kuanzia Januari 20 hadi tarehe 15 Julai kipindi cha ukame, maji ya Mto Nile ni mali ya Misri, ukiangalia Mkataba wa 1929, tunao tumeangalia, ndivyo unavyosema hali itakuwaje? Misri pia ina haki ya kuangalia mtiririko kutoka kwenye chanzo chochote cha maji kwenye mto sehemu iliyopitia, hayo ni kwa mujibu wa Mkataba wa 1929 na 1959. Misri ina uwezo wa kuzuia maji kwenye mradi wowote katika nchi ulizopita na ndiyo maana napata wasiwasi. Wakati huu Ethiopia wanataka kujenga bwawa kubwa la dola bilioni 4.2 tayari kuna mgogoro umeanza. Je, Mheshimiwa Waziri alipotuambia kwamba, sisi tukiridhia Azimio hili basi utekelezaji wake utaenda vizuri, hatuoni bado mgogoro upo kwa mtindo huo? Napata mashaka sana Mheshimiwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi sina pingamizi na kuridhia lakini nina wasiwasi kwamba kumbe Misri ule Mkataba wa Kikoloni wa 1929 na 1959 bado wanao na wanaona kwamba una nguvu zaidi kulikoni hiki kinachokwenda. Sasa Mheshimiwa Waziri, hili mimi naona kidogo lina matatizo. Vitisho hivi ambavyo wanatoa wenzetu vimekuwa ni vikubwa na mashaka ambayo yanaweza kutokea basi yanaweza kusababisha nchi yetu katika maangamizi au matatizo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kusema ni kwamba katika hali isiyo ya kawaida ukiangalia ramani hii ambayo wenzetu wa Kamati walipewa, kuanzia kwenye chanzo cha mto huu kwenye Ziwa Victoria kuna mabwawa makubwa katika nchi ya Misri yamejengwa na Sudani wamejenga. Mheshimiwa Waziri kuna *Aswan High Dam - Misri*, *Sennar Dam – Sudan*, *Jebel Aulia Dam – Sudan* na maeneo mengine. Sasa ukiangalia baina ya *Blue Nile* iliyokwenda Ethiopia, ukiangalia *White Nile* ambayo imekuja kwetu kuna *Gezira Irrigation Scheme* ambayo ilikuwa inatumia maji kwa wingi kupita kiasi. Ukija chini zaidi na kuangalia kutoka *upstream* kuja *downstream,* Sudani kuna *Bahr al Ghazal* na *Bahr al Jabal*. Sasa wenzetu wanatumia maji kwa kiwango kikubwa na nashukuru sana Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, nadhani alialikwa hivi karibuni huko Nairobi na kuna *paper* katoa, nikupongeze sana. Ilikuwa ni nzuri lakini ilikuwa na maangalizo mengi na mwisho alinukuu Aya ya *Quran, Surat*

*Al-Anbiyaa:* 21 - 30 ambayo ilikuwa inaeleza kwa waziwazi kwamba, tumejaaliwa uhai wa kila kitu kutokana na maji. Hiyo ni *paper* ya Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi tunaokwenda nao, tunataka turidhie hili lakini, je, wenzetu hawa kama hawakuridhia sasa, Misri kama haikuridhia na sifikirii kama atakubali kujitia kitanzi yeye mweyewe, Mkataba hata ukimbana bado yeye ana nguvu. Mimi naona huko tunakokwenda 2/3 ipatikane lakini bado Misri kama Misri ikiwa tu leo Ethiopia anajenga bwawa na tayari vitisho ni vingi, hawafahamiani kuna matatizo kama haya, seuze mambo mengine? Sasa basi, kwa kuwa sisi tunachangia 28% na tunatumia 0.1, mimi nashauri, Mheshimiwa Waziri ongeza mabomba ya maji Watanzania hawana maji, tafuteni fedha. Mnasema nchi bado inakopesheka, kila siku mnakuwa na wimbo wenu huo, nchi bado inakopesheka basi tafuteni hiyo mikopo wananchi wa Tanzania baadhi ya Mikoa wanachangia maji baina ya wanyama na binadamu. Tafuteni fedha mtoe mabomba kwenye Ziwa Victoria mpeleke katika maeneo mbalimbali watu wapate maji, huo ndio ushauri wangu. Kama hili mkilitekeleza basi, kuna tija kubwa kwa Watanzania kuamini kwamba Mkataba huu hauna kiini macho, hauna kizungumkuti, siyo wa kuridhisha mabwana na siyo ule wa shinikizo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba sana Mheshimiwa Waziri lakini haangalii kama alivyosema Mheshimiwa Gekul, anasikiliza mambo mengine, yaleyale aliyoyasema Mheshimiwa Gekul. Mheshimiwa Waziri nataka uangalie utaratibu wa kutafuta mabomba na kuyaunganisha kupeleka maeneo ambayo hayana maji. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo ambayo nimeyaeleza, naomba Mheshimiwa Waziri atuambie sasa Tanzania ina mpango gani wa kujenga mabwawa kama nchi nyingine? Atuambie katika maeneo yote ya vyanzo vyetu, ana mpango gani wa kujenga mabwawa kama wenzetu wanavyojenga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu tuseme kwamba ninyi mnataka haya maji yatumike kwa usawa, haki sawa kwa wote mnaiweza kweli nyie? Kwa sababu nyie mnataka tutumie maji haya kwa usawa na Misri wapate usawa wao, Mikataba hii ya Kikoloni inawalinda kwa misingi ya haki sawa kwa wote, asiyependa haki afanye nini, aelimishwe, sasa wengine hawaelimishiki tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachosema ni kwamba katika mabwawa hayo ambayo yanazalisha umeme, mambo ya uvuvi, mambo ya kilimo, bado Tanzania haijafikiria, mimi naona kama kuna shinikizo fulani hivi sasa juu ya Mkataba huu. Twende tu na sisi tuingie kuwe na hivi na vile lakini bado hamna uwezo wa kuibana Misri! Tunakwenda kuridhia jambo hili; jambo hili mimi nilisema limechelewa, halikuchelewa, kumbe hadi sasa kuna wasiwasi mkubwa kwamba Misri itakuwa na ubavu wa kufanya inavyofanya kama inavyoitishia nchi ya Ethiopia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, naomba nimalizie hapo, nimuombe Mheshimiwa Waziri atafute fedha kwa ajili ya kutoa maji kwenye Ziwa Victoria ili maeneo ambayo hayana maji katika Majimbo au Mikoa mbalimbali hasa yale maeneo ambayo wanachangia maji baina ya wanyama na binadamu basi waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote niunge mkono hoja ya Azimio hili. Azimio hili ni la muhimu kwa sababu ni kitu ambacho

kimechambuliwa na kimeonekana sasa kinaweza kikafanyika kuliko ilivyokuwa huko mwanzo kutokana na Mikataba ambayo iliwekwa na Wazungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Azimio hili sasa Tanzania itakuwa mshirika na ambaye anaweza akatoa maamuzi juu ya suala la Mto Nile. Angalizo ambalo napenda kuishauri Serikali, ni vyema sasa ikaangalia umuhimu wa kuyatumia haya maji na kuangalia misingi ambayo itawasaidia Watanzania hasa katika kuboresha shughuli za utunzaji wa mazingira. Kwenye eneo hili bado hatujapaangalia vizuri sana. Ni vyema nchi ambazo zitatumia maji kama nchi za Sudan, Misri, wakachangia kwa kiwango kikubwa kuboresha mazingira kwenye maeneo ambako ni vyanzo vya Mto Nile ili na sisi kama Watanzania tuweze kuneemeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kutunza vyanzo vya maji hata ule mto ambao tunauona ni endelevu baadaye utatoweka lakini sisi ambao tunatunza maji haya hatutakuwa na faida ya aina yoyote kama hajawa na mipango endelevu ya kutunza hifadhi ya mazingira. Kwa hiyo, naomba sana Serikali tunapoingia kwenye Mikataba hii tuangalie ni jinsi gani tutawasaidia hawa Watanzania wanaotunza vyanzo vya maji wananufaika vipi kwa kuwajengea uwezo ili waweze kuwa na mipango endelevu ya kutunza mazingira. Ni vyema nchi hizi washirika zikachangia kuhakikisha kwenye utunzaji wa mazingira wanapewa fedha ili ziweze kulinda mazingira na kuwapa faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili mimi nasisitiza ni vyema Serikali tunapojiingiza sasa kwenye Mkataba huu Maalum, tuangalie ni jinsi gani Mataifa haya ya Sudani na Misri yasije yakapora mazingira kwa kuwaona Watanzania hawatumii maji kama ambavyo na sisi tunatarajia. Ni vyema tukaangalia umuhimu sasa wa kutengeneza mipango ya kuwasaidia Watanzania hasa wa Mikoa ambayo imezungukwa na Ziwa Victoria, ianze kuwanufaisha mara moja. Kwa jitihada ambazo zimefanywa sasa na Serikali za kuchukua maji ya Victoria kuyaleta katika Mkoa wa Shinyanga, ni vyema sasa Serikali ikawa na mipango endelevu pamoja na jitihada ambazo zinafanywa na Serikali kupeleka maji Mkoa wa Tabora lakini ni vyema maji haya tukawa tunafikiria zaidi kuyapeleka mpaka Mkoa wa Singida na hatimaye kuyaleta mji wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na mipango endelevu ya kuangalia Watanzania kuliko kutunza maji ambayo yatawanufaisha zaidi wenzetu na wakati huo huo wao hawataki kutuchangia kwa ajili ya hifadhi ya mazingira. Katika hili lazima tuwe na mipango endelevu. Wenzetu wameyatumia vizuri sana maji haya, tumeenda Sudani tumeangalia jinsi walivyotengeneza mabwawa makubwa, jinsi wanavyotumia shughuli za umwagiliaji katika kuendesha nchi, kimsingi nchi ya Sudani, nchi ya Misri zinategemea sana Mto Nile.

Kwa hiyo na sisi ni vyema tukawa na mipango itakayowasaidia sana Watanzania kwa ajili ya kuboresha shughuli za kilimo cha umwagiliaji lakini wakati huohuo tuwe na mipango endelevu ya kuhakikisha Mikoa ambayo inazunguka Ziwa Victoria kwa maana ya Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza na Mikoa kwa ujumla ile ya Kanda ya Ziwa ili waweze kuneemeka kwa shughuli za kilimo na uhakika wa kupata maji. Itakuwa ni jambo la ajabu sana sisi tunatunza maji wanufaikaji wakubwa sana wanakuwa watu wa nchi za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja na natoa tu ushauri kwa Serikali tusiingie mikataba ambayo itawaumiza wananchi wa Tanzania, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Wachangiaji walioomba ni wengi lakini kwa sababu ya muda, naomba tumuite sasa Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya dakika kumi, zimepungua wako wengi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, ASIYE NA WIZARA MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa

kuliwasilisha kwa ufasaha sana Azimio hili. Vilevile nimpongeze Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa kuwasilisha aliyowasilisha. Pamoja na makandokando aliyoyasema lakini ameunga mkono, kwa hiyo, na mimi nasema naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, mchango wangu utakuwa kwa ufupi tu kwenye eneo muhimu sana tusije tukalisahau kwenye historia nalo ni mchango wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika kutufikisha hapa tulipo. Huo ndiyo mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanzia wapi? Imezungumzwa makubaliano kati ya Uingereza na Misri ya tarehe 7 Mei, 1929, hili amelieleza vizuri Mheshimiwa Waziri. Katika makubaliano hayo haikuruhusiwa kujenga miundombinu yoyote kwa ajili ya kilimo au umwagiliaji, uzalishaji wa umeme bila ruksa ya Misri. Sasa Uingereza ilisema hayo vilevile yalikuwa yanatuhusu sisi. Misri vilevile iliruhusiwa bila kipingamizi kufanya utafiti, kuanzisha vituo vya kupata *data* za kihaidrojia na kuweka wataalam katika maeneo yetu bila kipingamizi huku Afrika Mashariki na Sudan vilevile. Sasa haya mambo kwa kweli hayakuwa ya sahihi na hatukuyakubali. Vilevile kuna makubaliano ambayo Mheshimiwa Waziri ameyafanunua vizuri sana ya Sudan na Misri ambayo ni ya tarehe 12 Desemba, 1959 ambapo Misri na Sudan zilikubaliana kuhusu matumizi kati yao karibu ya maji yote ya Mto Nile. Hili hasa ndiyo chimbuko la mazungumzo haya yaliyopelekea kufikia hapa tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mwalimu anahusikaje? Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa ameligusia. Mimi nitaliendeleza pale alipoachia. Tarehe 30 Novemba, 1961 akilihutubia Bunge la Tanganyika siku chache kabla ya uhuru, Mwalimu alisema kwamba Serikali ya Tanganyika huru imekataa pendekezo la Uingereza kwamba irithi mikataba yote ambayo Uingereza ilikuwa imeingia kwa niaba yake ikiwa ni pamoja na Mikataba kuhusu Mto Nile.

Sasa hapo ndiyo utaona jeuri ya Mwalimu, jeuri ya Tanzania au jeuri ya Mtanzania ambayo kwa kweli inabidi tuifufue, ni heshima kubwa sana. Hilo sasa ndiyo chimbuko la falsafa ya Mwalimu inayoitwa *Nyerere Doctrine on State Succession.* Hii falsafa huko nje ya Tanzania inajulikana sana. Katika Vyuo Vikuu vingi ni sehemu ya mafunzo ya rasilimali za maji shirikishi na watu wamepata shahada, wameandika vitabu kuhusu falsafa ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kuhusu hili suala, isipokuwa falsafa hii haifahamiki sana nchini wala hatuizungumzi sana. Leo kwa kuridhia hili Azimio, tunamuenzi Mwalimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipi tunamuenzi? Baada tu ya kuelezea hayo katika Bunge kukataa kurithishwa Mikataba ya Kikoloni, Mwalimu alipeleka barua kwa Serikali ya Misri, Sudani na Uingereza na nukuu lakini tafsiri hii ya Kiswahili ni ya kwangu alisema ifuatavyo:-

"Serikali ya Tanganyika kwa kutambua umuhimu mkubwa wa maji ya Ziwa Victoria kwa Tanganyika na eneo la Bonde la Ziwa hilo kwa mahitaji ya baadaye na maslahi ya watu wa Tanganyika, imetafakari kwa undani hali inayojitokeza kutokana na ujio wa Tanganyika kama nchi huru na inayojitegemea kuhusiana na makubaliano ya mwaka 1929 kuhusu maji ya Mto Nile. Makubaliano hayo yako katika nyaraka za Serikali za Misri na Uingereza."

Mheshimiwa Mwenyekiti, akaendelea kusema:-

"Kutokana na tafakuri hii, Serikali ya Tanganyika imefikia uamuzi kwamba vipengele vya Mkataba vinavyohusisha nchi zilizo chini ya utawala wa Uingereza haviifungi Tanganyika huru. Hata hivyo, kwa kuzingatia umuhimu wa maji ya Mto Nile ambayo chanzo chake ni Ziwa Victoria kwa watu walio katika Bonde la Mto Nile, Serikali ya Tanganyika iko tayari kuwa na mazungumzo na Serikali nyingine, kwa wakati muafaka, kwa madhumuni ya kuandaa na

kukubaliana kuhusu njia za kudhibiti na kugawana maji hayo kwa njia ya haki na uwiano kwa nchi zote za bonde na kwa faida ya watu wake." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu aliyazungumza haya mwaka 1962 na huu ni mwaka 2015. Imepita miaka hamsini na tatu. Haya ni matokeo ya ndoto yake na ni matokeo ya mwongozo wake. Yote haya tuliyoyazungumza sisi ambao tumehusika katika majadiliano haya, tuliongozwa na falsafa ya Mwalimu. Nimeona nilizungumze hili na kulitilia mkazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie mchango wa Watanzania wengine katika hili. Kuna Mtanzania mmoja, Marehemu Mrisho Kivugo, Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, yeye alikuwa mmoja wa Wakurugenzi wa kwanza wa *TECCONILE* ambayo ilikuwa ni mwendelezo wa mazungumzo na ushirikiano katika ngazi ya kiufundi. Mtanzania mwingine ni aliyekuwa Mkurugenzi mwanzilishi wa *Nile Basin Initiative,* Ndugu Miraji Msuya ambaye alifanya kazi nzuri sana, lazima tumtambue. Vilevile tutambue kwamba *NBI* ambayo ni mfumo wa sasa wa mpito wa ushirikiano katika Bonde la Nile ulianzishwa Dar es Salaam. Kwa hiyo, Tanzania ina mchango mkubwa katika suala hili siyo katika majadiliano tu, lakini pia katika kuanzisha vyombo vya usimamizi wa Mto Nile. Kwa kweli tumechelewa. Tungekuwa wa kwanza katika kuridhia Makubaliano haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu lazima nitaje baadhi ya Maofisa waliofanikisha majadiliano zaidi ya miaka kumi na kwa ajili rekodi na *Hansard,* wako watu kama akina Washington Mutayoba, Michael Jeremiah Kamba, Lister Kongola, Hamza Sadick, Erick Mugurusi, Sylvester Matemu, Miraji Msuya, Mrisho Kivugo, Nerei Msimbira, Marehemu Flugence Kazaura, Marehemu Rwegalulira, Marehemu Mambali Mbogo Futakamba, Ndugu Sayi pamoja na wengine wengi. Mawaziri waliohusika na kusimamia majadiliano ni pamoja na Mzee Al-Noor Kassum, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete wakati akiwa Waziri wa Maji lakini vilevile akiwa Waziri wa Mambo ya Nje. Amehusika sana katika kuendeleza mazungumzo ya ushirikiano huu na sasa anasimamia kama Rais wa nchi katika kupitisha hili Azimio. Wengine ni Mheshimiwa Pius Ng'wandu, Mheshimiwa Juma Nkangaa, Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Antony Diallo, Mheshimiwa Steven Wassira, Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, Mheshimiwa Lwenge, Mheshimiwa Christopher Chiza, Mheshimiwa Jaji Frederick Werema na Mheshimiwa Jumanne Maghembe ambaye sasa ndiye analiwasilisha Azimio hili. Kwa hiyo, wote hawa ndiyo waliotufikisha hapa, tunawashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Ushirikiano wa *CFA* umejikita katika mambo muhimu mawili, moja ni matumizi kwa njia ya haki na uwiano na kwa umakini yaani *equitable and reasonable utilization.* Vilevile kutumia maji kwa njia ambayo haiathiri kwa viwango vikubwa nchi nyingine, *not to cause significant harm.* Hii ni dhana ambayo tangu zamani za Kilatini ipo kwamba usitumie mali yako kwa njia ambayo unaweza kuwadhuru wengine, wanasema *ne res tuas quasi aliena nocet.* Pamoja na kwamba sisi tunahitaji maji lakini hatuwezi kuyatumia maji hovyo hovyo kwa njia ambayo tunaweza tukawadhuru Sudan na Misri. Huu ni msingi muhimu sana na kwa hiyo wenzetu wa Sudani na Misri wasihofu ila watambue sisi vilevile tuna haki kutumia maji yaliyo katika nchi yetu bila kuwaomba ruksa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sudani na Misri zitalindwa sana katika Mkataba huu kwa sababu nchi lazima zitoe taarifa za mipango ya matumizi ya maji. Kwa hiyo, watajua tu tunafanya nini. Miradi yote lazima ifanyiwe Tathmini ya Athari kwa Mazingira *(Environmental Impact Assessment).* Nchi yoyote inaweza kuhitaji taarifa yoyote yanayohusu *Nile* na lazima taarifa hizo zipatikane. Halafu nchi kama nilivyosema zisiathiri nchi nyingine. Fidia itatolewa pale ambapo matumizi katika nchi moja yanaathiri matumizi katika nchi nyingine. Kuna mfumo wa usuluhishi na kama alivyosema Mheshimiwa Waziri vilevile tumekubaliana kwamba katika miezi

sita ya kuanzisha Kamisheni ya Bonde la Mto Nile basi tutajadiliana kufikia muafaka wa vifungu ambavyo mpaka sasa hatujakubaliana na ni kifungu kimoja tu ambacho ni kifungu cha 14(b).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke sasa kwamba mambo yanakwenda vizuri. Sudani nadhani wanatuelewa na huenda wakaingia katika Mkataba huu na kwamba Misri, Sudani na Ethiopia tarehe 21 mwezi Machi wamekubaliana kuhusu ujenzi wa bwawa kubwa, bwawa muhimu la *GERD* huko Ethiopia la megawati 6000. Sasa maadam Misri imekaa na Ethiopia na Sudani bila shaka itakaa na sisi sote ili tuweze kukamilisha Mkataba huu na wao wakawa sehemu ya Mkataba huu. Kwa hiyo, hizi ni dalili njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ni hayo ambayo nilitaka kuyasema kwa muda huu ambao umenipa. Nilikuwa nayo mengi lakini mengi nitayatoa katika mihadhara kama vile kwenye Vyuo Vikuu au sehemu nyingine. Kwa leo nimeona nisisitize kwamba kwa kuridhia Mkataba huu tunamuenzi Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Mwandosya. Sasa namwita Mheshimiwa Stephen Wasira kwa dakika kumi.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa dakika kumi ili na mimi niongeze sauti yangu katika suala hili. Nimeamua kutoa mchango wangu hapa kwa sababu tatu. Kwanza, mwaka 2006 nikiwa Waziri wa Maji nilishiriki katika mjadala na mashauriano kuhusiana na jambo hili. Pili, mimi ni Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika na maji ndiyo pembejeo kuu ya sekta ya kilimo. Tatu, ninawakilisha katika Bunge hili watu wanaoishi karibu sana na Ziwa Victoria ambalo kwa kweli haki zao lazima zilindwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili limechukua muda mrefu sana kujadiliwa na limechukua muda mrefu kwa sababu ya wenzetu wa Misri, nchi nyingine zote zinazozunguka Ziwa Victoria ambazo ndizo sehemu kubwa ya *Nile Basin* zilikwishakubaliana siku nyingi sana kwamba tuwe na Mkataba maana Nile yenyewe msingi wake na chanzo chake ni Ziwa victoria lakini wenzetu wa Misri na Sudan wakati wote walishikilia kwamba Mkataba ambao walisaini na Waingereza mwaka 1929 halafu ukafanyiwa marekebisho mwaka 1959 kwamba ufanywe ndiyo uwe msingi wa makubaliano juu ya matumizi ya maji ya Nile na kwamba nchi nyingine zote ambako chanzo cha Nile kinaanzia au zinazozunguka Ziwa Victoria lazima zipate kibali cha Misri ili kutumia maji ya Ziwa Victoria, nadhani ndiyo msingi wa majadiliano.

Sasa nadhani ameieleza vizuri Mheshimiwa Profesa Mwandosya kwamba Mwalimu alichosema ni kwamba Waingereza walipokuwa wanajadiliana na Misri sisi hatukuwepo maana hatukuwa nchi. Kwa hiyo, kwa kweli makubaliano yale yalikuwa kati ya Serikali ya Uingereza na Serikali ya Misri na kuwapa *veto* kwa Misri kuamua na kutumia sehemu kubwa ya maji na kwamba sisi tukitaka kuyatumia lazima tupate kibali cha Misri. Mimi nawakilisha watu wa Bunda na maji ya Ziwa Victoria yako palepale kwamba sisi tukitaka kuyatumia, nataka Watanzania waelewe tukitaka kuyatumia au kwa umwagiliaji au kwa namna yoyote nyingine lazima Tanzania ikapate kibali cha Misri. Mimi nauliza huo uhuru tuliodai uko wapi kwamba unaweza kushindwa kutumia maji unayoishi nayo hapo mpaka ukapate kibali cha nchi nyingine tena iko maili nyingi sana kutoka pale, hiyo hoja moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya wenzetu wa Misri wanasema sisi tuna maji mengi na kwa sababu hiyo kuwanyima maji au kutaka tugawane sawa basi ni kuwapa matatizo. Hata hivyo, mtu yeyote anayejua Mikoa inayozunguka Ziwa Victoria na ambaye anataka kwenda kushuhudia hivi sasa kiwango cha ukame kilichopo katika eneo lile ni kikubwa kiasi kwamba

hata mpunga sasa unakauka sasa huwezi kutumia maji ya Ziwa Victoria pale mpaka Serikali yetu iende Misri kuomba, hili ndiyo jambo linaloondolewa na Mkataba huu. Hilo ndiyo jambo linalorekebishwa na Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wale wanaosema tena Mkataba huu una jambo lingine limejificha jambo gani? Jambo lililopo katika Mkataba huu ni kuimarisha uhuru wa nchi yetu kushirikiana na nchi nyingine ili matumizi ya maji ya Ziwa Victoria na Mto Nile yaweze kutumika kwa haki kwa nchi zote. Sisi tunajua kwamba maji hayawezi kuwa ya nchi moja na maji hayajui mpaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tulipoenda kule Kusini kwenye mazishi ya Kapteni Komba, tulishuhudia mito inayoingiza maji katika Ziwa Nyasa. Kwa kweli Ziwa Nyasa linapata maji kutoka katika mito zaidi ya sita ambayo inatiririka na kuingiza maji katika Ziwa Nyasa. Sasa huwezi ukasema maji ya Ziwa Nyasa ni ya nchi moja, hayawezi kuwa ya nchi moja kama ambavyo ya Ziwa Victoria ahayawezi kuwa ya nchi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachosema kwenye Mkataba huu ni kwamba tuwe na utaratibu na chombo ambacho kitakuwa kinasimamia ugawaji wa haki wa maji kati ya nchi hizi. Wala kwa kusema hivi hatuwaambii wenzetu wa Misri msitumie maji hata kidogo, hatuwezi na hatuna haki lakini na wao vilevile kuwa na haki ya kutuzuia sisi kutumia maji ambayo tunaishi nayo, nayo si haki. Ndiyo maana *Article 4* inazungumza juu ya *equitable and reasonable utilization* kwamba tunakaa, tuna chombo cha kitaalam ambacho kinaamua kiwango gani cha maji kinatumika wapi na nchi yoyote inapotaka kuanzisha mradi mkubwa basi chombo hicho kinasema hapa haki ya nchi zote inaridhiwa, hivi ndivyo Mkataba unavyosema. Wenzetu wa Misri wanakataa kuridhia Mkataba huu kwa sababu moja tu wanataka Mkataba wa mwaka 1929 ambao unawapa haki ya kuamua matumizi na kwamba matumizi ya maji karibu yote yawe yanakwenda kwa ajili yao, nasema hii si haki.

Kwa hiyo, kama Waziri wa Kilimo, lazima tukubali jambo hili turidhie ili tunapohitaji maji haya kwa ajili umwagiliaji tumwagilie lakini bila kuathiri haki ya watumiaji wengine wa maji. Nadhani hili jambo lingekuwa jambo rahisi kulikubali kwa sababu haiwezekani sisi uhuru wetu tuukabidhi kwa watu wengine juu ya matumizi ya jambo hili lakini vilevile hatutaki mgogoro na nchi yoyote lakini haki zetu zilindwe bila kuathiri haki za nchi nyingine na nilidhani jambo hili ni *straight forward*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiongezea yale aliyoyasema Mheshimiwa Profesa Mwandosya, hii kitu inaitwa *Nyerere Doctrine of State Succession* ipo kwenye Umoja wa Kimataifa na Mwalimu aliipeleka *UN* ndiyo maana dunia nzima inaizungumza kwamba Wakoloni wanaweza kuzungumza kwa niaba yenu wakati ninyi siyo nchi, sisi hatukuwa raia wa Tanganyika, kwa sababu hapakuwa na Tanganyika huru. Kwa hiyo, Waingereza walijadiliana na marafiki zao sasa hatuwezi kuishi dunia hii na maisha yetu yote kwa kuzingatia Mkataba ambao Waingereza walifanya urafiki na wengine. Tuko tayari kuzungumza na Misri tukubaliane na wao waridhie ili tuwe na chombo ambacho kinatoa haki sawa kwa nchi zote za bonde la Mto Nile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, sasa namuita Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Azimio. Awali yote niseme tu kwamba na mimi mwenyewe naunga mkono Azimio hili.

La pili, nitoe shukrani za dhati kabisa kwa Kamati ya Kililmo, Mifugo na Maji kwa michango mizuri ambayo wameitoa ili kuboresha na ushauri huo wote niwaahidi tu kwamba sisi tutauzingatia. Niwashukuru sana Wabunge wote, kwa kweli sijaona Mbunge ambaye amekataa Azimio hili, kimsingi ni wote kabisa tunakubali Azimio hili lakini pia mmetoa maangalizo ambayo ni mazuri na sisi tunayapokea na tutaendelea kuyafanyia kazi huko mbele ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Profesa Mwandosya na Mawaziri wote ikiwemo Mheshimiwa Wasira na Mheshimiwa Edward Lowassa na Mawaziri wote waliopita ambao kwa namna moja au nyingine wametoa michango mingi sana mpaka leo hapa tumefikia sisi leo tunalishawishi Bunge tuweze kuridhia Azimio hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee niishukuru sana taarifa ya Kambi ya Upinzani kwa maana hapa sasa ni Tanzania kwanza sijaona mahali popote zaidi tu ya kutoa ushauri na ukurasa wa sita, ninukuu taarifa ya Kambi ya Upinzani, inasema:-

*"Kambi Rasmi ya Upinzani haipingani kabisa na Mkataba huu bali inapongeza kwani kipindi kirefu kumekuwa ni kilio cha baadhi ya nchi wanachama kuwa pindi watakapotumia maji ya Mto Nile wanakumbana na vitisho za nchi zilizokuwa na haki hii".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii imeturahisishia tu kwamba wao wenyewe Kambi ya Upinzani wanaridha na niahidi tu kwamba hayo maangalizo yote mliyotoa sisi tutayazingatia. Mimi nimshauri tu rafiki yangu Masoud ametoa wasiwasi wake lakini nimkumbushe pia hata sera na usemi wa CUF wa haki sawa kwa wote na asiyetaka haki…

**MBUNGE FULANI:** Aelimishwe.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Ndiyo, aelimishwe. Kwa hiyo, haki sawa ndiyo tunayoitafuta sasa katika Azimio hili. Kwa hiyo, ningeomba hiyo sera ya CUF ihamie katika Azimio hili kuwa na haki sawa na uwiano wa kutumia maji. Kwa hiyo, nikishukuru sana, naamini kabisa kwamba kwa msemo huo utakuwa umenielewa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niongeze tu kwa kusema kwa Azimio sisi tulikuwa tunatumia maji kidogo sana, kwa hiyo, baada ya Azimio hili na kuundwa chombo maana yake Tanzania itaongeza uwezo wa kutumia zaidi maji haya. Hili ninyi ni mashahidi kwamba likipita Azimio hili kukaundwa na chombo na sisi tutaendelea kuzishawishi nchi nyingine ziungane nasi ili miradi hii tunayoisema kila siku hapa tunajibu maswali, miradi ya Geita, Bukoba, Mwanza, unaenda mpaka Misungwi, Shinyanga tunataka kuleta maji Tabora, Nzega nitashangaa sana watu wakikataa kuunga mkono kwa sababu hii ndiyo itatupa sisi sasa fursa ya kuweza kuyatumia vizuri zaidi haya maji. Kwa hiyo, si kwamba kuridhia Azimio hili au kuna kitu gani kiko nyuma ya hili ni kwamba tutaongeza utumiaji wa maji kuliko ilivyo sasa. Kwa sababu kama alivyosema Mheshimiwa Wasira ni kwamba leo hii hata hayo tu tunayoyatumia sasa ilikuwa mbinde, lakini leo hii ukitaka kuendelea kuyatumia maana yake uombe kibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunataka kuondokana na mikataba hiyo ya enzi hizo, miaka 1929 na 1959 sasa tuko dunia nyingine kwamba tupate haki zaidi na uwiano wa kuweza kuyatumia haya maji na mimi naamini kabisa kwamba hata hii miradi tunayoilenga kuifanya tunaweza tukaitekeleza kwa ufanisi mzuri zaidi. Kwa hiyo, niwashawishi Wabunge wenzangu na mimi nimesimama sitaki kutumia nguvu nyingi sana kwa sababu nimeona kabisa kwenye taarifa ya Upinzani, kwenye kuongea mmojammoja, mimi niseme tu kwamba nami naunga nanyi,

niwashawishi tu kwamba kwa pamoja turidhie Azimio hili. Faida zimeshaongelewa, baada ya kuanzishwa kwa Kamisheni tutafaidika na jambo gani, yote yako wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwa kweli sina la kuongea zaidi, naunga mkono hoja na mengine mengi Waziri atakuja kuyasema, nawashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa naomba nimuite Mheshimiwa Waziri Mtoa Hoja.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nikushukuru sana kwa jinsi ambavyo umetuongoza katika kikao chetu cha leo hususan katika muda huu wa mchana ambapo tumejadili Azimio hili la Ushirikiano katika Bonde la Mto Nile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao na nataka niseme kwamba michango ambayo imetolewa ni michango ambayo kila mtu ametoa akiwa anasema kutoka moyoni mwake kwamba ni kitu ambacho ni muhimu na kwamba lazima tuwe makini katika kutekeleza Mkataba huu. Napenda pia nishukuru sana mchango wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji katika uwasilishaji wa Azimio hili. Maoni yao unaweza kusema yalikuwa *very comprehensive,* waliangalia Azimio hili kwa ujumla na wameleta mapendekezo ambayo sisi katika Serikali tunayapokea na tunayakubali na tutayatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nirudi nyuma kwamba wakati Serikali ilipowasilisha Azimio hili kwenye Kamati, Kamati pia ilikuwa imeita wadau aina mbalimbali ambao wengine walitufundisha kabisa maana walishiriki katika majadiliano ya kuandaa Mkataba na makubaliano haya. Kwa hiyo, napenda niishukuru Kamati yetu kwa kazi nzuri sana ambayo walifanya. Aidha, Kamati hii pia ilikubali kwenda mpaka Sudani na kutembelea mifumo ya Mto Nile kule na kuangalia ni jinsi gani wenzetu wanavyotumia mto ule na kutoa mawazo mengi ambayo Serikali imefurahi sana kuyapokea na nataka niwaahidi kwamba tutayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuzingatia maoni ya Kamati, napenda nitoe maoni katika maeneo machache. La kwanza, suala la maoni ya Kamati kwamba Serikali ijiandae vizuri kutayarisha wataalam kushiriki katika uendeshaji wa hii Kamisheni, hili ni wazo zuri na sisi tumeanza kujiandaa na kuandaa wataalam ili waweze kushiriki katika uendeshaji wa Kamisheni hii. Aidha, kwa sababu wafanyakazi katika Kamisheni hizi wanafanya kazi za muda, tutaishauri Serikali iweze kuwapokea wakirudi ili kutoa motisha ya wafanyakazi wengi zaidi kwenda kushiriki katika kazi hizi na hivyo kufaidika kama Tanzania kwa ajira zinazotokea katika Kamisheni hii lakini pia kutuletea mchango wa kitaalam katika kuendesha mambo yetu ya ndani. Nakubaliana na Kamati pia kwamba ni muhimu sana tujenga umahiri katika uendeshaji wa maji shirikishi kwa sababu katika mabonde yetu tisa hapa nchini, mabonde saba, yote ni mabonde ya maji shirikishi, kwa hiyo, ni muhimu sana sisi tujenge umahiri katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na *concern* katika mchango wa Kamati na pia alieleza suala hili Mheshimiwa Gekul kwamba Wakuu wa Nchi wasitunge sera. Napenda kusoma huu Mkataba wenyewe unasema:-

*"The conference of Heads of States and Government. The structure and procedures. The conference of Heads of States and Government, shall be composed Head of States and Government on Nile basin state and the conference shall establish its own rules and procedures. Functions, the conference shall be the supreme policy making organ of the commission."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kama watakaa pale kutengeneza sera, sera itatengenezwa lakini upitishaji wa sera na mwelekeo wa sera utawekwa na Wakuu wetu wa Nchi kama wao ndiyo *supreme body* katika makubaliano haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji wa Kambi ya Upinzani amejibiwa vizuri na Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa sababu hiyo, nitasema tu kwamba katika makubaliano haya tumeweka vifungu vinaonyesha kwamba theluthi mbili ya wanachama wakishaupitisha huu mkataba basi Tume itaanzishwa na Tume itakapoanzishwa itaongea na Mataifa yale ambayo hayajaweka saini ili katika kipindi cha miezi sita hili liweze kufikiwa. Nataka nieleze kwamba dalili zote zinaonyesha kwamba hata Misri iko njiani kurudi kwa sababu ni hivi juzi tu nchi ya Misri, Sudani na Ethiopia zilikutana na kukubaliana juu ya uendeshaji wa *Grand Renaissance Dam* ya Ethiopia yaani hili bwawa kubwa ambalo linasemwa na makubaliano yale nimesoma tafsiri yake ya Kiingereza japo siyo tafsiri rasmi lakini inaonyesha kwamba hivi vifungu vya kutoathiri wengine katika utumiaji wa maji vimo mle katika makubaliano yale na katika mkutano wetu wa mwisho wa Mawaziri, Waziri wa Misri ambaye huko nyuma alikuwa haudhurii naye aliudhuria mkutano huo. Kwa hiyo, tunayo matumaini makubwa kwamba wote watakuwa wanashiriki baada ya hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Hilda Ngoye kwa mawazo aliyotoa, ni kweli kwamba Tanzania ingekuwa ya kwanza kuweka saini katika mkataba huu lakini kila nchi ina utaratibu wake wa kuridhia mikataba, nchi zingine uridhiaji unafanywa na Baraza la Mawaziri, nchi zingine Mkuu wa nchi akishakubali inatosha lakini kwetu lazima tulete Bungeni na kwa sababu hiyo utaratibu wetu unachukua muda zaidi ya utaratibu katika nchi zingine. Hata hivyo, sisi ni watatu na katika suala hili hatujachelewa katika kupitisha Azimio hili.

Mheshimiwa Gekul, nadhani yako mambo ya msingi ambayo hakuyaelewa na nadhani labda hajasoma mkataba wenyewe na ndiyo maana alisikitika sana kwamba tunaupitisha. Kwa miaka yote hii mikataba iliyokuwepo ilikuwa inatukataza tusitumie maji ya Mto Nile. Mkataba huu unazipa nchi haki ya kutumia kwa uwiano kutegemea na kiwango cha maji ambacho wewe mwenyewe unatoa na wewe utaweza kutumia kwa kuelekea uwiano huo.

Kwa hiyo, hiki tunachopitisha hapa ndiyo kusahihisha matatizo aliyokuwa anayataja Mheshimiwa Gekul na nadhani atakaporudi nyumbani akasoma makubaliano haya ataelewa na kutupigia makofi akiwa nyumbani.

Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa na Profesa Mwandosya walieleza vizuri hii *Nyerere Doctrine of State Succession* na hii *Doctrine* imetumiwa hata kwenye Mikataba ya Umoja wa Mataifa ya ushirikiano katika masuala ya maji.

Mheshimiwa Masoud, nimesikia *concern* zako lakini nimeshangaa kwamba umesoma makubaliano ya juzi ya Sudani na Ethiopia na Misri lakini bado ukawa na wasiwasi ambao umeueleza hapa. Ningekushauri usome zaidi ule Mkataba, usome na Mkataba huu na uone *goodwill* ambayo iko humu ndani na nina uhakika utatuunga mkono katika jambo hili.

Mheshimiwa Selemani Kakoso, amesisitiza sana baada ya kuridhia Mkataba huu basi tuweze kuendelea kupanua matumizi ya maji ya Mto Nile. Nataka nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Kakoso kwa kuelezea hapa kwenye Katiba yetu hii Inayopendekezwa ambayo katika Ibara ya 51(1) inasema kila mtu ana haki ya kupata huduma ya afya na maji safi na salama. Mamlaka ya nchi itahakikisha kwamba huduma zilizorejewa katika Ibara ndogo ya (1) zinapatikana kwa urahisi kwa kuzingatia mahitaji ya nchi na rasilimali zilizopo.

Sasa kwa kuridhia Mkataba huu tunaweza kuchukua maji zaidi kutoka kwenye mfumo wa Mto Nile na mipango yetu kama ambavyo tulijibu maswali katika Bunge hili Serikali imepata msaada, inachukua maji ya Ziwa Victoria na kuyapeleka mpaka Nzega hadi Tabora na Igunga na kuvipa vijiji vyote ambavyo viko njiani maji safi na salama. Katika kufanya hivyo, nimetoa maagizo kwamba Mhandisi Mshauri aendelee na usanifu wa bomba la maji kutoka Tabora mpaka Sikonge na kuwapa watu wa hapo Sikonge maji ya Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tunafanya usanifu sasa wa kuchukua maji ya Ziwa Victoria katika eneo la Magu na kuyapeleka Bariadi, Langabili, Maswa mpaka Meatu na tutaangalia uwezekano wa kuyapeleka zaidi mpaka kufika Singida kutegemeana na hali ilivyo. Mimi nimetoka Ukanda wa Ziwa wiki iliyopita, ukiona ukame ulioko kule na fursa ambazo zinatolewa na Mkataba huu, ni muhimu sana na mimi nawaomba Waheshimiwa Wabunge tukubaliana na Mkataba huu ili tuweze kuokoa wakulima wetu ambao wanapata ukame huku maji yako karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wa Maji ambao wamenitangulia na nipende kushukuru mchango uliotolewa na Mheshimiwa Stephen Wasira na mchango alioutoa Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya. Katika ukanda wetu, Mheshimiwa Profesa Mwandosya ametajwa kama *authority* katika jambo hili. Napenda pia tukumbuke mwaka 2002 wakati ambapo Mheshimiwa Edward Lowassa akiwa Waziri wa Maji na wakati Mkataba huu ulipokuwa unajadiliwa kabla haujafika hatua hii alikwenda Misri kuwaeleza Wamisri kwamba Tanzania itachukua maji ya Ziwa Victoria kuyaleta Kahama na kuyaleta Shinyanga na hata ikibidi kuyapeleka mbele ya hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ningependa sana nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa ambaye naye alishiriki katika majadiliano haya. Kama alivyosema Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Mheshimiwa Rais wetu alikuwa mstari wa mbele katika mikataba hii na hasa wakati akiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Kazi hii imefanywa na Watanzania wengi, napenda kwa ajili ya muda niwashukuru wote kwa ujumla kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu lizingatie Mkataba huu na kuupitisha kama tulivyoomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*
*(Azimio la Makubaliano ya Msingi ya Ushirikiano katika Bonde la Mto Nile (Agreement on the Nile River Basin Co-operative Framework – CFA liliridhiwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Wote wameafiki, nakushukuru sana na kukupongeza Mheshimiwa Waziri kwa Azimio hili na najua kweli nchi yetu itanufaika na Mikoa yote iliyo kando ya Ziwa Victoria na hasa Mkoa wa Mara ambao unakabiliwa na ukame wa mara kwa mara pia uweze kunufaika na maji haya.

Nimepokea malalamiko Wabunge wanalalamika kwamba humu ndani kuna baridi kali na matokeo yake wanashindwa kuhimili hiyo baridi inabidi watoke nje kwenda kantini kunywa

chai, wakirudi humu baridi inazidi. Kwa hiyo, naomba wahusika kesho warekebishe huo mfumo wa baridi. *(Makofi)*

Baada ya hayo, sasa naomba kuahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.22 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 27 Machi, 2015, Saa Tatu Asubuhi)*